# UGATUZI WA UTAMADUNI WA KIKOLONI KATIKA TAMTHILIA ZA NGUGI WA THIONG'O

NA

NG'ANG'A SAMUEL IRUNGU

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

IDARA YA ISIMU NA LUGHA

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0271743 7

JUNI 2006

JOMO KENYATTA MEMORIAL
LIBRARY

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa minajili ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

.................................................... 23/10/2006

NG'ANG'A SAMUEL IRUNGU

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa na sisi tulioteuliwa na chuo kuisimamia.

....................................................

Dkt. K. W. WAMITILA

(Msimamizi)

.................................................... 23.10.06

Bw. HEZRON MOGAMBI

(Msimamizi)

## TABARUKU

Kwanza, kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na siha. Pili, kwa wazazi wangu wapendwa, Bw. Amos Ng'ang'a na Bi. Fridah Waithira kutokana na huba yao kwangu na kwa kunilea. Tatu, kwa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunipa ufadhili wa kimasomo katika Shahada ya Uzamili.

**YALIYOMO** **KURASA**


Ikirari ........ ii

Tabaruku ........ iii

Shukrani ........ vii

Muhtasari ........ ix

Orodha ya Vifupisho Vilivyotumiwa ........ x

**SURA YA KWANZA**

1.0 Usuli wa Tasnifu ........ 1

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ........ 3

1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 4

1.4 Nadharia Tete ........ 4

1.5 Sababu za Kuchagua Somo Hili ........ 4

1.6 Msingi wa Kinadharia ........ 5

1.7 Upeo na Mipaka ........ 16

1.8 Fasili ya Istilahi Zilizotumiwa ........ 16

1.8.1 Baada-ukoloni ........ 17

1.8.2 Ubaada-ukoloni ........ 17

1.8.3 Upinduzi ........ 17

1.8.4 Utovulaya ........ 18

1.8.5 Usemi ........ 18

1.8.6 Taswira potofu\ Taswira Dufu ........ 18

1.8.7 Utamaduni wa Kitaifa ........ 18

1.9 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili ..... 18

1.10 Njia za Utafiti ..... 23

Tanbihi ..... 24

**SURA YA PILI**

2.0 FASIHI, UKOLONI, UBAADA-UKOLONI NA UTAMADUNI ..... 25

2.1 Utangulizi ..... 25

2.2 Fasihi na Utamaduni ..... 25

2.3 Fasihi na Ukoloni/Ubaada-ukoloni ..... 28

2.4 Fasihi na Lugha Katika Fasihi ya Baada-ukoloni ..... 31

2.5 Hitimisho ..... 37

Tanbihi ..... 38

**SURA YA TATU**

3.0 UGATUZI KATIKA TAMTHILIA ZA *MTAWA MWEUSI* NA *KESHO WAKATI KAMA HUU* ..... 39

3.1 Utangulizi ..... 39

3.2 Misingi ya Ugatuzi ..... 39

3.3 Kuhusu Kazi Husika ..... 40

3.3.1 Muhtasari wa Tamthilia ya *Mtawa Mweusi* ..... 40

3.3.2 Muhtasari wa Tamthilia ya *Kesho Wakati Kama Huu* ..... 43

3.4 Mikakati ya Ugatuzi ..... 45

3.4.1 Maelezo ya Kiethnografia ..... 45

3.4.2 Lugha na Fasihi ya Baada-ukoloni ..... 53

3.4.3 Fasihi Simulizi Katika Fasihi ya Baada-ukoloni ..... 56

3.4.4 Uandishi Tena wa Historia Katika Fasihi ya Baada-ukoloni ..... 59

3.4.5 Uhusika na Mandhari Katika Fasihi ya Baada-ukoloni ..... 61

3.5 Hitimisho ..... 65

Tanbihi ..... 66

**SURA YA NNE**

4.0 UGATUZI KATIKA TAMTHILIA ZA *MZALENDO KIMATHI* NA *NITAOLEWA NIKIPENDA* .......... 67

4.1 Utangulizi .......... 67

4.2 Kuhusu Kazi Husika .......... 67

4.2.1 Muhtasari wa Tamthilia ya *Mzalendo Kimathi* .......... 67

4.2.2 Muhtasari wa Tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* .......... 70

4.3 Mikakati ya Ugatuzi .......... 74

4.3.1 Maelezo ya Kiethnografia .......... 74

4.3.2 Lugha na Fasihi ya Baada-ukoloni .......... 82

4.3.3 Fasihi Simulizi Katika Fasihi ya Baada-ukoloni .......... 85

4.3.4 Uandishi Tena wa Historia Katika Fasihi ya Baada-ukoloni .......... 90

4.3.5 Mandhari na Uhusika Katika Fasihi ya Baada-ukoloni .......... 94

4.4 Hitimisho .......... 97

**SURA YA TANO**

5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .......... 99

5.1 Utangulizi .......... 99

5.2 Mjadala na Maoni .......... 99

5.3 Mapendekezo ya Utafiti .......... 102

**MAREJELEO** .......... 104

**SHUKRANI**

Kukamilika kwa utafiti huu ni matokeo ya juhudi za watu wengi ambao sina budi kuwajibika kuwapa shukrani zangu za dhati. Kwanza, nawashukuru wasimamizi wangu ambao walipata wakati wa kusoma kazi yangu, kunielekeza na kunishauri katika kila hatua ya kazi hii. Wao ni Dkt. Wamitila aliyenifungulia pia milango ya maktaba yake ya kibinafsi yenye vitabu adimu na Bw. Hezron Mogambi kwa kuwepo nilipohitaji mengi kutoka kwake. Vilevile, nawashukuru wazazi wangu: babangu, Amos Ng'ang'a na mamangu, Fridah Waithira, pamoja na ndugu zangu wote kwa uvumilivu wao na kwa kunihimiza nisome.

Aidha nawashukuru Dr. D.H. Kiiru, mwenyekiti wa Idara ya Fasihi, Chuo Kikuu cha Nairobi na Bi. Margaret Njuguna kwa kuniandikia barua aali za kiwasifu nilipokuwa nikituma maombi ya kusomea Shahada ya Uzamili kwa Halmashauri ya Shahada za Juu katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Pia mwenyekiti wa Idara ya Isimu na Lugha wa wakati huo Profesa Kithaka wa Mberia namshukuru kwa msaada alionipa nilipoonyesha ari ya kusomea Shahada ya Uzamili. Namshukuru pia mwenyekiti wa sasa, Dkt. Mwenda Mbatia, sio tu kwa kunifunza na kwa kuiandikia barua Halmashauri ya Shahada za Juu ya Chuo Kikuu cha Nairobi kuiuliza iendelee kunifadhili kimasomo katika mwaka wa pili, bali pia kwa kunipa mwongozo wa awali na kunihimiza niendelee na utafiti huu nilipotafuta ushauri kutoka kwake. Namshukuru pia Dkt. Mbuthia kwa msaada wa vitabu na pia ushauri alionipa katika hatua za awali za utafiti huu.

Natoa shukrani zangu pia kwa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunifadhili kimasomo katika kipindi kizima cha kusomea Shahada ya Uzamili.

Vilevile, wahadhiri wafuatao wapokee shukrani zangu za dhati kwa kunifunza katika kozi mbalimbali: Profesa Abdulazizi, Dkt. Habwe, Dkt. Kineene, Dkt. Olali, Dkt. Buregeya, Bw Mungania na Bw. Ayub Mukhwana. Pia nawapa shukrani zangu wanafunzi tuliosoma nao na kuhimizana masomoni, Elizabeth Katola na Esther Muli. Aidha, kwa mwandani na mwanafunzi mwenzangu Winstone Jacktone Nyonje, kazi hii

haingekamilika bila mijadala ya kiakademia iliyoibuka mara kwa mara bila kupangiwa. Pia nawashukuru marafiki Julius Gichamba na Bitugi Matundura kwa kuniauni kwa mengi na hasa vitabu vya maktaba zao za kibinafsi.

Aidha, nawashukuru wafanyakazi wa maktaba za *Jomo Kenyatta Memorial Library, British Institute of Eastern Africa* na *Institute Francais de Recherche en Afrique (IFRA)* walionihudumia katika somasoma zangu. Na mwisho nawashukuru Racheal Maina, Justus Musau na Stella Ndunge kwa kuipiga chapa kazi hii. Kwa wote mlionisaidia katika utafiti huu na ambao majina yenu sikuyakumbuka zipokeeni shukrani zangu.

Hata hivyo, makosa yatakayopatikana katika kazi hii ni yangu mwenyewe.
Ahsanteni.

# MUHTASARI

Tahakiki nyingi za kazi za kifasihi za Kiswahili ambazo zimefanywa kuhusiana na ukoloni na ukoloni mambo-leo zimejikita katika nadharia ya U-Marx. Tahakiki za aina hiyo hubakia kuangazia suala la uhusiano wa kiuchumi kama kitovu cha harakati za ukoloni na ukoloni mambo-leo. Kwa namna hiyo mahusiano ya kitamaduni katika miktadha hiyo hufumbiwa macho. Utafiti huu ulitiwa chachu na ukweli huo pamoja na kwamba ukoloni wa kitamaduni ulitangulia ule wa kiuchumi. Ni kupitia kwanza kuwatawala watu kitamaduni ambapo kuwaondoa kutoka kwa mfumo wao wa kiuchumi (waliouzoea) hadi katika mfumo mpya wa kiuchumi (wa watawala) huwezekana.

Utafiti huu umezishughulikia tamthilia za Ngugi wa Thiong'o kwa kuzingatia ukweli huo. Katika sura ya kwanza, masuala ya kimsingi kuhusiana na utafiti yameshughulikiwa. Haya ni utangulizi, tatizo la utafiti, nadharia tete, madhumuni, msingi wa kinadharia, upeo na mipaka, fasili za istilahi zilizotumiwa kwa muktadha wa utafiti huu na yaliyoandikwa kuhusiana na somo hili.

Sura ya pili imeshughulikia masuala ya lugha, fasihi, utamaduni, ukoloni na ubaada-ukoloni. Upembuzi wa kina umefanywa katika kubainisha uhusiano uliopo kati ya dhana hizo. Sura hii imeyaangazia masuala ya kimsingi kuhusiana na nadharia ya baada-ukoloni vilevile.

Sura ya tatu na ya nne nazo zimeshughulikia uhakiki wa kazi husika. Sura ya tatu imeshughulikia tamthilia za *Mtawa Mweusi* na *Kesho Wakati Kama Huu* huku sura ya nne ikishughulikia tamthilia za *Nitaolewa Nikipenda* na *Mzalendo Kimathi.*

Mwishowe katika hitimisho, mapengo, mapendekezo na masuala muhimu ya ubaada-ukoloni kuhusiana na tamthilia zinazoshughulikiwa yanayoibuka katika uhakiki yameangaziwa.

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA

Uk. - Ukurasa

Taz. - Tazama

Khj. - Kama hapo juu

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Usuli wa Utafiti

### 1.1 Utangulizi

Umuhimu wa fasihi tafsiri katika lugha yoyote ile hauwezi kupuuzwa katika uhakiki wa fasihi yake. Fasihi tafsiri huchangia katika kuikuza lugha husika na fasihi yake (Gromova 2004, Zaja 1986). Umuhimu huo hauwezi kugunduliwa pasipo kufanyiwa uhakiki kazi zilizotafsiriwa.

Fasihi ya Kiswahili imepokea kazi nyingi za kifasihi kutoka lugha nyingine kupitia tafsiri, katika tanzu zake zote za fasihi yake. Hata hivyo, ni tahakiki chache ambazo zimefanywa kuonyesha mchango wa kazi hizo. Katika lugha ya Kiswahili, mara nyingi kazi hizo hutajwa tu ama katika historia ya fasihi ya Kiswahili au kwa namna isiyoonyesha kueleweka kwa mchango wa kazi husika katika fasihi ya Kiswahili.

Kazi yoyote ya kifasihi inapotafsiriwa huwa sehemu ya fasihi ya lugha pokezi na ni muhimu wahakiki wa fasihi ya lugha hiyo waihakiki ili kutoa thamani yake kifasihi. Kwa mfano, sehemu kubwa ya fasihi ya lugha ya Kiingereza ni ya fasihi tafsiri. Kwa mfano, kazi za waandishi maarufu kutoka lugha nyingine kama; Bertolt Brecht (Kijerumani), Yevtushenko Yevegeny (Kiurusi), Henrik Ibsen (Kinorwe), Neruda Pablo (Kihispania), Eugene Ionesco (Kirumania), Anton Chekhov (Kiurusi) na wengine wengi zimekuwa sehemu ya fasihi ya lugha ya Kiingereza. Kazi hizo zimeendelea kufanyiwa uhakiki na wahakiki wa fasihi kwa lugha ya Kiingereza.

Vivyo hivyo, wahakiki wa fasihi ya lugha ya Kiswahili hawana budi kuzihakiki kazi zilizotafsiriwa katika lugha yake kama njia ya kukuza lugha hiyo na fasihi yake (Kimaudhui na Kifani). Utafiti huu unadhamiria kuziangizia tamthilia za Ngugi wa Thiong'o zilizotafsiriwa hadi katika lugha ya Kiswahili. Ngugi ni mwandishi wa fasihi ambaye umaarufu wake umedhihirika katika tanzu za riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Hata hivyo, ni katika uandishi wa riwaya anapojulikana zaidi. Aidha, hii ni kutokana na umaarufu wa riwaya kama utanzu.

Katika uandishi wake, Ngugi hushughulikia masuala ya athari za ukoloni katika bara la Afrika na hasa nchini Kenya. Kimsingi, fasihi andishi ya Afrika Mashariki [kama zilivyo fasihi za jamii zilizotawaliwa kikoloni] iliibuka kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kitamaduni yaliyoletwa na ukoloni na ukoloni mamboleo (Wanjala, 1978: vii). Fasihi hii basi ni uitikio wa hali ya migongano na mitafaruku iliyoletwa na ukoloni. Maingiliano ya kitamaduni yaliyoletwa na ukoloni yalizua hali changamano katika jamii zilizotawaliwa kikoloni. Hasa katika Afrika Mashariki, utamaduni wa Kiulaya ulilazimishiwa watawaliwa. Hali hii ilidhalilisha utamaduni wa Waafrika wa eneo hili.

Utafiti huu unadhamiriwa kuchunguza namna ambavyo mwandishi huyu, kama mwandishi wa fasihi ya baada-ukoloni, anavyoumbua utamaduni wa kikoloni kwa kuugatua na mbinu anazozitumia kutekelezea hilo. Katika ukoloni, utamaduni wa Kiulaya ulitukuzwa kama kitovu huku tamaduni nyingine zikirejelewa kama za kishenzi na duni zilizohitaji kutupiliwa mbali. Ugatuzi katika fasihi ya baada–ukoloni huwa mradi wa kuvunjilia utovulaya *(eurocentrism)* kama njia ya kuupinga ukoloni wa kitamaduni.

Chinweizu na wengine (1980), Liyong (1969), na Ngugi (1986, 1993) wanaeleza kuwa jukumu la ugatuzi wa utamaduni wa kikoloni ni la mwandishi wa fasihi ya baada–ukoloni. Ugatuzi huo ni njia ya kuelewa mchakato uliotumiwa kuzidhalilisha tamaduni za watawaliwa katika ukoloni. Aidha, ni njia ya kuzipa tamaduni za waliotawaliwa kikoloni uhai tena. Hiyo ndiyo njia ya kuikomboa fasihi ya watawaliwa kuwapa msingi wa kujiendeleza upya baada ya ubeberu wa miaka mingi. Vilevile, ni namna ya kuikolonishua fasihi ya jamii zilizotawaliwa kikoloni.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu unahusu majaribio ya Ngugi wa Thiong'o katika tamthilia zake kuugatua utamaduni wa kikoloni/Kiulaya na kujenga utamaduni wa kitaifa. Hapa dhana ya utamaduni wa kitaifa inatumiwa kwa namna anavyoifasili Fanon (1963:166). Maana yake ni juhudi za pamoja za wanajamii (waliotawaliwa kikoloni) katika fani ya kiakili za kuelekeza, kutetea na kutukuza matendo ambayo kupitia kwayo jamii yao imejijenga. Katika kuikolonishua fasihi ya Kiafrika, Chinweizu na wengine (1980:1) wanaeleza kwamba wajibu uliopo kwa mwandishi wa fasihi ya Kiafrika ni kumaliza hali ya kutawaliwa kwa utamaduni wa Kiafrika na utamaduni wa kigeni, kuondoa fikra zote za kikoloni na utumwa ili kuweka misingi mipya ya Afrika huru ya kisasa.

Tafsiri na fasiri katika fasihi ni mbinu zinazopendekezwa katika kuhakikisha tamaduni na fasihi za jamii za ulimwengu zinahusiana na kuingiliana katika hali huru (Wa Thiong'o, 1993: 10 – 11). Hivyo kila fasihi, ikiwa bado inahifadhi utambulisho wake wa lugha ya jamii yake iakisi pia mikondo mingine ya fasihi kupitia tafsiri.

Mambo yanayochunguzwa kuhusiana na suala hili ni kama vile: ugatuzi wenyewe na mikakati anayoitumia Ngugi kuugatua utamaduni wa kikoloni. Mintarafu hii swali linalotafutiwa jawabu ni:

Ni kwa namna gani, Ngugi wa Thiong'o kama mwandishi wa fasihi ya baada-ukoloni anavyougatua utamaduni wa kikoloni?

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu unalenga:

i) Kuchunguza namna Ngugi wa Thiong'o, kupitia tamthilia zake, anavyouumbua utamaduni wa kikoloni kwa kuugatua.

ii) Kuchunguza namna tamthilia za Ngugi zinavyoakisi uandishi wa fasihi ya baada–ukoloni kupitia ugatuzi.

### 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu unaongozwa na nadharia tete kwamba:

i) Tamthilia za Ngugi zinauumbua utamaduni wa kikoloni kwa kuugatua.

ii) Tamthilia za Ngugi zinaakisi uandishi wa fasihi ya baada-ukoloni.

### 1.5 Sababu za Kuchagua Somo Hili

Uchaguzi wa somo hili unatokana na sababu kuu mbili. Kwanza, hakuna utafiti mwingine uliowahi kufanywa kubainisha kwamba tamthilia za Ngugi wa Thiong'o ni harakati ya kuugatua utamaduni wa kikoloni. Aidha, nadharia ya baada-ukoloni haijatumiwa katika

tafiti ambazo zimeshafanywa kuhusiana na tamthilia za mwandishi huyu kama itakavyojitokeza katika sehemu ya kazi zilizoandikwa kuhusiana na utafiti huu.

Pili, katika fasihi ya Kiswahili, Ngugi wa Thiong'o kama mwandishi ambaye tamthilia zake zimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili (ni sehemu ya fasihi ya lugha hiyo) hajaangaziwa ili kuukadiria mchango wake. Hivyo, utafiti ambao utaangazia ujumla wa tamthilia zake unahitajika.

Kwa kuzingatia masuala haya, utafiti huu unatarajiwa kutoa mchango kwa mtalaa wa fasihi ya Kiswahili na nyongeza kwa utafiti wa jumla kuhusu kazi za Ngugi wa Thiong'o ambao tayari umefanywa na wahakiki wengine.

## 1.6 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya baada-ukoloni. Nadharia ya baada-ukoloni hushughulikia uhakiki wa fasihi za jamii za mataifa yaliyotawaliwa kikoloni au zinazoendelea kupata athari za ukoloni au fasihi ambazo zimeandikiwa katika mataifa yaliyotawala mataifa mengine kikoloni zinazoshughulikia suala la ukoloni au watu waliotawaliwa kikoloni (Lyre, 1997). Kuhusiana na istilahi baada-ukoloni, Ashcroft na wengine (2002: 2) wanaeleza:

> *Istilahi baada-ukoloni hutumiwa kujumlisha tamaduni zote zilizoathiriwa na mchakato wa ukoloni kutoka wakati wa ukoloni hadi sasa.*
>
> *(Tafsiri yangu)*

Pamoja na ukoloni mkongwe, maelezo haya yanazingatia kuendelezwa kwa ukoloni kwa sura ya ukoloni mambo-leo na mataifa ya Ulaya katika mataifa ya Ulimwengu wa Tatu hata baada ya uhuru wake. Nadharia ya baada-ukoloni ni tahakiki ya uhusiano baina ya Ulaya na "Wengine" pamoja na uhusiano wa kikoloni wenyewe. Nadharia hii hulenga kuwapa sauti watawaliwa wa ukoloni kupitia kuelewa na kuhakiki miundo ya ukandamizaji iliyotumiwa na inayotumiwa katika ukoloni na ukoloni mambo-leo.

Kuna madai yanayotofautiana kuhusu nadharia hii ilipoanzia lakini Edward Said ndiye anayerejelewa sana kuwa mwasisi wa nadharia hii katika kazi yake maarufu ya *Orientalism* (1978). Katika kazi hii Said, anaonyesha mchakato mzima uliotumiwa na wakoloni wa eneo la Mashariki: Uingereza, Ufaransa na baadaye Marekani wa kujenga taswira potofu za Mmashariki, Mashariki na mitalaa ya Umashariki ili kuyafikia maslahi yao. Dhana hizi haziwakilishi uhalisi kuhusiana na Mashariki. Said anapendekeza mbinu za kukosoa upotoshi huo uliofanywa na ukoloni (Said, 1978: 20-36).

Tahakiki ya Edward Said ya seti ya 'imani" inayorejelewa kama Umashariki (orientalism) huunda usuli muhimu katika mitalaa ya baada-ukoloni. Kazi yake huangazia na huchunguza upotoshi uliokitwa mizizi na ukoloni katika chukulizi nyingi huku ikihoji baadhi ya mawazo yanayokubaliwa katika viwango vya kibinafsi, kiakademia na kisiasa.

Kulingana na kazi ya Said, Mashariki (The Orient) huwakilisha mfumo wakilishi ulioundwa na kani za kisiasa zilizoiweka Mashariki katika usomi wa Kimagharibi,

urazini wa Kimagharibi na himaya ya Kimagharibi. Mashariki hivyo huwepo kwa sababu ya Magharibi na iliundwa na Magharibi kutoka kwa mkabala wa Kimagharibi.

Hivyo, inajitokeza kuwa Umashariki ni namna ya uakisi fulani wa Mashariki (usiozingatia uhalisi wa Mashariki) unaowakilishwa kama mfumo mzima wa kimawazo na kiusomi. Kwa kuzingatia fasiri hizo za Umashariki na Mashariki basi Mmashariki (The Oriental) ni mtu anayewakilishwa na mfumo wa kimawazo wa Umashariki. Mtu huyo huonyeshwa akiwa na sifa za udhaifu wa kike lakini anayehatarisha maslahi ya Kimagharibi. Hapa pana usebusebu. Hivyo, Mmashariki ni mtu aliyelimbikiziwa sifa za kijumla za kuuridhisha ukoloni wa Kimagharibi pamoja na taswira dufu.

Wanamuundo-leo wameiangazia historia ya tafsiri katika fasihi ya baada-ukoloni. Gayatri Spivak, kwa mfano, ameshughulikia athari za kiitikadi katika fasihi tafsiri katika mataifa ya Ulimwengu wa Tatu na upotoshi unaofanywa katika utaratibu wake (katika, Munday, 2001: 133). Hivi tafsiri ilitumiwa kama asasi ya kikoloni. Fasihi za kikoloni zilizodhalilisha mtawaliwa zilitumiwa kulazimisha na kuzamisha akilini mwake itikadi zilizoendeleza ukoloni. Hasa Fasihi za Kiusafiri za wasomi wa Kimagharibi waliozitalii nchi za watawaliwa, ziliwaonyesha kama watu duni na wenye tamaduni za kishenzi wakilinganishwa na tamaduni za Kimagharibi. Mathalan, tafsiri kama: *Kiini cha Giza (Heart of Darkness)* yake Joseph Conrad inawafasiri Waafrika, Wakongo kwa namna hasi.

Kutokana na upembuzi huu basi, ni sahihi kudai kwamba kutafsiriwa kwa kazi za Ngugi katika Kiswahili (lugha ya watawaliwa) ni mkakati wa kupindua asasi ya tafsiri na kisha kuitwaa ili itumikie watawaliwa katika kujigundua kinyume na ilivyotumiwa katika ukoloni, kuwadhalilisha.

Aidha, nadharia ya baada-ukoloni imejengeka katika dhana ya "Wingine". Homi Bhabha (1983) katika makala yake ya *"The Other Question"* anaiangalia dhana ya Wingine kama mtalaa wa ukoloni. Anachunguza jinsi utaratibu wa kumuumba mtawaliwa kama mtu wa aina nyingine (aliye tofauti na mkoloni mwenyewe) ulivyoratibiwa. Hali hii ndiyo iliyomsukumia na kumuengua mtawaliwa hadi katika nafasi ya pembezoni katika nyanja zote za maisha na hasa katika utamaduni huku ukimtukuza mkoloni kama kitovu cha mambo yote.

Mitalaa ya Kimagharibi hasa anthropolojia na ethnografia ilitumiwa kukita upotoshi huo mizizi. Baadaye hata sanaa ilijumuishwa katika utaratibu huo na hasa fasihi. Fasihi ya Kiusafiri ya wasafiri wa Kiulaya ilipania kufasili Ulaya kwa namna ya kuonyesha tofauti yake na "Wengine" (Loomba, 1998: 71).

Fasihi ya baada-ukoloni huchunguza uhusiano wa fasihi na ukoloni. Fasihi ilitumiwa katika kuujenga ukoloni kama anavyoeleza Fanon (katika Bhabha 1983: 46):

> *Katika kipindi cha awali katika utoto, mtoto katika ukoloni hukumbana na taswira potofu za kimbari na kiutamaduni katika bunilizi za watoto, ambapo mashujaa weupe na mashetani weusi huwa kirejeleo cha ujitambulishi wa kiitikadi na kinafsi.* *(Tafsiri yangu)*

Mitalaa ya lugha ya Kiingereza na fasihi yake zilitumika kama asasi za kikoloni. Asasi hizi zilitumiwa kukengeusha mtawaliwa kutokana na utamaduni wake. Hata hivyo, kama anavyoeleza Bhabha (katika Loomba, 1998: 89-90) hali hiyo ya mkoloni kutaka kujirudufu katika nafsi ya mtawaliwa haikufaulu. Hali ya kutaka aigwe na mtawaliwa haikufaulu kama ilivyo katika mawasiliano ambapo hayafaulu kwa asilimia mia. Kuna uwezekano wa mambo fulani kutompata msikilizaji kama ilivyokusudiwa na mtoa habari. Hivyo, watawaliwa wa kikoloni badala ya kubadilishwa na mchakato wa ukoloni na kuwa kama mkoloni, alitokea kuwa kiumbe ambaye si Mzungu (asilimia mia) wala si Mwafrika katika uasili wake. Hali hiyo ilisababishwa na ukweli kwamba muktadha wa mazingira ya utamaduni wa watawaliwa hayangewiana na utamaduni wa kigeni. Yalikuwa tofauti na mazingira ambayo utamaduni huo ulizaliwa.

Mintarafu hiyo, Bhabha anaeleza kwamba mamlaka ya kikoloni basi yaliishia kuwa na umahuluti na usebusebu[4] *(hybridity and ambivalence)*, hivyo kufungua nafasi kwa mtawaliwa kupindua mtalaa wa mtawala. Nafasi hii ni ya kumwezesha kuhoji "ukweli" uliojengwa na mkoloni kumhusu. Upembuzi huu unatuelekeza katika masuala muhimu yanayoshughulikiwa na nadharia hii. Ashcroft na wengine (2002:37) wanarejelea mikakati mikuu miwili ya nadharia ya baada-ukoloni. Mkakati wa kwanza ni wa kukataa amali na kategoria za utamaduni wa kibeberu, viwango vya kiujumi na namna ya umapokeo wake unaochukulia kuwepo kwa maana moja thabiti katika neno. Hii ni hatua ya kuikolonishua lugha. Mkakati wa pili unahusiana na unakamilisha mkakati wa kwanza. Mkakati huu unapendekeza lugha ya kikoloni ichukuliwe na itumiwe katika "kubeba mzigo wa tajriba ya utamaduni wa watawaliwa" (khj: 38).

Mkakati huu wa pili kuhusu lugha huchukua mielekeo miwili katika fasihi ya baada-ukoloni barani Afrika. Mwelekeo wa kwanza ulitiwa chachu na Chinua Achebe (Loomba, 1998: 91). Msimamo wake ni kuwa, kutokana na hali ya wingilugha barani Afrika na kuwepo kwa lugha ya Kiingereza iliyoletwa na ukoloni, fasihi za Kiafrika zinafaa ziandikwe kwa lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, hiki si Kiingereza sanifu bali ni Kingereza kilichofinyangwa ili kiweze kubeba tajriba ya utamaduni wa Kiafrika.

Msimamo wa pili nao ulitiwa chachu na Ngugi wa Thiong'o (1986: 20-21). Ngugi anaonyesha uhusiano wa lugha na utamaduni, kwamba lugha ya Kiingereza ndiyo iliyobeba utamaduni wa kikoloni. Hivyo, fasihi ya Waafrika katika lugha ya Kiingereza ni ya mabwanyenye ambao hawawezi kueleza hali ya umma mkubwa. Fasihi inayodhamiriwa kunufaisha umma mkubwa lazima iandikwe kwa lugha ya watawaliwa, kwani ndiyo wanayoielewa.

Mitazamo hii pamoja na hoja zake zinazopingana imetumiwa katika uandishi wa fasihi ya baada-ukoloni. Fasihi ya Kiswahili inajiweka katika msimamo unaotetewa na Ngugi. Aidha, Ayi kwei Armah (katika Mulokozi, 2000: 76) anaunga mkono matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kuleta utambulisho na umoja wa Kiafrika. Hivyo, fasihi za ulimwengu zitafsiriwe katika lugha ya Kiswahili na kisha katika lugha nyingine za Kiafrika. Hivi Waafrika wengi wataweza kuzisoma na kuzinduka kwa kuona namna wanavyowakilishwa hasa katika fasihi za Kiulaya. Utetezi wa kukiinua Kiswahili kama

lugha ya Waafrika (watawaliwa) unaungwa mkono pia na wasomi wa Kiafrika, kwa mfano, Wole Soyinka na Ali Mazrui (Chimerah 1998; 128).

Upembuzi huu kuhusu lugha unaweka fasihi ya Kiswahili katika kitovu cha usomi wa fasihi ya baada-ukoloni barani Afrika na hivyo kuwepo kwa haja ya kuona inavyoitikia hali ya ubaada-ukoloni.

Nadharia ya baada-ukoloni pia huangazia namna ambavyo fasihi za baada-ukoloni huendeleza dhana ya kupinga ukoloni na amali zake za kiutamaduni au anavyoeleza Mbatia (2001:62), "kusisitiza tofauti za kiutamaduni na fasihi za jamii za baada-ukoloni na utamaduni na fasihi za Kiulaya" pamoja na kupindua dhana za Kiulaya zilizotumiwa kuuendeleza ukoloni. Athari ya mwelekeo huu ni kupinga madai ya ubia yaliyoendelezwa na wahakiki wa Kimagharibi wa mitalaa ya kibinadamu *(humanists)*. Kwa mujibu wa Barry (2002:192), kudai kuwepo kwa fasihi zenye umuhimu wa kiubia ni kupuuza kuwepo kwa tofauti za kiutamaduni, kijamii, kimaeneo na kitaifa katika jamii za ulimwengu. Bila shaka kudai matumizi ya "viwango vya kiubia" katika fasihi ni kuhalalisha thamani na viwango vya Kiulaya. Ni kuungama kwamba utamaduni wa Kiulaya ndio unaofaa na tamaduni nyingine ni duni na hazifai. Hivyo, waandishi wa tamaduni nyingine wajaribu waandike kama waandishi wa Kiulaya ili fasihi zao zikubalike! Hii ni njia ya kuendeleza ukoloni. Nadharia ya baada-ukoloni hupinga ubeberu huu wa kiutamaduni. Aidha, namna ambavyo kazi mahsusi inavyojaribu kujiengua na kanuni za tanzu za Kimagharibi huangaziwa. Hatua hizi hudhamiriwa

kuondoa ubeberu wa kiutamaduni wa Kiulaya unaoziona fasihi na utamaduni kwa jumla wa watawaliwa kuwa duni.

Suala lingine ni la mgogoro wa utambulisho katika jamii ya baada-ukoloni. Utambulisho wa jamii hizo uliharibiwa na shughuli za ukoloni kama vile uhamishwaji, biashara ya watumwa pamoja na kudhalilisha kwa utamaduni wao. Hali hiyo hujitokeza katika fasihi za baada-ukoloni kupitia ukengeushi wa kiutamaduni na lugha (Ashcroft na wengine, 2002:9). Ubaada-ukoloni husisitiza umahuluti katika utambulisho kwani ndiyo hali halisi ya jamii za baada-ukoloni. Ukengeushi huo unaweza kuondolewa kupitia kubomolewa kwa amali za utamaduni wa kikoloni. Hivi watawaliwa wataweza kuuokoa utambulisho uliodhalilishwa.

Kwa muhtasari nadharia ya baada-ukoloni:

(i) Hukataa mtazamo wa kiubia unaofanywa na wahakiki wa fasihi za Kimagharibi. Aidha, huonyesha upungufu wa mtazamo huo hasa kushindwa kwake kuonyesha tofauti za kiutamaduni.

(ii) Huchunguza uwakilishi wa tamaduni za "wengine" katika fasihi za kikoloni kama namna ya kuafikia lengo (i).

(iii) Huonyesha namna ambavyo fasihi zinazodaiwa kuwa ni za kiubia hufumbia macho masuala ya ukoloni na ubeberu.

(iv) Husisitiza masuala ya upana na tofauti za kiutamaduni pamoja na kuchunguza namna yanavyoshughulikiwa katika fasihi husika.

(v) Hutambua umahuluti katika tamaduni za baada-ukoloni ambapo watu binafsi katika jamii za baada-ukoloni huweza kutokea kuwa katika zaidi ya utamaduni mmoja (kwa mfano, utamaduni wa mkoloni unaosambazwa na mfumo wa elimu ya kikoloni na utamaduni wa mtawaliwa anaoupata kupitia elimu ya kienyeji ya kimapokeo).

(vi) Huendeleza mtazamo ambapo athari na hali za ukoloni huonwa kama chachu ya kani ya mabadiliko katika jamii za baada-ukoloni. Madhara ya ukoloni hutafutiwa namna ya kuyabadilisha ili yafaidi watawaliwa.

Utafiti huu vilevile unatumia dhana ya ugatuzi kama inavyojitokeza katika nadharia ya udenguzi. Kimsingi mwasisi wa nadharia ya Udenguzi, Derrida (Taz. *Structure, sign and play in the Discourse of Human Sciences*) hupinga utovuneno kwa kuwa maandishi ndiyo muhimu kuliko usemi. Anadai kwamba maandishi ndiyo muhimu kwani usemi uliotumiwa katika kuumba ulimwengu kwa sasa haupo lakini umehifadhiwa katika maandishi (Hardy, 1998: 485).

De Man na Wahakiki wa Yale waliyatumia mawazo ya Derrida katika fasihi na hivyo kuipa nadharia ya udenguzi mashiko zaidi katika fasihi. Tukio hilo lilitokea katika miaka ya sitini, kipindi ambacho "siasa" za kuhoji mawazo ya Uhakiki Mpya zilikuwa kali katika vyuo vikuu vya Kimarekani. (Rorty 1995: 1780). Mawazo ya De Man ni katika udenguzi wa balagha (lugha ya kifasihi). Katika udenguzi kwa fahiwa hiyo makini huelekezwa katika lugha ya kifasihi na mbinu zake, kama vile, ishara, taashira, sitiara, tashbihi miongoni mwa nyingine kwani ndiyo humwezesha kifasiliwa kwa kazi mahususi

katika maana nyingi. Hali hii inawezesha kupata maana katika matini ndani *(subtext/ silences)*.

Hivyo nadharia hii nayo inatuwezesha kupata dhana zilizofichika za ugatuzi wa utamaduni wa Kimagharibi katika kazi za Ngugi katika harakati za kuupa utamaduni wa jamii aliyoiandikia (watawalia wa kikoloni) kutambuliwa tena. Aidha, Rorty (Khj) anashadidia hili anaposema:

> *Usomi unaoongozwa na udenguzi katika falsafa na fasihi umetoa ushahidi wa kuaminisha kwamba uhakiki wa kidenguzi unaweza kuangazia "mantiki' iliyofichika katika mahusiano ya kimamlaka na utawala. Mantiki hii lazima ifichuliwe kama sharti la kwanza katika kujigundua kisiasa.*
>
> *(Tafsiri yangu)*

Kwa kulinganisha dhana ya ugatuzi (katika nadharia ya baada-ukoloni) na dhana ya udenguzi (katika nadharia ya udenguzi-kudhihirisha kutokuwepo kwa kitovu cha maana), inajitokeza kwamba ni dhana zinazotumika sambamba katika utafiti huu. Dhana hizi ndizo hutumika katika upinduzi.

Upinduzi ni dhana inayohusiana sana na ugatuzi. Upinduzi ni dhana ya nadharia ya udenguzi. Upinduzi huvunjilia mbali migawo uwili inayopingana na ambapo mgawo mmoja unachukuliwa kuwa wa hadhi ya juu. Dhana hii hutumiwa katika fasihi ya baada-ukoloni kuumbua migawo uwili inayoendeleza ukoloni ambapo kimsingi migawo uwili ya kimaniki *(Manichean binary)* hutumika. Kimsingi mgawo uwili wa kimaniki huwa wema/uovu. Ukoloni ulijipachika mgawo wa wema huku watawaliwa wao wakipachikwa

mgawo wa uovu. Mathalan, tunapata katika ukoloni weupe/weusi, wenye urazini/wasio urazini, wenye ustaarabu/washenzi, nuru/giza miongoni mwa migawo mingine.

Upinduzi katika uhakiki wa fasihi ya baada–ukoloni hulenga kuufuta mpaka wa migawo hiyo ili kuonyesha kuwa haikujengeka katika misingi ya kikweli. Ilidhamiriwa kuwapumbaza watawaliwa ili watawaliwe kikoloni. Mintarafu hii tunapozingatia ugatuzi katika tamthilia za Ngugi hatuna budi kugusia upinduzi. Ni dhana zinazoenda sambamba katika mitalaa ya ukolonishuaji.

Utovuneno umeathiri mitazamo ya kiusomi ya Kimagharibi pamoja na utamaduni wake. Mgawo uwili wa migawo inayopingana ulitumiwa hata katika kumtenga mtawaliwa katika ukoloni kutokana na mtawala. Migawo hiyo ni kama watu weusi/watu weupe wenye urazini/ wasio na urazini, giza/nuru, waliostaarabika/washenzi n.k. Hivyo, mwingiliano wa nadharia hizi mbili ni muhimu katika utafiti huu.

Loomba (1998: 70) anaeleza kuwa, kazi za kifasihi ni mkusanyiko changamano wa ishara za lugha. Lugha na ishara zake ni uwanja ambapo itikadi tofauti hukutana na kuvutana. Mintarafu hii itikadi za ukoloni pamoja na za kuupinga hutokea katika kazi hizi za kifasihi za baada–ukoloni. Mfumo wa lugha ya kifasihi huwezesha hili kutokana na tamathali zake za usemi.

## 1.7 Upeo na Mipaka

Utafiti huu unachunguza namna ambavyo utamaduni wa Kimagharibi unavyogatuliwa katika tamthilia za Ngugi wa Thiong'o pamoja na zile ambazo ameandika kwa ushirikiano na waandishi wengine. Mwenyewe, Ngugi ameandika michezo minne: *Mtawa Mweusi* (1970) na mkusanyiko wa michezo mifupi mitatu wenye kichwa, *Kesho Wakati Kama Huu* (1976). Michezo iliyoko ni: *Waasi*, *Kidonda Moyoni* na *Kesho Wakati Kama Huu*. Aidha, kwa ushirikiano ameandika tamthilia mbili: *Nitaolewa Nikipenda*, ambayo ameiandika na Ngugi wa Mirii. Mchezo huu uliandikwa kwanza kwa lugha ya Gikuyu kwa kichwa *Ngaahika Ndeenda* (1977). Nayo tamthilia ya *Mzalendo Kimathi* iliyoandikwa kwanza kwa lugha ya Kiingereza kama *The Trial of Dedan Kimathi* (1977) ameiandika na Micere Mugo.

Tamthilia alizoziandika Ngugi peke yake na zile alizoziandika kwa ushirikiano na waandishi wengine ndizo zinazoshughulikiwa katika utafiti huu. Riwaya zake na hadithi fupi hazijashughulikiwa.

## 1.8 Fasili za Istilahi

Ni muhimu hapa kufasili baadhi ya istilahi ambazo zimetumiwa katika utafiti huu kwa sababu wakati baadhi yake hazitumiki katika matumizi ya kawaida (kifasihi), nyingine ni mpya na matumizi yake hayajakubalika miongoni mwa wasomi wa fasihi ya Kiswahili.

### 1.8.1 Baada-ukoloni

Istilahi hii imetumiwa ikiambatanishwa na dhana nyingine kwa mfano: nadharia ya baada-ukoloni, fasihi ya baada-ukoloni, kipindi cha baada-ukoloni na tamaduni za baada-ukoloni. Hivyo, maana yake ni muhimu ibainishwe katika muktadha wa matumizi. Katika miktadha ya kwanza miwili, inarejelea matumizi yake kinadharia kama upinzani wa ukoloni na utawala wa kikoloni. Hivyo, fasihi ya baada-ukoloni ni fasihi inayopinga ukoloni. Matumizi ya aina ya pili ni katika muktadha wa kihistoria hasa mfuatano wa vipindi. Hapa panabainika vipindi kama: kipindi cha kabla ya ukoloni, kipindi cha ukoloni na cha baada-ukoloni.

### 1.8.2 Ubaada-ukoloni

Istilahi hii inatumika katika fahiwa ya kinadharia kuonyesha hali ya kupinga kategoria za kikoloni. Fasihi inayopinga kategoria hizo basi inaafiki hali hiyo. Aidha, ubaada-ukoloni ni hali ya jumla inayokumbatiwa na uandishi wa kifasihi unaoongozwa na nadharia ya baada-ukoloni.

### 1.8.3 Upinduzi

Istilahi hii inatumiwa kwa maana ya kuyumbisha migawo uwili inayopingana ambapo mgawo mmoja unawekewa hadhi ya juu. Kiini chake ni kuuekua mgawo uliopewa hadhi awali na kufuta mipaka inayobainisha migawo hiyo.

### 1.8.4 Utovulaya

Istilahi hii inarejelea hali ambapo Ulaya inawekwa kama kitovu na tamaduni nyingine zinafasiliwa kutoka kwa mkabala wake. Kitovu hiki ndicho kinachoweka viwango mbalimbali "vya kiubia" katika harakati za ukoloni.

### 1.8.5 Usemi

Istilahi hii inatumiwa kurejelea upembuzi wa kinadharia na pia maneno ya kutamkwa (kinyume na maandishi/ maneno yaliyoandikwa).

### 1.8.6 Taswira potofu/taswira dufu

Istilahi hii inatumiwa kurejelea dhana ambazo kimsingi hazina ukweli lakini zinakaririwa kumhusu mtawaliwa wa kikoloni na mtawala wa kikoloni ili kuzizamisha akilini mwake na azifasili kama "ukweli" kumhusu.

### 1.8.7 Utamaduni wa kitaifa

Istilahi hii inatumiwa kwa fahiwa inayopendekeza Fanon, kwamba ni juhudi za pamoja za wanajamii, katika fani ya kiakili za kuelekeza, kutetea na kutukuza matendo ambayo kupitia kwayo jamii yao imejijenga (1963: 166).

## 1.9 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili

Kufikia sasa, Cook na Okenimkpe (1997) ndio ambao wameshughulikia kazi zote za Ngugi kwa pamoja. Wamezifasili tamthilia zake kwa kutumia mandhari ya kisiasa na kiuchumi ambapo tamthilia hizo ziliandikiwa. Mahusiano ya kiuchumi ya watawaliwa na

watawala katika ukoloni na ukoloni mambo-leo ni suala ambalo wamelishughulikia kwa kina. Katika suala hilo umiliki wa ardhi wameuangazia zaidi. Hata hivyo, Cook na Okenimkpe wamezishughulikia tamthilia za Ngugi kwa ufinyu ikilinganishwa na namna wanavyoshughulikia riwaya. Kila riwaya imeshughulikiwa katika sura nzima ilhali tamthilia zimeshughulikiwa pamoja katika sura moja. Kwa hilo wanaelekea kukubaliana na Gitahi (1980) ambaye anadai kwamba Ngugi anaonyesha kufaulu katika uandishi wa riwaya kuliko tamthilia.

Madai hayo yanakosa mashiko hasa kwa kuwa hakuna utafiti uliofanywa kulinganisha riwaya na tamthilia zake kukadiria ubora wa mwandishi huyu katika tanzu hizo mbili. Huenda pia utafiti wa aina hiyo usisaidie kwa kuwa tanzu zenyewe mbili hutumia vigezo tofauti kabisa vya usanii na vya kiuhakiki. Kufaulu kwa mwandishi hudhihirishwa na wahakiki. Hivyo haitoshi kudai kutofaulu kwa Ngugi katika uandishi wa tamthilia bila kuwepo kwa uhakiki wowote kuthibitisha madai kama hayo. Hata hivyo, utafiti wa Cook na Okenimkpe ni muhimu kwa utafiti huu kwani suala la uzalishaji mali, umiliki wa ardhi, matumizi yake na thamani inayowekewa na jamii husika ni sehemu ya utamaduni wao.

Gitahi (1980) naye anachunguza maendelezo ya mwandishi huyu katika mtazamo wa Kisosholojia. Ingawa ameteua baadhi ya riwaya za Ngugi anaungama kwamba tamthilia za Ngugi hazijafanyiwa uhakiki wa kuridhisha. Vilevile, kama Cook na Okenimkpe, Gitahi anakita utafiti wake katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa katika muktadha wa ukoloni na ukoloni mambo-leo. Katika suala la utamaduni, Gitahi anataja tu

kuwa kazi za Ngugi zinaonyesha mgongano wa tamaduni. Utafiti huu unapiga hatua zaidi katika kuonyesha namna tamthilia za Ngugi zinavyoonyesha mgongano wa tamaduni na namna utamaduni wa kikoloni unavyobomolewa. Utafiti huu pia unatumia nadharia tofauti.

Githae (1978) anatalii kazi za Ngugi katika kutafuta maono yake kuhusu Afrika. Aidha, katika kazi hii Githae anawaangazia waandishi wengine kama Chinua Achebe, Margaret Laurence na Elspeth Huxley. Kama watafiti tuliowarejelea hapo awali, Githae anatoa kauli kwamba Ngugi amefaulu sana katika uandishi wa riwaya kuliko tamthilia. Tatizo lililopo katika kauli yake ni kutothibitishwa. Yumkini kauli yake ilichochewa na kutaka kuziweka tamthilia za Ngugi pembezoni ili ashughulikie riwaya kwani waandishi wengine anaowaangazia ni waandishi wa riwaya. Kuna kutowiana kwa uhakiki wa riwaya na tamthilia.

Hata hivyo, utafiti wake ni muhimu kwani katika sehemu mojawapo ya sehemu zake, anaangazia taswira potofu kuhusu Afrika ambazo Wazungu huziendeleza na namna ambavyo Ngugi anazipinga. Hii ni katika riwaya za *Weep Not Child, Petals of Blood* na *The River Between*. Utafiti huu unaangazia tamthilia.

Mugai (2000) ameshughulikia tamthilia ya *Mzalendo Kimathi*. Hata hivyo, lengo lake ni kutalii taswira za shujaa Kimathi kama zinavyojitokeza katika tamthilia hii. Aidha, anaangalia kazi nyingine za kifasihi zinazoshughulikia shujaa huyu ili kuona taswira zake zinavyojitokeza. Utafiti huu ni muhimu kwetu kwani unatoa thamani za kiutamaduni za

jamii ya Gikuyu kuhusiana na asasi ya ushujaa. Utafiti huu utazitathmini thamani hizo ili kuona ikiwa zimetumika katika harakati za ugatuzi katika tamthilia ya *Mzalendo Kimathi*.

Karanja (1990) anaihakiki tamthilia ya *Mzalendo Kimathi* kwa kutumia mtazamo wa nadharia ya Ki-Marx. Ukombozi anaourejelea ni wa kiuchumi na anatumia mwelekeo mmojawapo ya mielekeo ya U-Marx, uyakinifu wa Kisoshalisti. Uhakiki huu tofauti na wa Karanja haushughulikii harakati na mahusiano ya kiuchumi. Suala la uzalishaji mali linashughulikiwa tu kama sehemu ya utamaduni.

Smith (1989) anaangazia uandishi wa Kiafrika na changamoto ambazo zinaukumba, zikiwemo za ukoloni na tajriba ya kikoloni. Aidha, hizi ndizo kani ambazo zimezipa fasihi andishi za Kiafrika muundo. Kazi yake inamwangazia Ngugi wa Thiong'o kama mwandishi wa Kiafrika anayekabiliana na changamoto hizo. Hivyo, kazi yake inaufaa utafiti huu hasa kuufahamisha kuhusu Ngugi anavyolikabili suala la ukoloni. Umuhimu mwingine ni mawazo anayoyatoa mtafiti huyu kuhusiana na tofauti kati ya michezo ya kuigiza ya Kimagharibi na Kiafrika kwa kutumia tamthilia ya Ngugi ya *Nitaolewa Nikipenda*. Hata hivyo, utafiti huu unapiga hatua zaidi katika kuchunguza namna Ngugi anavyozitwaa tofauti hizo na kuzitumia kama mkakati wa ugatuzi.

Naye Killam (1984) anauangazia uandishi wa Ngugi wa Thiong'o na mchango wake wa kuipa fasihi ya Kiafrika msisitizo. Katika uangazio wake, anachunguza uhusiano wa fasihi na ubeberu wa Kiulaya hasa ulivyoielekeza fasihi andishi ya Kiafrika. Killam pia anaangalia dhana za lugha, na historia katika riwaya na tamthilia za Ngugi. Dhana hizi ni

muhimu katika fasihi ya baada-ukoloni na zinaufahamisha zaidi utafiti huu. Hata hivyo, utafiti huu unaangazia dhana zaidi za fasihi ya baada-ukoloni kwa kuzingatia tamthilia zote za Ngugi.

Tejani (1973) katika utafiti wake anaangazia umuhimu wa hadhira ya kienyeji na mandhari ya kienyeji katika fasihi ya "kisasa" ya Kiafrika. Katika kazi yake anaangazia uandishi wa Ngugi, La Guma, Mphahlele, Okara na Peters. Jambo la umuhimu kwa utafiti huu ni tahakiki anayoitoa kuhusu michezo ya kuigiza ya Ngugi iliyoko katika mkusanyiko wa *Kesho Wakati Kama Huu*.

Tejani anaangazia umuhimu wa wahusika "wageni" ambao ni: Mgeni katika *Waasi* na *Kesho Wakati Kama Huu* na Ruhiu katika *Kidonda Moyoni*. Hawa ni wahusika ambao wamepata nafasi ya kutalii tamaduni nyingine, utamaduni wa Kimagharibi ukiwepo. Wahusika hawa wana tajriba za tamaduni zao za kienyeji na utamaduni wa Kimagharibi na wanatetea kuzitwaa baadhi ya dhana za utamaduni huo ili kuuboresha utamaduni wao. Wahusika waliopo katika hali kama hiyo huangaziwa katika fasihi ya baada-ukoloni. Hali yao hurejelewa kama umahuluti. Umahuluti katika fasihi ya baada-ukoloni huwa kani ya ubunifu inayaweza kuleta mabadiliko chanya katika jamii zilizotawaliwa kikoloni.
Hivyo, utafiti wa Tejani una manufaa kwa utafiti huu hasa unavyoupa mwanga wa awali katika kuhakiki michezo hiyo ya kuigiza. Hata hivyo, utafiti wetu ni mpana zaidi kwani unaangazia dhana zaidi za fasihi ya baada-ukoloni katika tamthilia zote za Ngugi wa Thiong'o.

Kwa hakika ni machache yaliyoandikwa kuhusu tamthilia za Ngugi. Yaliyochanganuliwa hapa ni yale yaliyoweza kupatikana. Suala kuu linalojitokeza katika kazi hizi ni kutumiwa kwa nadharia ya U-marx katika kuhakiki kazi za Ngugi. Githae (1978: ix) anaelezea kwamba uhakiki wa Ki-Marx ndio uhakiki wa kipekee unaoshughulikia vizuri maudhui ya ukoloni, ukoloni mambo-leo na ubeberu katika fasihi. Wahakiki wa baadaye walielekea kuchukua mtazamo huo. Tatizo lililopo ni kwamba U-Marx hauwezi kuangazia masuala ya utamaduni zaidi ya historia na mahusiano ya kiuchumi. Hivyo panatokea pengo katika tahakiki zinazoegemezwa U-Marx katika kushughulikia suala la utamaduni katika muktadha wa ukoloni tunapozingatia mahusiano ya kiutamaduni kati ya watawaliwa na watawala. Matumizi ya nadharia ya baada-ukoloni ni mwafaka zaidi katika kuangazia mahusiano ya kiutamaduni katika ukoloni na ukoloni mamboleo.

### 1.10 Njia za Utafiti

Utafiti huu unatoa data katika tamthilia zinazoshughulikiwa. Data hiyo imehakikiwa kwa kutumia vigezo vya nadharia zinazotumia. Tumedurusu pia vitabu vilivyoandikwa kuhusiana na mitalaa ya ukoloni pamoja na utamaduni ili kuufahamisha zaidi utafiti huu hasa uhusiano wake na fasihi.

Kwa jumla utafiti huu ni wa maktabani. Mashauri kutoka kwa wanazuoni wa fasihi pia yametafutwa katika kuhakikisha utafiti huu umefuata mkondo ufaao.

**Tanbihi**

1. Istlahi hii kama kisawe chake katika Kiingereza haijapata mwendelezo unaokubaliwa na wasomi wa fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, Wamitila (2002: 166) anatumia Ki-Baadaukoloni, Mbatia (2001: 62), Njogu na Chimerah (1999: 15) wanatumia Baada-ukoloni. Hata hivyo, utafiti huu haudhamirii kuendeleza mjadala wake mwendelezo wa Baada-ukoloni utatumiwa.
2. Ugatuzi hapa unatumiwa kwa maana ya kuondoa msisitizo katika utamaduni wa Kimagharibi na badala yake msisitizo uangaziwe katika tamaduni za jamii zilizotawaliwa kikoloni (Taz. Wamitila 2003: 257).
3. Dhana ya kukolonishua katika uhakiki huu inatumiwa kwa maana ya kuondoa athari za ukoloni. Istilahi hii iliingizwa katika fasihi ya Kiswahili na Wamitila (2002: 168).
4. Istilahi hii inarejelea hisi za mseto zinazopingana, kwa mfano, katika ukoloni, watawaliwa walitakiwa waige utamaduni wa mkoloni ili wawe kama mkoloni na wakati huo huo wajione kuwa wao ni tofauti na mkoloni (wana ngozi nyeusi, ni wajinga, hawawezi kuwa kama Mzungu n.k.).

# SURA YA PILI

## 2.0 FASIHI, UKOLONI, UBAADA-UKOLONI NA UTAMADUNI

### 2.1 Utangulizi

Sura hii itaangazia masuala muhimu ya utafiti huu ambayo ni fasihi, ukoloni, ubaada-ukoloni na utamaduni. Kiini cha sura yenyewe ni kuonyesha mwingiliano wake katika fasihi ya baada-ukoloni. Uhusiano wa dhana hizi ndio kiini cha uitikio wa uandishi wa fasihi ya baada-ukoloni. Kiini cha mjadala wa sura hii ni kuweka msingi imara katika uhakiki wa kazi husika.

### 2.2 Fasihi na Utamaduni

Dhana ya utamaduni ni pana na katika usomi, wasomi huimega tu sehemu wanayojishughulisha nayo. Msogeleo tutakaoutumia ni unaouangalia utamaduni kwa namna mbili anazoeleza Wamitila (2003:330). Kwanza, kuuangalia utamaduni kama uzoefu wa kimaisha wa watu fulani. Katika fahiwa hii pana, utamaduni ni mwenendo wa maisha unaoundwa na watu katika juhudi zao za pamoja za kupatana na mazingira yao. Ni jumla ya: sanaa, sayansi, asasi za kijamiii ukiwemo mfumo wao wa imani na matambiko yao (Wa Thiongo, 1972:4). Utamaduni hurithiwa na humpa binadamu hadhi ya kiutu pamoja na kumwezesha kujiendeleza kimaisha.

Kila utamaduni hujikita katika mfumo fulani wa kuufasili uhalisia ambao huwawezesha watu katika utamaduni huo kuelewana kama jamii. Hali hii huwapa sababu ya kufanya mambo fulani, sababu ya kuwepo na kuwa na utaratibu fulani ulio na wiano katika

ulimwengu usio na mpangilio wenye wiano (Ani, 1996:2). Umuhimu wa utamaduni ni kutosheleza mahitaji ya binadamu. Mahitaji hayo ni ya aina mbili (White, 1943:244). Kwanza, yale mahitaji ambayo yanaweza kutoshelezwa kupitia kuzua raslimali zinazotokana na binadamu mwenyewe. Kwa mfano, kuimba, kucheza ngoma, kubuni visasili, kuunda asasi za kijamii kwa matilaba ya kuingiliana na binadamu wenzake. Mahitaji ya aina ya pili hutoshelezwa na raslimali za ulimwengu wa nje; za kimazingira.

Kwa mkabala wa kwanza, fasihi ni sehemu ya utamaduni na hudhamiriwa kutosheleza mahitaji ya aina hiyo ya kwanza (ambayo hutoshelezwa na raslimali zinazotokana na binadamu mwenyewe). Fasihi kwa hali hiyo ni raslimali, ni zao la jamii. Kwa maneno ya Gibbe (1978:2).

> *Fasihi ni zao la jamii. Ni zao ambalo ni chombo vilevile cha jamii hiyo ambacho kinaweza kutumiwa kwa shari ama kwa heri. Inaweza kutumiwa kusaidia kuwachonga wanajamii ili wayaangalie mazingira yao kwa udadisi na uchambuzi ili wayarekebishe. Vilevile, inaweza kutumiwa [na watu fulani] kuwapumbaza au kuwatia kiwi machoni wanajamii wasiweze kuyaangalia kwa jicho pevu mazingira yao.*

Maoni kuhusu mahitaji ya kijamii yanayotoshelezwa na raslimali zitokanazo na binadamu mwenyewe yanaendana na aina ya pili ya msogeleo wetu kuuhusu utamaduni. Aina hii ya pili huuangalia utamaduni kwa maana finyu kurejelea sanaa, fasihi na matendo mengine ya kiujumi (Wamitila 2003:330). Lugha hapa inachukua nafasi ya kati.

Ikiwa utamaduni huwasaidia wanajamii kupatana na mazingira yao na kuufasili uhalisia, basi maneno huwasaidia kuueleza ulimwengu wao. Lugha kimantiki inahusiana na

maneno na ni mfumo wa kuvipa vitu majina. Binadamu huudhibiti ulimwengu wake kupitia kuufasiri kwa lugha yake. (Wa Thiong'o, 2004:65). Hapa madai ya Fanon (1967: 17-18) yanaafiki sana kwamba kutumia lugha fulani ni kuuchukua utamaduni wake. Vivyo hivyo, binadamu anayemiliki lugha pia anaumiliki uhalisia wa ulimwengu unaowasilishwa na lugha hiyo. Hasa ni kuukubali mwono-ulimwengu[1] wa lugha hiyo.

Upembuzi huu unazua suala la mitazamo ya uhusiano wa lugha na utamaduni. Mitazamo hiyo ni, kwanza, lugha ni sehemu ya utamaduni wa jamii fulani na pili, lugha ni chombo cha kuubebea utamaduni; huakisi utamaduni. Mitazamo hii ina hoja zinazokamilishana. Hata hivyo, bila kuingilia mjadala wake ni wazi kwamba utamaduni ni mali ghafi ya fasihi na fasihi ni sehemu ya utamaduni wa jamii husika.

Katika kujadili mahitaji yanayotoshelezwa na raslimali za kitamaduni zinazotokana na binadamu mwenyewe tulitaja kwamba sanaa ni mojawapo wa raslimali hizo. Fasihi ni sehemu ya sanaa. Mshikamano huu unafumbatwa vizuri na Wicke (katika, Hardy 1998: 564) anapoeleza:

> *Kusoma kazi ya kifasihi ni kuusoma utamaduni wa jamii husika. Kazi ya kifasihi huwa ni nafasi mwafaka ya kuutalii utamaduni wa jamii iliyoandikiwa. Lugha ya kazi ya kifasihi husheheni viashiria vya utamaduni husika. Kwa namna hiyo fasihi si kiakisi kilichosimikwa cha utamaduni bali ni sehemu ya utamaduni husika na hasa kiashiria muhimu cha kuonyesha masuala muhimu ya kiutamaduni yaliyokuwepo wakati kazi husika ilipoandikwa.* *(Tafsiri yangu)*

Utamaduni ni zao la historia ya jamii, lakini pia huakisi historia hiyo, Mathalan, tunazo kazi za kifasihi zinazoakisi historia ya jamii husika. Utamaduni huhusisha seti za thamani za kiutu ambazo watu hujiangalia kupitia kwazo na pia mahali pao na wakati. Kwa mfano, thamani hizo huongoza maamuzi ya kijamii kama kuadhibu na kutuza. Fasihi ina dhima ya kuongoza jamii husika katika kutambua na kukumbatia thamani ambazo zinawezesha kupatikana kwa maisha yenye uwiano.

## 2.3 Fasihi, Ukoloni na Ubaada- ukoloni

Katika sehemu hii tunaangazia namna ambavyo dhana za ukoloni na ubaada-ukoloni zinavyohusiana na dhana za fasihi na utamaduni. Dhana za ukoloni mkongwe na ukoloni mambo-leo pia zitazingatiwa. Uhusiano uliopo kati ya dhana hizi mbili unaweza kueleweka kwa kuzingatia haram/piramidi ya mpangilio wa jamii katika kipindi cha ukoloni. Pale juu kabisa palikuwa na Wazungu na katikati palikuwa na Wahindi. Nao watu weusi, Waafrika walikalia sehemu ya chini iliyo kubwa. Mpangilio huu uliwagawa watu kufuatia hali zao kijamii, kiuchumi na kisiasa. Baada ya uhuru mipaka katika mpangilio huu wa uhusiano iliondolewa.

Waafrika waliokuwa na elimu wakapata uwezo wa kupanda katika nafasi ya juu kabisa na ya katikati. Mkoloni alipoondoka, Waafrika waliokuwa na elimu ya Kimagharibi walikalia sehemu sawa na Wazungu waliobakia. Hivyo tabaka hilo dogo la wasomi ndilo lililorithi nafasi za uongozi zilizoachwa na ukoloni. Elimu ya kikoloni iliwaandaa sawasawa kuwa kama mkoloni mwenyewe. Walijiona bora kuliko wenzao ambao hawakuwa na elimu ya Kimagharibi.

Mintarafu hii fasihi ya baada–ukoloni huangalia ukoloni kama mwendelezo wa ukoloni. Dhana ya ukoloni inapotajwa huzua mahusiano kama: kuingiliwa kwa jamii fulani na jamii nyingine, ukandamizaji kiuchumi au kutawaliwa kwa wenyeji wa eneo fulani na wageni, hasa Wazungu. Ukoloni, ambapo mataifa hudhibitiwa na mataifa mengine ulitokomezwa kirasmi katika kipindi cha uhuru, kile kimebaki ni utawala wa ukoloni mambo-leo katika mahusiano ya kimataifa na mahusiano ya kindani ya kijamii (Thomas: 1994:2).

Msogeleo wetu katika mjadala huu unaongozwa na uchukulizi sahili kwamba ukoloni haueleweki vizuri kimsingi kama uhusiano wa kiuchumi na kisiasa kama tafiti nyingi za awali kuhusu kazi za Ngugi zilivyoelekea kuonyesha (Taz. Githae (1978: ix). Tunadhamiria kuonyesha kuwa ukoloni kwa njia nyingine umekuwa mchakato wa kitamaduni. "Ugunduzi" na uingiliwaji wa waliotawaliwa kikoloni na wakoloni ulibuniwa na kupewa kani kupitia fasihi na kupitia njia nyingine zilizolenga kuathiri utamaduni wa watawaliwa. Amin Samir (1988: vii) anashadidia ukweli wa ukoloni kuwa mfumo wa kiutamaduni kupitia kuchanganua dhana ya utovulaya. Anaeleza:

> *Utovulaya ni tukio la kitamaduni kwa namna unavyochukulia kuwepo kwa tamaduni nyingi tofauti zinazounda historia ya jamii mbalimbali. utovulaya haujishughulishi na kuibuka na kanuni za kijumla za maendeleo ya binadamu bali hujiweka kama ubia na hudai kwamba kuigwa kwa muundo wa Kimagharibi na jamii zote za ulimwengu ndilo suluhisho kwa matatizo ya jamii za ulimwengu.* *(Tafsiri yangu)*

Katika tahakiki za kisasa za baada-ukoloni, mkabala wa kiubeberu wa fasihi za kiusafiri umekuwa ukiangaziwa. Fasihi hiyo huangaziwa kama namna ya uduhushi wa tamaduni za jamii nyingine (zisizo za Kiulaya) kwa niaba ya Serikali zao. Edward Said katika *Orientalism (1978)* ambapo anauhakiki mchakato wa ukoloni, anazipa asasi za kikoloni kipaumbele. Asasi hizo ni kama, mitalaa ya ethnografia, anthropolojia na fasihi za kiusafiri za waandishi wa Kiulaya.

Hasa katika fasihi za kiusafiri zilizoandikwa na Wazungu kuhusu watu wa Mashariki, Said anatambua tatizo kuu ambalo ni kuandikiwa nje ya muktadha na uelewa wa Mashariki. Hilo hufanya maandishi kuhusu Mashariki kuwa na uwakilishwaji uliopotoshwa. Mfano mzuri anaoutoa ni wa mchezo wa kuigiza wa Aeschylus, *The Persians*. Anaeleza kuwa uwakilishi wa kidrama wa mchezo huu huonyesha wazi kwamba hadhira inatazama uigizwaji wa hali isiyo asili, ambapo mtunzi asiyeelewa Mashariki ameutengeneza kuwa taashira ya kusimamia Mashariki kwa ukamilifu (khj: 32). Huu ulikuwa mchakato wa kuunda "wengine" na kuwafasiri Wamashariki katika mkabala wa Kimashariki.

Ukoloni ulilenga kutengua utamaduni wa watawaliwa. Wasomi, waandishi wa kazi za fasihi wakiwemo, kama viongozi wanaoelekeza jamii zao katika thamani za maadili, ujumi, utambuzi wao wa kuwepo na hatima yao ndio waliolengwa. Hili lilifanikishwa kupitia taasisi za elimu ambapo mfumo mzima wa elimu ulidhamiriwa kuwatayarisha wapokeaji wake kuuona ulimwengu kupitia macho ya Kimagharibi. Mathalan wasomi ambao ndio macho na masikio ya jamii husika ndio walioathirika zaidi (Wa Thiongo,

2004:64). Hii ndiyo sababu kama itakavyodhihirika katika sura ijayo Ngugi hujishughulisha sana na kundi hilo la wasomi. Aidha, katika fasihi ya Kiswahili kuna waandishi wanaoshughulikia kundi hilo. Kwa mfano, tamthilia ya *Mashetani* (1971) yake Ebrahim Hussein na *Marejeo* (1986) yake Chacha Nyaigoti Chacha.

## 2.4 Fasihi na Lugha Katika Fasihi ya Baada-Ukoloni

Njia mojawapo ambayo ukoloni ulitenga wasomi na jamii zao ni kupitia kuwatenganisha na lugha zao na kuwaunganisha na lugha za kikoloni (Wa Thiongo, 2004:64). Upembuzi huu unatuelekeza katika fikra za mtazamo wa baada-ukoloni kwa fahiwa ya Ki-Foucault. Mtazamo huu huangazia uhusiano baina ya lugha, ukweli na mamlaka *(Power).* Hapa "ukweli" ni kile kinachojulikana kuwa "kweli" katika mfumo fulani wa kanuni katika mtalaa mahsusi. Mamlaka nayo ni kile ambacho humiliki, huamua na huthibitisha ukweli.

Ukweli hauwezi kutenganishwa na mamlaka kwani ni nyenzo yake. Ukweli pia ni zao au matokeo ya mamlaka. Kwa maneno ya Foucault (1977 katika Ashcroft na wengine 2002: 165) *"Huwezi kutumia mamlaka bila kuunda ukweli"*. Kwa mtazamo wa fasihi ya baada-ukoloni ukweli unaozungumziwa hapa ni taswira potofu anazopumbazwa nazo mtawaliwa kuamini kuwa ndio "ukweli". Mtalaa wa baada-ukoloni basi unajikita katika mvutano wa kudhibiti kimamlaka; mamlaka hayo yakiwa yameangaziwa katika lugha ya kikoloni. Mamlaka hujikita katika lugha kwa sababu lugha husheheni nyenzo ambazo hubuni "ukweli".

Ukweli huu unapozamishwa akilini mwa watawaliwa, mtawala huwa amefaulu kuwatia shemere. Lugha hubeba utamaduni na historia ya jamii. Hivyo, hubeba kumbukumbu za jamii. Mchakato wa ubunifu ndio huunda kazi ya kifasihi. Hivyo, ubunifu ni uwezo/nguvu za uundaji wa kiakili. Kile ambacho huundwa ni utamaduni (Denham 1978:19) fasihi ikiwemo. Uwezo wa kuubadili ulimwengu wa nje hadi katika ulimwengu ambao binadamu ameupa umbo na maana, ndio ubunifu. Kinachofanya mwandishi kuumba ulimwengu huu wa kiakili ni katika kujaribu kutafuta wiano kwa kuwa ulimwengu wa nje hukosa wiano huo. Ubunifu huumba uhalisi hasa tunaokumbana nao katika fasihi. Fasihi ina dhima ya kuongoza jamii husika katika kutambua na kukumbatia thamani ambazo zinawezesha kupatikana kwa maisha yenye upatanifu. Mwandishi wa fasihi huzua mawazo muhimu, kupitia ubunifu, ambayo huiwekea jamii yake msingi. Hivyo mwandishi huyo ni kiongozi wa aina fulani katika jamii husika. Kiongozi ambaye mawazo yake hukubalika katika kuiendeleza jamii (Okot p' Bitek 1986: 38 – 41).

Upembuzi huu unaelekeza katika ukweli kwamba uhalisia unaorejelewa ndio utamaduni. Hivyo, ubunifu huumba utamaduni kutokana na maumbile (ulimwengu wa nje). Ubunifu pia huumba lugha ya kifasihi. Kazi nyingi za kifasihi huakisi mchakato wa kihistoria wa utamaduni wa jamii husika. Hata hiyo, kazi hizo hufinyanga baadhi ya sehemu za utaratibu huo na hali hii ndiyo hupambanua historia na kazi za fasihi za kihistoria za wakati mahsusi wa kihistoria. Waandishi wa fasihi katika jamii zilizotawaliwa kikoloni kutokana na kutengwa na lugha zao, kumbukumbu za jamii zao huzikwa chini ya kumbukumbu za Kiulaya. Kuzikwa huko hudhamiriwa kuziweka kumbukumbu hizo katika mchakato wa kusahaulika. Jamii ambayo haiwezi kuunga historia yake haina

uwezo wa kuangazia mustakabali wake. Hata hivyo, uungaji huo lazima uteue yaliyo muhimu na kuacha yasiyo muhimu katika historia na mapokeo yake (khj: 65).

Fasihi bora haiwezi kufumbia macho hali ya kisiasa iliyopo au ya wakati fulani mahsusi inayoshughulikia. Dhana ya fasihi katika ukoloni/ukoloni mambo-leo na harakati za kuupinga imekuwa ikishughulikiwa na fasihi ya baada-ukoloni. Aidha, fasihi huziba pengo baina ya uhalisia na ubunifu. Kuhusu fasihi na ukoloni, Loomba (1998:70) anaeleza:

> *Kazi za kifasihi ni mkusanyiko changamano wa ishara za lugha. Lugha na ishara ni mahali ambapo itikadi tofauti hukutanishwa na huvutana. Mintarafu hii itikadi za ukoloni pamoja na za kuupinga hutokea katika kazi hizi – mfumo wa lugha huwezesha hili.* (*Tafsiri Yangu*)

Katika kuoanisha hoja za Ngugi na Loomba (kuhusu dhana za fasihi, lugha na jamii) tunapata kwamba kazi za fasihi ni sehemu ya taasisi za kijamii, kwa mfano, masoko na mifumo ya elimu. Taasisi ya mifumo ya elimu hutekeleza jukumu muhimu katika kuunda mamlaka ya kitamaduni ya mkoloni katika koloni zake. Dhana za utamaduni wa kigeni hupenyeza kwanza katika wasomi ambao nao huzisambaza katika jamii zao. Hata hivyo, fasihi haiakisi tu itikadi tawala bali pia huakisi mivutano, uchangamano na tofauti katika tamaduni za kikoloni. Mathalan huu ndio msingi wa mawazo ya Homi Bhabha ya umahuluti na usebusebu (katika Loomba 1998: 89 – 90).

Fasihi basi ni uwanja muhimu wa mgusano wa tamaduni tofauti zinazokutana. Tamaduni hizo haziingiliani tu bali pia hupinduana katika hali ya kutetea hadhi. Fasihi simulizi

huakisi hali hii. Aidha, ni kutokana na wepesi wake wa kuitikia dhana za kigeni katika utamaduni wake. Katika muktadha wa ukoloni, fasihi inayoibuka katika pande zote mbili (upande wa watawaliwa na upande wa wakoloni) hufyonza na kutwaa dhana za utamaduni huo mwingine. Mintarafu hii, tanzu mpya, mawazo mapya na tambulisho mpya huundwa katika mchakato huo wa maingiliano. Kwa mfano, katika fasihi simulizi ya Kiswahili kuna dhana zinazojitokeza zinazopindua ukoloni (hata labda bila urazini wa watumizi wa fasihi hiyo). Kwa mfano, katika vitendawili ambao ni utanzu wa fasihi ya watoto utapata kitendawili kama: "Mzungu anachungulia dirishani." Jibu lake huwa ni "Kamasi".

Sitiari ya kamasi katika kitendawili hiki inaekua dhana ya ukoloni katika mwili wa watawaliwa. Ukoloni/mkoloni unamithilishwa na uchafu usiohitajika katika maisha ya watawaliwa. Kwa namna hii fasihi inajitokeza kama namna muhimu ya kutwaa, kupindua na kuhoji itikadi tawala za kikoloni na uwakilishaji wake pia.

Ukoloni nao ulitumia fasihi na lugha kukuza mtazamo kwamba utamaduni wa Kiulaya ndio uliokuwa utamaduni bora zaidi ulimwenguni. Kuanzishwa kwa idara za Kiingereza katika vyuo vikuu barani Afrika na fasihi ni mradi uliodhamiriwa kujenga, kuimarisha na kugongomeza mawazo hayo.

Weupe ulihusishwa na mambo mazuri huku weusi ukihusishwa na dhana ya kutovutia na mabaya yote. Hii ni mitazamo iliyokuzwa katika kipindi cha mvuvumko wa sanaa[2] katika ulaya. Riwaya kama *Heart of Darkness*, yake Joseph Conrad inashadidia hili kutokana na

namna inavyowasawiri watu weusi: kama wala watu, wala mizoga, wanaonuka, wajinga miongoni mwa taswira nyingine hasi.

Loomba (khj: 75) anaeleza kuwa fasihi ya Kiulaya ni "kalibu" ya historia ya maingiliano ya Ulaya na tamaduni nyingine. Mintarafu hii fasihi haiwezi kutenganishwa na historia na siasa za Kiulaya. Katika utaratibu wa kuziandika fasihi zake, Ulaya huchukua nafasi ya kitovu cha historia ya ukoloni. Hata usomi wa Fasihi Linganishi ulizuka kutokana na maingiliano ya fasihi na tamaduni. Siasa za kikoloni zilitumika hivyo Fasihi Linganishi ikaweka fasihi za Ulaya na Marekani katika kitovu cha usomi wa fasihi ulimwenguni. Fasihi hizi ndizo zilizotiliwa msisitizo kuwa ndizo zilifaa kusomwa (khj).

Hata uhakiki wa kitovulaya ulisisitiza orodha kuu[3] ya Kimagharibi *(Western Canon)* kama zilizoashiria utamaduni na thamani bora za kifasihi. Hivyo, utamaduni na fasihi ni nyanja ambazo zilichukua nafasi muhimu katika siasa za ukoloni. Udhibiti wa kitamaduni wa watawaliwa waliolazimishwa kujifunza fasihi ya Kimagharibi ulimaanisha kudhahilishwa kwa ubunifu na utendaji wa kiakili wa kimapokeo wa waliofunzwa fasihi hiyo. Waandishi wa jamii hizo za watawaliwa walipaswa kuiga mitindo ya Kimagharibi ya uandishi ili kazi walizoziandika zitambuliwe kuwa kazi za kifasihi. Ni katika msingi huo ambapo lugha ni sehemu muhimu ya urazini wa uhalisia wa Ulimwengu wa Tatu. Uhalisia wa Kimaajabu katika fasihi ya mataifa ya Ulimwengu wa Tatu hutumiwa kufasiri utamaduni wa Kimagharibi kwa mwono wa "wingine".[4]

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION



JOMO KENYATTA MEMORIAL
LIBRARY

Kwa kuzingatia haya yote, ni wazi kwamba hatua ya kwanza ya kuondokana na ukoloni huo wa kimawazo ni kuondokana na utamaduni wa kikoloni. Kupitia kuzipa msisitizo fasihi, lugha na tamaduni za watawaliwa zilizodhalilishwa. Fasihi zisizo za Kimagharibi zinafaa zigunduliwe tena zisherehekewe, zisambazwe upya na zifasiliwe tena sio tu katika kuuangazia mwono wa utamaduni wa Kiulaya lakini kama mchakato wa ukolonishuaji (khj 92).

Huu ndio mradi mkuu wa fasihi ya baada-ukoloni. Ni njia ya kuzipa hadhi sawa tamaduni za ulimwengu ili ziweze kuwa na mahusiano mwafaka na maingiliano huru. Aidha, hakuna jamii iliyo na uhodhi wa thamani bora ikilinganishwa na jamii nyinginezo. Jukumu la fasihi ya baada-ukoloni ni kukomboa mawazo ya watawaliwa kutokana na ukoloni wa kimawazo. Hili lazima lifanywe kwa utaratibu wa kubuni tena thamani za utamaduni wa watawaliwa kwa namna ambayo itajenga jamii husika upya. Ujenzi huu ndio utakaowezesha kuiponya jamii ya watawaliwa kutokana na ubeberu wa kiutamaduni. Shughuli hiyo lazima ifanywe kwa kutafuta tena, kugundua tena na kuunda tena vielelezo vya jamii inayotarajiwa.

Fasihi hii huzingatia ukweli kwamba uumbaji wa taswira potofu za kimbari na kuzamisha dhana za mawazo ya kuwa washenzi akilini mwa watawaliwa yalikuwa muhimu katika mwono-ulimwengu wa kikoloni. Hivi ni kudai kuwepo kwa utamaduni wa kikoloni. Utamaduni huo wa kikoloni unatambulishwa na dhana kama: kujifasiri kutokana na kuwa tofauti na "wengine", kuwa na uhodhi wa ustaarabu, fikra za umbari, kuchukuliwa kuwepo makundi ya watu wasiokuwa na utamaduni na historia miongoni mwa dhana nyingine. Fanon (1964:32) anashadidia haya anapoeleza:

> *Ikiwa utamaduni ni muungano wa ruwaza za kitabia [tabia hizo ziwe ni za kiakili au za kimatendo] zinazotokana na maingiliano ya binadamu na mazingira yake, binadamu mwenzake akiwepo, basi inaweza kudaiwa kwamba umbari ni elementi ya utamaduni. Hivyo, kuna tamaduni zilizo na umbari na nyingine ambazo hazina.*
>
> *(Tafsiri yangu)*

Waandishi wengi wa jamii zilizotawaliwa kikoloni wameandika kazi zinazoonyesha kwamba jamii zao zilikuwa na mipangilio mwafaka ya taasisi zake za kijamii, kwamba madai ya kikoloni kuwa jamii zao hazikuwa na historia, utamaduni, ustaarabu na mengineyo hayana mashiko. Aidha, Chinweizu na wengine (1980:291) wanaeleza kuhusu Afrika kwamba, waandishi na wahakiki wa fasihi ya Kiafrika ni wafanyakazi katika utamaduni wa jamii zao. Kwamba maendeleo katika bara la Afrika sio muhimu tu katika uchumi lakini pia katika kuunda taasisi mwafaka za kitamaduni; urazini chanya.

**2.5 Hitimisho**

Katika sura hii masuala muhimu kuhusiana na fasihi ya baada-ukoloni yamezungumziwa. Masuala yaliyojadiliwa ni: Uhusiano wa lugha, fasihi, utamaduni na ubaada-ukoloni na ukoloni. Uhusiano wa dhana hizi ndio msingi na kiini cha usomi wa fasihi ya baada-ukoloni. Vilevile, uhusiano huu ndio unaoleta haja ya kuudengua ili kuzikolonishua tamaduni za jamii zilizotawaliwa kikoloni.

Mikakati mikuu ya ugatuzi inayoibuka katika mjadala wa sura hii ni matumizi ya fasihi simulizi katika fasihi ya baada-ukoloni ya jamii za watawaliwa, matumizi ya lugha ya

watawaliwa au lugha za kikoloni zilizoekuliwa katika fasihi ya watawaliwa, uandishi tena wa historia ya watawaliwa na maelezo ya utamaduni wao ili kubainisha thamani zake na kuupambanua na utamaduni wa kikoloni. Haya ni baadhi ya masuala muhimu yanayotarajiwa kuibuka katika tamthilia zinazohakikiwa katika sehemu inayofuata.

**Tanbihi**

[1] Mwono-ulimwengu hutoa fasiri, dhana na chukulio zinazosaidia kupanga upatanifu wetu na mazingira na kupanga uwiano wa fikra zetu katika uhalisia.

[2] Hiki ni kipindi cha enzi za karne za 14, 15 na 16 katika Ulaya wakati ambapo palizuka maslahi mapya katika sanaa na fasihi yaliyotiwa chachu na usomi wa mawazo ya kisanaa ya Uyunani ya kale. (Taz. *Oxford Advanced Learners Dictionary*).

[3] Ni dhana ambayo hutumiwa kueleza kazi kuu za kifasihi zinazofunzwa na kuandikiwa sana. Kazi hizi hupata umaarufu na kutambuliwa kupitia mpito wa miaka kuwa kazi muhimu (Taz. Wamitila, 2003: 172)

[4] Wamitila K.W. (mawasiliano ya moja kwa moja, 8/5/2006).

# SURA YA TATU

## 3.0 UGATUZI KATIKA *MTAWA MWEUSI* NA *KESHO WAKATI KAMA HUU*

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia tamthilia za awali za Ngugi, *Mtawa mweusi* (1970) na *Kesho Wakati Kama Huu* (1976). Hizi ni tamthilia ambazo ameziandika yeye mwenyewe. Uhakiki huu wa tamthilia za awali ni muhimu kuufanya kwanza kabla ya kuzihakiki tamthilia za baadaye ambazo ameziandika kwa kushirikiana na waandishi wengine. Hili linatuwezesha kutathamini hali ya maendeleo katika uandishi wake wa tamthilia.

### 3.2 Misingi ya Ugatuzi

Ugatuzi ni mwelekeo wa uhakiki wa fasihi wa siku hizi. Kiini chake huwa ni kuhamisha msisitizo kutoka maeneo yaliyochunguzwa na kutiliwa msisitizo kwenye maeneo mengine yaliyopuuzwa hapo kabla (Wamitila 2003: 257). Kwa hali hii ugatuzi unapotumiwa katika mitalaa ya ukoloni hasa katika fasihi ya baada–ukoloni hudhamiriwa kutilia msisitizo utamaduni wa watawaliwa wa ukoloni. Sauti za watawaliwa hawa zilidhalilishwa na ukoloni na kwa hivyo ni muhimu ziangaziwe.

Mwandishi wa fasihi ya baada–ukoloni huwa na jukumu la kuwasilisha sauti za watawaliwa wa ukoloni. Gayatri Spivak[1] (katika Loomba 1998:233-4) anahoji ni kwa kiasi gani wasomi wa fasihi ya baada-ukoloni wanaweza kuwasilisha sauti za watawaliwa waliosukumizwa pembezoni na ukoloni (Katika Loomba 1998:233-4). Inaweza kudaiwa elimu ya Kimagharibi iliyolenga kuusambaza utamaduni wa Kimagharibi (Mazrui

1990:7) ilibadilisha utambulisho wa wasomi hao na hivyo kuwatenga na jamii zao. Hata hivyo, waandishi bora wa fasihi ya baada-ukoloni huwa na msimamo wa kiitikadi wa kukolonishua tamaduni za jamii zao. Mintarafu hii huweza kuzitwaa sauti za jamii zao na kuziwakilisha katika kazi zao za kifasihi. Sehemu ya tajriba yao huwa sawa na ya wanajamii wenzao na hivyo wao ni sehemu ya jamii husika. Kwa mfano, katika kazi za Ngugi kuna chembechembe za kitawasifu zinazoonyesha yeye ni sehemu ya jamii anayoiandikia. Yeye alikulia katika mandhari ya ukoloni (Cook na Okenimkpe 1997: 35).

Kazi za kifasihi za baada-ukoloni huashiria ubainifu wake katika uwakilishwaji wake (kwa namna yake kazi za kifasihi ni taashira za maisha ya jamii husika) kupitia: mandhari, majina ya wahusika na hata maudhui na lugha. Waandishi hudhamiria kubainisha utamaduni wao kama utamaduni tofauti unaojibainisha na ule wa kikoloni (Ashcroft na wengine 2002:58). Hii hasa ndiyo dhana ya ugatuzi tunayoirejelea katika uhakiki wetu.

### 3.3 Kuhusu kazi Husika

#### 3.3.1 Muhtasari wa Tamthilia ya Mtawa Mweusi

Tamthilia hii ina mwangazia Remi, mhusika mkuu. Remi anampenda Thoni lakini kutokana na kuona haya anashindwa kumweleza. Anapopata ujasiri wa kumjulisha anagundua kwamba Thoni alikuwa anaolewa na nduguye mkubwa. Baada ya miezi sita nduguye anafariki kutokana na ajali ya barabarani na kulingana na utamaduni wa kabila lao, Remi alipaswa kuingia mafa na mke wa nduguye aliyefariki. Kwa kukwepa hilo alitorokea mjini.

Tamthilia inaanzia katika kijiji ambapo makundi mbalimbali yanamtaka Remi arejee kijijini (kutoka mjini). Ndiye mtu wa pekee katika kabila lake ndogo aliyekuwa na elimu ya chuo kikuu. Sababu za kumtaka arudi zinatofautiana. Mkewe anamtaka ili achukue mahali pake kama mumewe wa pili; mamake Remi anamwonea huruma Thoni na anamtaka mwanawe arudi aishikilie familia yake. Thoni amekataa kuchukua mwanamume mwingine na anachagua kumsubiri Remi kwa uaminifu ingawa alijua kuwa Remi alikuwa anamkataa. Nao wazee kutokana na ushauri wa Remi wa kukipigia kura Chama cha Mwafrika wanamtaka arudi ili awe kiongozi wa kabila katika serikali. Mchungaji naye anamtaka Remi ili arudi amsaidie waliongoze kabila katika Ukristo.

Katika kitendo cha pili, tamthilia inamwonyesha Remi akiwa mjini. Ana uhusiano wa kimapenzi na msichana wa Kizungu, Jane. Katika mazungumzo yake na Omange, rafikiye, Remi anayapinga mawazo ya ukabila. Marafiki hawa wanashangazwa na kuongezeka kwa ukabila miongoni mwa viongozi kutoka wakati wa uhuru. Wazee wanapomwendea ili awe kiongozi wa kabila, Remi anakataa. Vilevile, anakataa wito wa Mchungaji wa kurudi kijijini. Lakini baadaye anamtuma Mchungaji kijijini kuwaarifu wanakijiji kwamba angerudi. Hata hivyo, kama anavyoeleza baadaye, dini haikusaidia jamii yake wakati wa ukoloni bali iliwagawanya na hivyo kuwadhoofisha na hapa mkoloni akaweza kuwatawala (uk 74).

Hata hivyo, makundi hayo mawili, wazee na Mchungaji wanaacha athari kwa Remi kupitia taashira za nyenzo zao, kifurushi cha ushirikina na Biblia. Lakini katika kurudi

lazima ajinasue na mpenziwe Jane ambaye anamuona kwamba hawawezani kutokana na tofauti zao za kitajriba. Lakini sababu hii inadhoofishwa na sababu kwamba hangemchukua Jane kwa sababu tayari alikuwa ameoa. Hili linamkasirisha Jane anayetoka na kumwacha.

Katika kitendo cha mwisho chenye kichwa, 'Marejeo ya Mtawa', makundi tofauti yanamngoja Remi kwa hamu. Thoni ana tamaa ya kupatana na Remi ingawa hataki kuonyesha wazi. Hata hivyo, kwa mshangao wa msomaji Ngugi anakipeleka kilele katika maudhui ya kisiasa. Sehemu ya kwanza ya tamthilia ilijenga mgogoro wa tamthilia katika ndoa ya Remi na Thoni na inatarajiwa basi mgogoro huo ungejengwa hadi kilele chake.

Remi anapofika kijijini anaanza kuhutubia mikutano ya kisiasa wakiwa na rafikiye Omange. Hotuba zake zinaelezewa na mhusika, Jirani wa Pili. Katika hotuba zake anakashifu ukabila na hata kuwazomea wazee wa kabila kwa kuuendeleza. Hata hivyo, hotuba hizi hazijitokezi kuwa na manufuaa kwa jamii katika kurekebisha tatizo lolote. Zinaonyesha kujisikia kwa wasomi kuwa watu bora zaidi katika jamii zao. Remi hatoi mwongozi wowote kwa jamii yake katika kukabiliana na matatizo yake ila tu anaukashifu ukabila.

Thoni anapomsikia Remi akidai kwamba angekosea kumuoa mtu aliyekuwa mpenzi wa mtu mwingine anatoweka na kugunduliwa baadaye akiwa amejiua. Remi anabaki kujilaumu kwa kumfanya Thoni ajiue. Hakuelewa kwa wakati unaofaa kuwa Thoni alikuwa na mapenzi ya dhati kwake. Kwa kifupi tamthilia hii inaangazia maudhui ya

ukabila, ufidhuli na ufinyu wa kimaono wa wasomi wa elimu ya kikoloni na uongozi wa baada-ukoloni.

### 3.3.2 Muhtasari wa *Kesho Wakati Kama Huu*

Mkusanyiko huu una michezo ya kuigiza mitatu kila mmoja wenye kitendo kimoja. Michezo hiyo ni *Waasi*, *Kidonda Moyoni* na *Kesho Wakati Kama Huu*. Michezo hii inaangazia maudhui tofauti lakini yanayoungwa pamoja na suala la ukoloni.

*Waasi* ni mchezo wa kuigiza unaowakilisha mvutano wa tamaduni. Utamaduni wa Kiafrika na utamaduni wa Kimagharibi katika wasomi wanaoupata katika elimu ya Kimagharibi. Charles, kijana aliyeelimika elimu ya 'mtu mweupe" anarudi nyumbani kutoka chuo kikuu nchini Uganda akiwa na mpenziwe, Mary wa kutoka kabila moja la Uganda. Hata hivyo, nyumbani, babake, Nguru ashamtafutia mwanamke (zawadi) wa kuoa, Mumbi.

Mumbi anatoroka anapojua kuwa Charles ambaye alitakiwa kuolewa naye alikuwa na mpenzi mwingine. Anaishia kujiua. Naye Mary baada ya mazungumzo na Charles yanayoonyesha akili pevu na maono mapana kuhusu mustakabili wa jamii za Kiafrika anamuacha Charles anayeshikilia lazima amridhishe babake an kabila lake kwa kumuoa mwanamke waliyemchagulia.

Ploti ya mchezo huu imefumwa pia na hatua za kufunuka kwa laana inayomwandama babake Charles, Nguru. Alilaamiwa na babake kwa kumuoa mwanamke aliyekuwa hafai

kuolewa. Milio ya bundi na paka aliyosikia Mgeni yanaashiria maafa yanayotokea mwishoni mwa mchezo huu.

Nao mchezo wa *Kidonda Moyoni* ni mchezo unaoigiza athari za ukoloni katika asasi ya ndoa katika jamii zilizotawaliwa kikoloni. Ruhiu, mhusika mkuu, aliyekuwa mpigania uhuru wa Mau Mau anarejea nyumbani baada ya kuachiliwa huru na serikali ya kikoloni. Nyumbani anakuta kuwa mkewe alipata mtoto kutokana na kubakwa na Mzungu, mkuu wa wilaya. Ruhiu anaazimia kumuua mtoto huyo. Baadaye anapompata mkewe akiwa amekufa naye anaanguka na kufa.

Dhuluma alizofanyiwa kizuizini pamoja na waliotuhumiwa kuwa wapiganaji wa Mau Mau zinaonyesha udhalimu wa ukoloni. Aidha, kabla hiyo wazee 1 na 2 wanasimulia kumbukizi zilizompelekea Ruhiu aliyekuwa shujaa wa Mau Mau kukamatwa.

Mchezo wa kuigiza wa *Kesho Wakati Kama Huu* unaonyesha hali ya mijini ya mataifa ya Kiafrika katika kipindi cha baada ya uhuru. Serikali za mataifa haya zinaonekana kuwa za warithi wa ukoloni wanaoendeleza maslahi ya mkoloni. Matumaini ya wananchi ya wakati wa uhuru yameyeyuka. Serikali zao haziwajali na zinawajali wageni (watalii) kutoka mataifa ya Kimagharibi – ambao "wanachukizwa na uchafu ambao polepole unatambaa kwenye jiji letu ambalo lilikuwa lulu ya Afrika" (uk 40).

Ukoloni kwa watawaliwa kama wachuuzi, wanunuzi, Mtengeneza – makopo, Mshona – viatu haukuisha wakati wa uhuru. Unaendelezwa na tabaka la warithi wa ukoloni wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali serikalini.

**3.3 Mikakati ya Ugatuzi.**

**3.4.1 Maelezo ya kiethnografia**

Ethnografia ni maelezo ya kiutamaduni. Fasihi za baada-ukoloni hudhamiria kutoa ubainifu wa tamaduni za jamii za waliotawaliwa kikoloni. Kazi hizo huwa kama ethnografia za tamaduni za jamii za waandishi wa baada-ukoloni. Maelezo ya kiethnografia huipa kazi husika ladha ya kienyeji, pia muundo inapojengekea (Ashcroft na wengine 2002: 62). Kazi ya kifasihi lazima ijengeke katika muundo fulani wa kitamaduni ambao utavurugwa (katika mandhari ya kikoloni) na utamanduni wa kikoloni.

Katika *Mtawa Mweusi*, Ngugi amefanya jaribio la kuuwakilisha utamaduni wa jamii yake. Ingawa tamthilia hii inashughulikia masuala mapana ya kisiasa na matatizo ya mataifa ya bara la Afrika baada ya uhuru, tunapata chembe za utamaduni wa kabila la Marua ambalo ni kabila la Kiafrika. Chembe hizi ni taashira za utamaduni mzima na msomaji asiyeufahamu vizuri anajipata akishirikishwa katika mtalaa wake. Kwa maneno mengine, msomaji analazimika kuiweka tamthilia kando ili ajifahamishe kwanza na utamaduni wenyewe kama njia ya kupata maana katika tamthilia kwa ukamilifu.

Asasi ya ndoa katika utamaduni huu inadokezwa. Remi anapotoroka nyumbani anatoroka kanuni za utamaduni huo kuhusu ndoa. Kanuni zilizo wazi kwamba alifaa kumrithi mke

wa nduguye aliyekufa ili aendeleze jamaa yake. Ni njia ya utamaduni huo ya kuhakikisha kwamba kifo hakisambaratishi maisha ya jamii. Pengine tamthilia inalifafanua hili kutokana na kwamba mamake Remi hatakiwi kuolewa baada ya mumewe, Ngome kufa. Jamaa yake iliachwa ikiwa imara na hapakuwa na haja ya kupata mwanaume wa kuiangalia.

Ni asasi hii ambayo ukoloni unadhalilisha kupitia elimu inayowafanya wasomi wake wauone utamaduni wake haufai kufuatwa katika kuiendeleza. Remi msomi wa elimu hiyo anakiuka kanuni za utamaduni huo. Katika *Kidonda Moyoni,* ukoloni unamwondoa Ruhiu katika kutekeleza wajibu wake katika familia yake. Mkuu wa mkoa anambaka mkewe na kuidhalilisha ndoa hiyo. Aidha, katika *Kesho Wakati Kama Huu,* Njango anabaki kuiendesha familia baada ya mumewe kuuawa katika vita ya uhuru. Mandhari ya miji iliyoletwa na ukoloni ni tisho kwa utamaduni wa watawaliwa. Wahusika kama Remi na Wanjiro wanajipata wakiwa huru kutofuata utamaduni wa jamii zao. Remi anaanza mapenzi na msichana Mzungu, Jane naye Wanjiro anaazimia kuolewa na Asinjo, mtu wa kabila lingine. Charles, katika *Waasi* naye anataka kumuoa Mary, msichana ambaye pamoja na kuwa si wa kabila lake ametoka nchi nyingine, Uganda.

Katika kazi hizi za Ngugi, mifumo ya imani ya jamii husika inaangaziwa. Katika *Waasi*, Mgeni anapokutana na Mzee, mchezo unapofunguka, kutokana naye panajitokeza imani katika utamaduni wao ambapo amani inapokithiri sana huashiria mabaya. Mawazo yake yanaashiria falsafa nzito ya jamii hii kwamba maisha ni utaratibu wa mpishano wa furaha

na huzuni. Maisha hayakamiliki kwa furaha tu au huzuni. Baadaye anaeleza hofu yake kutokana na sauti za bundi na paka alizozisikia.

Mzee 1 anakubaliana naye kwamba sauti kama hizo huwa, *"nyaraka za Murungu"* (Mungu) (uk. 1). Hatari inayozungumziwa na Mgeni wakiwa na Mzee 1, tamthilia inaionyesha katika mtafaruku unaotokea katika arusi ya Charles anayopangiwa na babake. Ni hatari iliyopo katika kutoelewa utaratibu wa kuingiliana kwa tamaduni tofauti. Utaratibu ambao unafaa kutokea katika hali huru. Ndio ambao Mzee 1 anasherehekea anaposema:

*Mzee 1: ... mwana anatuletea pamoja naye busara yote ya mtu mweupe na kutupa sisi nguvu mpya pamoja na mila zetu. (uk. 7)*

Mwandishi pia anashughulikia imani kuhusu laana katika jamii yake. Katika *Waasi,* Nguru ni mwenye laana, kama adhabu ya kumuoa msichana asiyefaa kulignana na utamaduni wa jamii yake.

Laana yake inaleta athari kubwa ya kitanzia inapohusishwa na maafa yanayotokea katika arusi ya mwanawe. Kutokana na imani ya jamii yake:

*Mgeni: ...laana ni kama ugonjwa wa kuambukiza, unaweza kumshika yeyote yule aliyekaribu (na mlaaniwa) (uk. 5)*

Aidha, katika *Mtawa Mweusi*, Nyobi hachelei kuhusisha madhila ya jamaa yake katika laana. Anapoangazia kuhusu kifo cha mwanawe mkubwa, baadaye mumewe na kisha kutoroka kwa Remi anaishia kuamini kwamba mtu fulani aliilaani familia yake.

Wazee na kabila nao wanaamini katika dawa za ushirikina ambazo wanaamini zitawasaidia kumpata Remi. Hata hivyo, tamthilia ya *Mtawa Mweusi* inaiekua imani hii kwa wazee hawa kushindwa kumpata. Anaporudi, Remi anabaki kuwazomea kwa kuupalilia ukabila.

Thamani za jamii hii pia zinaangaziwa katika *Waasi.* Nguru anaonyeshwa kama mtu aliye na hadhi kubwa katika jamii yao. Kuwa tajiri, kuwa na wake wengi, bidii na kuweza kuimudu nyumba ni thamani za hali ya juu. Mtu aliye na sifa hizo hata jamii humpandisha kihadhi kuweza kuwa, *"kiungo cha jamii na mizimu"* (uk. 4). Hapa mdokezo wa metafizikia ya jamii hii unafanywa. Pana uunganifu wa ulimwengu halisi na ulimwengu wa mizimu (wafu). Katika *Kidonda Moyoni,* Ruhiu anaeleza kuwa ulinzi wake wakati wa vita ulitokana na mizimu. *"Mzimu wa watu weusi ulikuwa pamoja nami"* (uk. 24). Mpaka si dhahiri kama ilivyo katika metafizikia ya Kimagharibi.

Katika *Mtawa Mweusi* metafizikia hii inarejelewa ambapo pana ufungamano kati ya ulimwengu na binadamu. Hapa mgawo wa uwili unaopingana wa binadamu/visivyo binadamu unavunjwa. Thoni anaeleza kuwa ingawa ana masikitiko mengi atatafuta faraja katika miti, milima, ndege, mijusi, wadudu, nyota, mwezi na giza (uk. 6). Leopold Senghor (katika, July 1987: 29), Mbiti (1969:16) wanashadidia uunganifu huo kwa kueleza kwamba metafizikia ya Mwafrika (mtu mweusi) husisitiza uunganifu wa maumbile, mizimu na hata ambao hawajazaliwa.

Uunganifu huu unajitokeza pia Thoni anapotafakari kujiunga na ulimwengu wa waliokufa ili kujiepusha na adha za ulimwengu halisi kupitia mbinu rejeshi. Anakumbuka jinsi akiwa mtoto alivyokufa na kuuona utulivu wa ulimwengu huo.

> Thoni:..*kulikuwa giza sana huko, na kimya kabisa, giza lisiloonyesha chochote au maumivu, kicheko wala mateso; lakini amani tu...amani... nilipotoka nchi hiyo walisema nalikuwa nimekufa (uk.75).*

Hii ni metafizikia inayoendana na ya Kiafrika (katika jamii nyingi) ambapo mpaka baina ya uhai/kifo huwa si dhahiri. Huu ni uhalisia ulio tofauti na ule wa Kimagharibi ulio na msingi wake katika udhanifu wa Kimagharibi aliouwekea msingi Plato. Aidha, katika uhalisia wa jamii husika (ya Kiafrika) mgawo uwili wa ndoto / ukweli katika imani ya jamii hii haupo. Namna ndoto za Thoni na Nyobi katika *Mtawa Mweusi* (uk. 63) zinabashiri maafa yanayotokea mwishoni mwa tamthilia Remi anaporudi ndivyo inavyotokea katika ndoto ya Mzee I katika *Waasi* inavyobashiri maafa yanayotokea mwishoni mwa mchezo.

Katika utamaduni wa jamii ya mwandishi, suala la dini pia linagusiwa. Dini ya kabila la Marua inawasilishwa kwa taashira ya dua ya wazee wa kabila wanayoifanaya ili Muumba awawezeshe kumpata Remi katika *Mtawa Mweusi*. Dua hii inafuata utaratibu mahsusi ambapo kiongozi anakariri maneno fulani nao wazee wanayarudia nyuma yake. Dini hii ndiyo inayopingana na dini ya Kikristo. Mchungaji aliye mwenezi wake anapinga mila na desturi za kabila. Katika tamthilia nguvu anazozisimamia Mchungaji zinapingana na nguvu zinazosimamiwa na wazee.

Hali ya umahuluti na usebusebu wa kidini unajitokeza katika wahusika Nyobi na Thoni wanaojiona Wakristo. Hawaelekei kubobea katika dini hii ya kigeni. Dini hii inapinga mila na desturi za kabila lao lakini wahusika hawa hawafaulu kwa vyovyote kujiepusha na pingu za utamaduni huo wa kabila. Kwa mfano, Nyobi anaamini kuwa mfuatano wa maafa katika nyumba yake yanasababishwa na laana kutoka kwa mtu fulani (uk.7). Aidha, anapoulizwa na mzee ikiwa anaamini dawa ya ushirikina inayotumiwa kumrejesha Remi anaungama kuwa anaamini (uk. 12). Hii ni njia ya kuipindua dini ya Kikristo ambayo imeangaliwa na mwandishi kama asasi iliyotumiwa kuufanikisha ukoloni. Ni dini iliyotumiwa kuuhalalisha ukoloni. Dini hii iliwaaminisha Waafrika kuwa waliabudu miungu, imani iliyofaa kutupiliwa mbali. Katika shughuli zao wamishenari walitegemea ulinzi wa serikali zao za kikoloni.

Wahusika Nyobi, Thoni na Mchungaji hawaonyeshi kuielewa dini hii kwa kiwango ambacho kinaweza kuwafanya waitumie kuyaongoza maisha yao. Wanabaki kukariri dhana zake kikasuku. Kwa mfano, Nyobi anawapa baraka wazee ili kuweza kumrudisha Remi hivyo alishiriki ushirikina. Mchungaji naye badala ya kuwa katika hali ya kuielewa jamii yake ili aweze kuusambaza Ukristo anajitenga nayo. Anabaki kukashifu mila na desturi za Wamarua bila kuonyesha kuelewa ni kwa nini hazifai.

Suala lingine analolishughulikia Ngugi katika tamthilia zake kuhusiana na utamaduni ni dhana ya wakati. Dhana ya wakati katika tamthilia zake inajibainisha na ile ya Kimagharibi. Wakati dhana ya wakati katika utamaduni wa Kimagharibi huangaliwa

kihisabati, Mbiti (1969: 19) anaeleza kuhusiana na dhana ya wakati katika jamii za Kiafrika:

> *Kulingana na falsafa ya Kiafrika, dhana ya wakati huwepo katika kuhusishwa na matukio lakini sio kihisabati. Hivyo, wakati huundwa na matukio na hauwezi kutambuliwa katika ombwe tupu.*
>
> *(Tafsiri yangu)*

Hivyo, wakati katika muktadha wa kimapokeo wa jamii za Kiafrika hufasiliwa na matukio ambayo tayari yametokea, yanayotokea na yaliyo na uwezekano wa kutokea. Tukio ambalo halijatokea haliwezi kujumuishwa katika dhana ya wakati (Khj.17). Kwa namna hii, wakati una vivimbe viwili *(two dimensions)*: pana wakati mrefu uliopita na wakati wa sasa. Tukio linapotokea huingia katika wakati uliopita Hivyo, wakati katika tamaduni za kimapokeo za Kiafrika hufunuka kwa kuelekea nyuma kuliko kuangaziwa katika wakati ujao kama ilivyo katika utamaduni wa Kimagharibi. Dhana ya utambuzi wa wakati Kimagharibi ambapo pana wakati uliopita usio na mwisho, wakati wa sasa na wakati ujao usio na mwisho ni dhana za kigeni katika muktadha wa tamaduni za Kiafrika (khj).

Mintarafu hii tuna nyakati kama mafunguliang'ombe, jogoo wa kwanza na mafungianyama katika tamaduni za Kiafrika. Vivyo hivyo, tunapata utambuzi huu wa majira katika tamthilia za Ngugi. Katika *Waasi*, Mgeni anapowaona wanawake waliokuwa wamebeba mizigo ya kuni na chakula alibaini palikuwa na sherehe fulani, sherehe nyingine lakini haingekuwa tohara kwani hayakuwa majira yake (uk. 2). Katika

*Mtawa Mweusi*, Nyobi anashadidia ukweli huu anapotaja majira ya *"majilio ya mvua na kutoweka kwake" (uk.3)*.

Hata hivyo, utamaduni wa jamii ya mwandishi una baadhi ya mambo yasiyofaa katika maendeleo ya jamii ya baada-ukoloni. Ngugi anautathmini utamaduni wa jamii yake bila upendeleo wa kupofusha wanaohusishwa nao wanaharakati wa Unegritudi. Ikiwa wanaharakati wa Unegritudi hulaumiwa kwa kuuonyesha utamaduni wa Kiafrika kama utamaduni usio na ila (July 1987:223), Ngugi anauangalia katika uhalisia wake. Hasa katika *Mtawa Mweusi* anatathmini nafasi ya mwanamke katika utamaduni wa jamii yake.

Onyesho la kwanza, kitendo cha kwanza kinaangazia mazungumzo ya Nyobi na Thoni. Suala kuu linalojitokeza ni kuwa wanawake hawa wanalalamikia hali yao ya kudhalilishwa na mfumo wa kibabedume wa utamaduni wao. Thoni anamngoja Remi mumewe arudi. Anaungama kuwa hawezi kuishi bila mume. Remi naye mjini yuko huru kuwa na uhusiano na mwanamke wa Kizungu, wakati Thoni anatakiwa abaki nyumbani akingoja kuhurumiwa na mmewe. Hana uhuru wa kutoka katika hali hiyo hadi mmewe aamue. Nyobi naye anafungua moyo wake kueleza masikitiko yake:

*Nyobi:* *Nimeona maumivu ya mapigo,*
*Uchungu wa kuzaa na mapigo ya kifo,*
*Katika hayo nimejifunza jambo moja*
*Furaha ya mwanamke ni kukaripia watoto wake*
*Katika kuona vilio na tabasamu zao,*
*Kuwafanyia japo madogo wale uwapendao.*
*Mwanamke bila mtoto si mwanamke timamu*
*Lakini pamoja na hayo nimejifunza ya kwamba*
*Kusumbuliwa na kufedheheshwa hufuata furaha hii. (uk. 4)*

Kwa mujibu wa maelezo hayo, mwanamke katika utamaduni huu hana uhuru. Vilevile, dhana ya ushirikina inaangaziwa. Wazee wanaotumwa kumshawishi Remi arudi nyumbani wanatumia uchawi. Aidha, katika *Waasi,* suala la kumchagulia Charles mchumba linaonyesha upungufu wa utamaduni wa jamii hii.

Masuala ya kiutamaduni anayowasilisha Ngugi kama: asasi za kijamii kama ndoa, metafizikia ya jamii yake, dhana ya wakati na thamani nyingine za utamaduni wa jamii yake anafanya hivyo ili kuuangazia utamaduni wa watawaliwa wa kikoloni kama kitovu cha ina yake. Ni namna ya kuupa msisitizo. Hali hii inamfanya msomaji auelewe vizuri hasa thamani zake. Hali hii inaupa hadhi tena iliyodhalilishwa na ukoloni. Utamaduni wa kikoloni unapewa nafasi finyu hasa kuonyesha athari zake hasi kwa utamaduni wa watawaliwa.

### 3.4.2 Lugha na Fasihi ya Baada-ukoloni

Katika fasihi ya baada-ukoloni katika lugha za kikoloni, lugha ya kikoloni iliyoekuliwa hudhihirika. Kwa mfano, fasihi za baada-ukoloni katika lugha ya Kiingereza huwa katika Kiingereza kilichoekuliwa ili kiweze kubeba tajriba na utamaduni wa watawaliwa. Lakini katika kazi za fasihi zilizoandikwa kwa lugha ya watawaliwa, lugha ya Kiingereza na utamaduni wake hudokezwa ili kuonyesha tofauti iliyopo baina ya lugha na utamaduni huo na ule wa watawaliwa. Kuekuliwa na kupinduliwa kwa lugha ya kikoloni si mbinu tu ya fasihi ya baada-ukoloni bali pia ni sehemu ya maudhui ya upinduzi wa utamaduni wa kikoloni. Kuekuliwa kwa lugha ya kikoloni inayobeba utamaduni wake si kitendo chanya bali hasi kwani usanifu wake huumbuliwa.

Utamaduni na lugha ya kikoloni unapewa nafasi finyu. Katika tamthilia za Ngugi mdokezo wa utamaduni na lugha ya kikoloni zimepewa nafasi ndogo sana. Dhana hizo za kikoloni zimewakilishwa na asasi kama elimu inayoeleweka huuendeleza utamaduni na lugha hiyo. Hivyo, wahusika kama Charles katika *Waasi* Remi na Omange katika *Mtawa Mweusi* wanatumiwa kuwasilisha athari za utamaduni wa kikoloni.

Katika kipengele hiki cha ugatuzi tunatatizwa na dhana za kuwa tunashughulikia fasihi tafsiri. Baadhi ya nyenzo za ugatuzi za lugha huenda zisijitokeze katika tafsiri. Katika kazi za fasihi za baada-ukoloni zilizoandikwa kwa lugha za kikoloni maneno ambayo hayajatafsiriwa huwa wazi, kwani utamaduni wa kikoloni huashiriwa na lugha yenyewe na ule wa watawaliwa huwakilishwa na yaliyomo, mandhari, wahusika miongoni mwa mengine. Katika kazi zilizoandikwa kwa lugha za watawaliwa utamaduni wa kikoloni huwa pembezoni na athari zake hujitokeza katika baadhi ya wahusika, mandhari ya aina fulani au taashira nyinginezo.

Ngugi katika kazi tunazozishughulikia amewasilisha kazi zake katika tafsiri ya lugha ya Kiswahili. Kiitikadi lugha hii inatumiwa kufuatia mojawapo wa kanuni za fasihi ya baada-ukoloni za Kiafrika; kutumia lugha za watawaliwa (Taz. Sehemu ya msingi wa kinadharia) hata hivyo, utamaduni husika ni tofauti na wa lugha ya Kiswahili. Kwa namna hiyo ni rahisi kuorodhesha misemo, methali na nahau za utamaduni wa Gikuyu ambao Ngugi anauangazia. Utamaduni huo ndio msingi wa kazi za Ngugi tunazishughulikia.

Maneno mahsusi ya utamaduni husika ambayo hayajatafsiriwa hutumiwa katika fasihi za baada-ukoloni. Maneno haya hutumiwa kuonyesha ubainifu wa kitamaduni pamoja na kumshirikisha msomaji ili ajifahamishe utamaduni huo. Kimsingi, maneno hayo hayatolewi sherehe (maelezo). Hali hiyo hulazimisha msomaji kujifahamisha utamaduni husika, ambapo maneno hayo yana maana, kama njia ya kuelewa kazi hiyo. Tushaeleza mahali pengine (Sura ya pili) kwamba kusoma kazi ya kifasihi ya baada-ukoloni ni kuutalii utamaduni wa kazi husika. Hali hiyo huutilia msisitizo utamaduni huo. Kimsingi msomaji hutolewa nje ya kazi anayoisoma hadi katika mukdtadha wa utamaduni husika (Ashcroft na wengine 2002:63).

Katika mchezo wa kuigiza wa *Waasi*, neno *thahu*[2] (uk.5) halijatafsiriwa. Halijatolewa maelezo yoyote. Hii ni mbinu ya ugatuzi na huwa mwaliko kwa msomaji kuutalii utamaduni husika ili apate maana yake itakayomwezesha kuielewa kazi yenyewe. Kwa namna hii usomaji wa fasihi ya baada-ukoloni ni zaidi ya usomaji wa kazi yenyewe. Huwa ni mtalaa wa utamaduni wa watawaliwa unaohusika. Utamaduni huu unabainishwa na ule wa kikoloni na unapata hadhi ya juu kutokana na kuangaziwa.

Neno lenyewe ni taashira ya utamaduni wake. Katika muktadha wa matumizi yake ni zaidi ya neno lenyewe. Maneno kama hayo huonyesha masafa baina ya utamaduni wa kikoloni na ule wa watawaliwa.

Hapa hatuwezi kupuuza hata misemo, methali na nahau za utamaduni wa watawaliwa. Mbinu hizi hutoa busara iliyojengeka katika utamaduni huo na huashiria kwamba hakuna

utamaduni ulio na uhodhi wa busara. Kwa mfano, katika *Waasi* tunapata methali kama. *"Safiri uone kwamba si mama yako tu anayepika chakula kitamu" (uk. 3)*. Hii ni methali anayoitumia mgeni na inafumbata falsafa kwamba utamaduni husika unathamini tamaduni nyingine. Hakuna utamaduni usio na thamani zake.

### 3.4.3 Fasihi Simulizi Katika Fasihi ya Baada-ukoloni

Matumizi ya fasihi simulizi hudhamiriwa kuiwekea fasihi ya watawaliwa msisitizo. Katika muktadha wa ukoloni barani Afrika utamaduni andishi katika fasihi ni wa kigeni; uliletwa na ukoloni katika elimu yake. Fasihi ya mapokeo ya jamii za Kiafrika ni fasihi simulizi. Aidha, Chinweizu na wengine (1980:2) wanaeleza:

> *Fasihi simulizi ya Kiafrika ni muhimu katika mradi wa ukoloniishuaji wa fasihi ya Kiafrika. Hii Ni Kwa sababu fasihi simulizi ni hifadhi ya thamani, uhisishi, ujumi na mawazo ya kimapokeo ya Kiafrika na ubunifu ambao haujaingiliwa. Hivyo ni lazima fasihi simulizi iwe msingi, ielekeze na iwe nafasi ya kuanzia kwa fasihi huru ya Kiafrika.* (Tafsiri yangu)

Nukuu yao inafumbata umuhimu wa fasihi simulizi katika kuikolonishua fasihi ya Kiafrika. Aidha, Abiola Irele (1981: 9-24) anashadidia hili anapondai: *"Fasihi simulizi ndiyo fasihi ya kirasimi katika bara la Afrika"*.

Katika tamthilia zake, Ngugi ametumia dhana mbalimbali za fasihi simulizi. Anafanya jaribio la kuufuta mpaka baina ya fasihi andishi/fasihi simulizi. Katika udenguzi, kupindua mgawo uwili kama huo unaopingana hudhamiria kuufuta mpaka uliopo ili kushusha hadhi ya mgawo ulioangaliwa kuwa wa hadhi ya juu. Kimsingi tamthilia huwa ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa. Ni dhana hii ya uandishi iliyoingizwa na elimu ya

kikoloni katika utamaduni wa watawaliwa inayoshushwa hadhi kwa kuwekewa dhana ya usimulizi.

Katika *Mtawa Mweusi* ugatuzi huu unajitokeza. Kwanza ni kupitia kwa "*wimbo wa Afrika*" (uk. 63). Wimbo huu unaimbwa kuonyesha ushirikiano na umoja. Utanzu huu wa fasihi simulizi unaowasilishwa na watu wengi katika hali ya ujima unapowekwa katika tamthilia inayosomwa na mtu binafsi ni ishara ya ugatuzi. Kwa namna hii dhana ya tamthilia kama inavyojulikana inaekuliwa na inachukua umbo lililo baina ya fasihi simulizi na andishi.

Aidha, hadithi simulizi inatumiwa katika tamthilia. Remi anasimulia matukio yaliyomfanya aikimbie kabila lake katika muundo wa hadithi simulizi (uk. 34 – 9). Kwa muda utendaji unasimamishwa kuupisha usimulizi huo. Usomaji wa sehemu hiyo unaibua dhana ya fasihi simulizi. Kwa maneno mengine, msisitizo unatolewa kutoka tamthilia (inayofungamana na utamaduni andishi) hadi hadithi simulizi (inayofungamana na utamaduni simulizi). Aidha, hatuwezi kupuuza mhusika, Remi ambaye amekengeushwa na elimu ya kikoloni na anatumiwa katika kuisimulia. Pamoja na kwamba inazua, katika usomaji, hali ya kumsikitikia kwa hali aliyopo na mkakati wa kuigatua elimu ya kikoloni katika kuupindua mgawo uwili unaopingana wa elimu rasmi/elimu isiyo rasmi. Hapa elimu rasmi inafungamana na elimu ya mfumo wa kikoloni aliyoipata Remi nayo elimu isiyo rasmi inafungamana na elimu ya kimapokeo ya jamii yake.

Mchezo wa kuigiza wa *Waasi* unaangazia utanzu wa nyimbo ulio wa fasihi simulizi. Wimbo wa arusi (uk. 14) ambao haujatafsiriwa unaimbwa katika kuihui sherehe ya arusi ambayo inaelekea kufanyika. Aidha, Mumbi anapokufa, mwandishi anaelekeza ngoma ya kifo ibuniwe. Kwa hali hii fasihi simulizi ya watawaliwa inashirikishwa kutolewa kutoka upembezoni hadi katika kitovu cha fasihi. Hivi inainuliwa kihadhi. Nyimbo hizi pia zinaleta hali ya uunganifu wa fasihi na uamilifu wake katika maisha ya watawaliwa. Fasihi katika jamii hii haiwi ya kuchangamsha tu au amali ya mtu binafsi bali ni mali ya jamii na hufungamana na matukio yake ya kijamii.

Katika *Kidonda Moyoni* pia usimulizi unapewa nafasi kubwa. Hali iliyopelekea kuwekwa kizuizini. Kwa mhusika mkuu Ruhiu inasimuliwa na wahusika Mzee 1, 2, na Kiongozi (uk. 19-22). Ni hali inayoekua utanzu wa tamthilia. Mpaka baina ya hadithi simulizi / tamthilia unafutwa katika kutoa hali ya kuutukuza utanzu wa tamthilia ulio na chimbuko katika utamaduni wa Kimagharibi na hadithi simulizi zilizo za watawaliwa wa jamii ya mwandishi. Aidha, ni hali ya kuitilia msisitizo fasihi simulizi.

Vilevile, katika *Kesho Wakati Kama Huu,* mpaka wa tamthilia na fasihi simulizi si dhahiri. Mathalan matukio yaliyopelekea hali walio nayo watawaliwa inasimuliwa na wahusika, Njango na Mshona-viatu. Sauti ya Mwandishi (mhusika) inaupa mchezo huu sifa za hadithi simulizi. Usimulizi wake unawasilisha matukio kama yanavyofunuka. Pamoja na usimulizi pana pia utanzu wa nyimbo, kwa mfano, wimbo anaoueleza Mshona-viatu (uk 43) waliuimba ili kujipa moyo wa ushirikiano katika kupambana na mkoloni.

Kwa kifupi kazi hizi za Ngugi zinafuta mpaka baina ya fasihi andishi na fasihi simulizi. Hasa usimulizi na uimbaji zinachukua nafasi kubwa kuliko utendaji kinyume na inavyotarajiwa katika tamthilia. Hii inatilia msisitizo fasihi asilia ya watawaliwa.

**3.4.4 Uandishi Tena wa Historia**

Mojawapo wa sababu za kuandika fasihi za baada–ukoloni ni kuandika historia tena kutoka kwa mkabala wa watawaliwa wa kikoloni. Hii ni kutokana na sababu kwamba ukoloni ulipotosha historia ya watawaliwa. Wanamuundo-leo wamedai kuwa hapawezi kuwa na historia moja na wana maoni kwamba maisha ya watawaliwa wa ukoloni yanaweza kuangaliwa tu kupitia kwa "*historia nyingi*" (Loomba 1998:13).

Madai haya ya wanamuundo-leo yanaelekeza katika mjadala kuhusu lugha na utamaduni. Lugha hubeba utamaduni na historia ya jamii husika (Wa Thiong'o 1993: 30). Kwa hali hii mchakato wa ukoloni uliyoipa elimu ya Kimagharibi na lugha ya Kimagharibi hadhi ya juu ikilinganishwa na elimu za kimapokeo na lugha za watawaliwa ilianzisha utaratibu wa kudumaza lugha, utamaduni na historia ya watawaliwa. Katika hali hii ni muhimu fasihi ya baada-ukoloni iandike tena historia ya jamii husika katika mkabala wa watawaliwa wa kikoloni.

Tamthilia za Ngugi zinaiangazia historia ya jamii yake iliyodhalilishwa na ukoloni. Katika tamthilia hizi anapinga historia pendelevu ya kikoloni inayoangazia upande wa mkoloni tu. Kwa mfano, mwanafalsafa wa Kijerumani, Hegel katika mihadhara yake kuhusu falsafa ya historia alidai kuwa bara la Afrika lilipitwa na historia (Irele 2002:

113). Ni hali hii ya kurekebisha upotoshi ulioitenga Afrika kutokana na mchakato wa historia ya ulimwengu anayoitikia Ngugi.

Katika *Kidonda Moyoni,* mwandishi anaandika historia ya jamii yake kutoka kwa mkabala wa watawaliwa. Mzee 1 na 2 wanasimulia kuhusu harakati za wapigania uhuru. Ujasiri wa Ruhiu na wenzake unajitokeza wazi. Mashujaa hawa waliingia msituni kupigana, Hali ya Hatari ilipotangazwa. Ujasiri wa Ruhiu unajitokeza kutokana na kutowasaliti wenzake hata baada ya kutesewa kizuizini. Aidha, historia hii ya ukoloni Ruhiu anaielezea,

> *Ruhiu: Kwa karne nyingi mtu mweupe anawauza watu weusi kwa vipande thelathini vya fedha, kwa faida ya jamii ya watu weupe. Amewatumia watu weusi, jasho jeusi, utajiri mweusi kujengea miji yake na viwanda (uk. 23).*

Kinachojitokeza hapa ni historia inayopindua "*historia*" kwa mtazamo wa Kimagharibi inayoangazia watu maarufu huku ikipuuza watu wa hali ya chini (wa kawaida). Kwa Ngugi, wahusika kama Mshona-viatu, Mtengeneza–makopo, mumewe Njango na wengine ndio viwakilishi halisi vya watu wanaoiunda historia. Hivyo, katika, *Kesho Wakati Kama Huu* shujaa Dedan Kimathi anarejelewa miongoni mwa wahusika ambao walishiriki katika vita vya ukombozi. Historia hii ndiyo inayomfanya Njango kuona kwamba vita anavyopigana Mgeni (vya kuzuia Halmashauri ya Jiji) kubomoa vibanda vya watu maskini) na vita alivyopigana mumewe (vya kumwondoa mtu mweupe) havina tofauti. Tabaka ndogo lililochukua madaraka kutoka kwa wakoloni liliendeleza ukoloni.

Ngugi anaibomoa historia iliyofumbia macho mchango wa wanawake katika maendeleo ya kijamii. Mathalan, nafasi ya wanawake katika vita vya uhuru inaakisiwa na wahusika kama Njango, mkewe Ruhiu, Wangari katika *Kesho Wakati Kama* Huu na Nyobi na Thoni katika *Mtawa Mweusi.* Wanawake hawa wanajitokeza kama mihimili ya jamaa zao katikati mwa misukosuko ya ukoloni. Mwandishi anawaonyesha pia kama mashujaa wa aina yake.

### 3.4.5 Uhusika na Mandhari Katika Fasihi ya Baada-ukoloni

Uhusika na mandhari ni dhana zinazojitokeza kama mikakati ya ugatuzi. Wahusika wanaoakisi hali ya watawaliwa katika mandhari ya utamaduni wao wameangaziwa. Hali hii inapindua fasihi ya kikoloni iliyosisitiza orodha kuu ya Kimagharibi. Wahusika katika tamthilia za Ngugi wameonyeshwa wakipambana na mazingira yao katika kujaribu kuwa na maisha yenye wiano. Aidha, masuala yanayoshughulikiwa yanawahusu wahusika watawaliwa. Ukoloni, ukoloni mambo-leo, ukabila, matabaka, dini, ukengeushi na mengineo ni masuala ambayo mwandishi ameyashughulikia katika tamthilia zake. Aidha, ni masuala nyeti yanayowakabili wahusika katika muktadha wa ubaada-ukoloni.

*Katika Mtawa Mweusi,* Thoni na Nyobi ni wahusika wa kike wanaosawiriwa katika hali asili ya maisha ya watawaliwa. Mazungumzo yao yanaupa mchezo ladha ya maisha halisi ya watawaliwa. Wanalalamikia hali zao katika utamaduni unaodhibitiwa na ubabedume. Aidha, wahusika wengine katika tamthilia hii wana uamilifu kama huo. Mgogoro uliopo unaoigawa jamii ya tamthilia katika makundi tofauti unaakisi maslahi mbalimbali ya jamii hiyo ya baada-ukoloni. Kila kundi (wazee wa kabila, jamaa yake Remi, Mchungaji)

linapania kutosheleza maslahi yake. Wahusika kama Jane na Omange nao ingawa wako nje ya utamaduni msingi wa tamthilia wanakamilisha picha ya jamii hiyo ya baada-ukoloni.

Nao mchezo wa *Kesho wakati kama huu* unawakilisha mandhari ya mijini yaliyoletwa na ukoloni. Wahusika wanaokaa katika mtaa wa vibanda kama Njango na Mshona- viatu walilazimika kuhamia mjini ardhi yao ilipotwaliwa na walowezi. Utamaduni hujengeka katika mandhari fulani mahsusi pamoja na wahusika. Katika *Kesho Wakati Kama Huu* pamoja na wahusika kukengeushwa kutokana na ardhi yao vilevile wamekengeushwa kutokana na utamaduni wao. Ukoloni ulizingatia ukweli huo na ndipo tunapata hata watawaliwa waliotolewa katika ardhi yao na kuwekwa katika kambi za vizuizi. Mazingira ya mjini huleta tamaduni tofauti pamoja na hivyo hali ya umahuluti na usebusebu wa utambulisho. Mathalan tunampata Remi, Omange na Jane (waliotoka katika tamaduni mbalimbali) katika *Mtawa Mweusi* wakiingiliana. Aidha, katika *Kesho Wakati Kama Huu*, Wanjiro haelewi ni kwa nini mamake anamkataza kuolewa na Asinjo ambaye si wa kabila lao.

Katika *Mtawa Mweusi* pana mandhari ya aina mbili. Shambani na mjini. Katika mandhari ya shambani tunapata jamii zinazoishi huko zinasawiriwa zikiongozwa na muundo fulani wa utamaduni. Ingawa kuna kani kama dini ya ukristo zinazojaribu kuingilia muundo huo hazielekei kufua dafu. Misingi ya utamaduni katika mashamani ni imara. Hii inaonyeshwa na wahusika kama Nyobi na Thomi ambao hata kama ni Wakristo bado

pingu za utamaduni zinawadhibiti. Haya ndiyo mandhari asili ya utamaduni huo. Dini ya kabila la Marua ingali imara na inaendelea kuongoza wafuasi wake.

Mandhari ya mjini anakotorokea Remi, ni ya Kigeni. Miji ilitokea katika wakati wa ukoloni kutokana na haja ya kuwa na vituo vya utawala wa serikali za kikoloni. Hapa Remi yuko huru kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Jane bila kuzuiwa na kanuni za utamaduni wake.

Utawa anaohusishwa nao Remi ni wa kitashtiti. Utawa ni dhana isiyo ya utamaduni wa jamii yake. Ni dhana ya dini ya kikristo iliyofungamana na ukoloni. Mtawa hudhamiria kutafuta ukweli fulani kuhusiana na dini. Lakini utawa wa Remi unakosa kiini. Anaporudi kijijini na kudai, *"Sasa nafahamu yote. Kukaa kwangu mjini kumenifundisha kila kitu"* (uk. 72), msomaji anakosa kuelewa mambo anayorejelea Remi. Mwandishi hajamkuza mhusika huyu katika hatua za kujitambua. Hali hii inaweza kuangaziwa kuwili. Kwanza, inaweza kurejelewa kama upungufu katika utunzi. Pili, inaweza kurejelewa kama mbinu ya kimaksudi ya kuiekua elimu ya Kimagharibi inayoleta mfarakano katika jamii za watawaliwa wa kikoloni. Maneno anayoyatamka yanajitokeza kama ya kupachikwa tu. Ikiwa Remi alikuwa amepata ukweli fulani ambao hakuwa anaujua mwanzoni basi angeweza kutatua suala la ndoa alilolitoroka. Anabaki kuwa mfano bora wa wasomi fidhuli wanaojiona kuwa bora kuliko watu wengine.

Remi hapa anawekwa katika hali ya kudhihakiwa kwa kuutoroka utamaduni wake. Mamake katika kumuasa anaonyesha busara ya kimapokeo na upofu alio nao Remi kuhusu utamduni wa jamii yake.

*Nyobi:* *Mwanangu. Usiingie kiwi kwa mwako*
*Utakaowaka usiku na kesho umezimika, kuwa majivu na makaa. Tunza nyumba yako, na humo utaona moto uwakao usiku na mchana kati ya mafiga matatu. Mna chakula na joto la uzima vinavyokungoja. (uk. 71)*

Katika mandhari ya watawaliwa, mwandishi anawafanya wahusika kumfasiri mkoloni kutoka kwa mkabala wao. Huu ni upinduzi wa mtalaa wa mkoloni uliomfasiri mtawaliwa kutoka kwa mkabala wa mkoloni mwenyewe. Kwa mfano, katika novella maarufu ya Joseph Conrad, *Kiini cha Giza,* watawaliwa wa nchi ya Kongo wanasawiriwa kwa taswira hasi. Watu weusi wanasawiriwa kama: wajinga, wenye nyuso za kutisha, wenye maumbo madhubuti, wenye macho makubwa yasiyopepesa, wala mizoga, wanaonuka miongoni mwa taswira nyingine hasi. Wahusika wa tamthilia za Ngugi nao wanawafasiri wakoloni. Mkoloni, kwa mfano, katika *Kidonda Moyoni,* anaelezwa kama kiumbe dhalimu, anayekandamiza wengine, mwizi wa raslimali na mbakaji. Kulingana na Ruhiu mkoloni anafaa kuondolewa kwa namna anavyoazimia kumuua mtoto aliyezaliwa kupitia kitendo cha ubakaji. Ruhiu anazua taswira ya bara la Afrika kupitia kwa mamake:

*Ruhiu:* *Kwako, wewe, mama wa Afrika yetu na wa jamii nyeusi, nawiwa maisha yangu. (uk. 23)*

Aidha majina ya wahusika wa tamthilia hizi yanaakisi utamaduni wa jamii yao. Majina kama Ruhiu, Wanjiro, Nyobi, Thoni, Mumbi, Nguru yana maana tu katika utamaduni

wake. Majina ya Kiafrika huwa na maana, hubeba ama historia au hueleza dhana fulani. Haya yote hutokana na utambuzi wa kidini au namna wanavyofasiri kuwepo kwao. Majina hayo hubeba dhana zinazohusishwa na mwenye jina husika kama; kabila, ukoo, familia, na dhana nyingine (Osabutey-Aguedze 1990:206). Maana inayobebwa na majina hayo inajikita katika utamaduni wa jamii yao. Kwa mfano, Ruhiu ni jina linalomaanisha upanga; katika *Kidonda Moyoni* ndiye anayeongoza vita vya "kuukata" ukoloni katika jamii yake. Majina haya ni taashira ya utamaduni husika na yanawekwa sambamba na majina mengine kama Remi, Charles, Mary, Jane yanayoonyesha ufungamano wao na utamaduni wa kigeni.

### 3.5 Hitimisho

Katika sura hii tamthilia za awali za Ngugi: *Mtawa Mweusi* na *Kesho Wakati Kama Huu* zimehakikiwa ili kubainisha namna zinavyougatua utamaduni wa kikoloni. Mikakati ya ugatuzi inayojitokeza ni: kuekuliwa kwa lugha ya kikoloni, maelezo ya kiethnografia, matumizi ya fasihi simulizi, uhusika na mandhari na uandishi tena wa historia. Kimsingi, kazi hizi za awali hazionyeshi msimamo dhabiti wa mwandishi katika uandishi wa fasihi ya baada-ukoloni. Hata hivyo, baadhi ya masuala ya baada-ukoloni yanajitokeza kama tulivyoeleza. Kiujumi kazi hizi ni hafifu. Kwa mfano, wahusika wakuu kama Charles katika *Waasi* na Remi katika *Mtawa Mweusi* wanaelekea kuwasilisha ujumbe uliopachikwa. Kujigundua kwa wahusika hawa hakujakuzwa kihatua ili kubainika kimantiki.

Masuala ya kitamaduni tuliyoyashughulikia katika sura hii ni yale ambayo mwandishi anayaonyesha kama namna ya kuangazia utamaduni wa watawaliwa wa kikoloni. Hivyo, anaupa utamaduni huo msisitizo. Hali hii inamuweka msomaji katika hali ya kuuelewa utamaduni wa jamii husika vizuri hasa thamani zake zilizodhalilishwa na ukoloni. Hali hii inaupa hadhi tena utamaduni huo. Utamaduni wa kikoloni unapewa nafasi finyu hasa kuonyesha athari zake hasi kwa utamaduni wa watawaliwa.

**Tanbihi**.

[1] Katika makala yake ya *Can the Subaltern Speak* (1985) (Taz. Loomba 1998:233-4), anatoa tahakiki ya uwakilishwaji wa sauti za jamii za watawaliwa wa kikiloni na waandishi katika jamii hizo.

[2] Thahu ni neno la lugha ya Gikuyu linalomaanisha najisi au uchafu unaoweza kumkirihi mtu. Mtu mwenye Thahu hafai kuingiliana na watu wengine asiwapake uchafu. Mtu anayeingiliana naye huonekana kuwa sawa naye.

# SURA YA NNE

## 4.0 UGATUZI KATIKA *MZALENDO KIMATHI* NA *NITAOLEWA NIKIPENDA*

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia tamthilia ambazo Ngugi ameshirikiana na Waandishi wengine kuziandika. Tamthilia hizi ni *Mzalendo Kimathi* (1978) waliyoiandika na Micere Mugo na *Nitaolewa Nikipenda* (1982), waliyoiandika na Ngugi wa Mirii. Suala la ushirikiano katika uandishi hasa katika kazi za kibunifu huleta utata katika kubainisha mchango wa kila mwandishi. Hata hivyo, ni rahisi kutambua mwendelezo wa msimamo wa kiitikadi kutoka kazi za mwandishi mwenyewe hadi zile alizoziandika kwa ushirikiano. Vilevile, kwa kuangalia uandishi wa kijumla wa waandishi watatu wanaohusika ni rahisi kutambua kwamba msimamo wa kiitikadi wa Ngugi wa Thiong'o unatawala. Hivyo, utafiti unaojishughulisha na kazi zake hauwezi kupuuza kazi hizi kwa kusingizia kuhusika kwa waandishi wengine.

### 4.2 Kuhusu Kazi Husika

#### 4.2.1 Muhtasari wa Tamthilia ya *Mzalendo Kimathi*

Tamthilia ya *Mzalendo Kimathi* inawakilisha historia ya mapambano ya uhuru nchini Kenya. Waandishi wanafanya hivyo kwa kuunda ploti inayoangazia mashtaka anayofanyiwa shujaa Kimathi katika mahakama ya kibeberu. Ploti ya mchezo huu ni changamano. Mbinu rejeshi imetumiwa kuangazia kwa upana mapambano ya wapigania haki za watawaliwa. Kimathi ameangaziwa zaidi kama ishara ya ujasiri wa mashujaa waliopigania haki. Hili linaonyeshwa kupitia kurejelewa kwa mashujaa wengine kama: Waiyaki, Me Katilili, Mbatiani, Koitalel miongoni mwa wengine. Aidha, uhusika mpana

wa wahusika wasiobainishwa kwa majina halisi kama Mwanamke, Mvulana, Msichana na Askari ni uhusika unaodhamiria kuonyesha ujenzi wa historia uliofanywa na watu wa kawaida katika jamii. Wahusika mvulana na msichana ambao ni watoto ni ishara ya kivikale na wanaonyesha vizazi vya jamii. Vizazi hivi ndivyo vinavyobeba matumaini katika mustakabali wa jamii husika.

Kwa hali hii tamthilia kama drama iliyoandikwa inaakisi dhima ya kijamii ya drama: kufunza hasa watawaliwa namna ya mapambano ya kuzipata haki za kijamii. Tamthilia hii inamwonyesha Kimathi kama mfano wa kuigwa katika harakati za kiukombozi. Yeye anajitolea hadi katika kifo mikononi mwa mkoloni bila kupwaya katika msimamo wake wa kuvunjilia mbali udhalimu wa kikoloni.

Hata hivyo, mapambano hayo yanakwazwa na usaliti. Kuna kundi la waliopata elimu ya kikoloni, kwa mfano, wenye mabenki, wafanyabiashara, Padri na wenye tamaa za kujinufaisha kwa gharama ya ukandamizwaji wa watawaliwa. Hata miongoni mwa wapiganaji wapo waliojisalimisha, kwa mfano, Gati, Hungu, Gaceru na Wambararia, nduguye Kimathi.

Umoja unaoashiriwa na nyimbo zinazoimbwa kwa pamoja na matumaini miongoni mwa wahusika kama Mwanamke, Mvulana na Msichana ni silaha aali katika mapambano ya watawaliwa dhidi ya ukoloni. Suala la nyimbo au fasihi simulizi kama itakavyojitokeza katika sehemu ya mikakati ya ugatuzi zinajitokeza kama usemi wa kuupinga ukoloni. Aidha, kauli wanayoitoa waandishi wa mchezo huu ni kuwa historia ya jamii za Kiafrika

iliundwa na watu wa kawaida. Mintarafu hii uhusika wa Mwanamke, Msichana, Mvulana na wapiganiaji haki (umati) unadhamiriwa kutoa fasiri pana isiyosimikwa katika mtu binafsi katika uundaji wa historia.

Kuhusiana na shujaa Kimathi, matukio muhimu ni mashtaka anayofanyiwa mahakamani mara tatu, vishawishi vinne akiwa gerezani na akiwa kiongozi wa mapambano msituni. Hotuba anazozitoa pamoja na anavyoelezewa na wahusika wengine ndiyo yanayomjenga kama shujaa.

Askari wa Kwanza na wa Pili wanasimamia mikinzano iliyopo katika msimamo wa watawaliwa katika mapambano. Askari wa Kwanza anaonyesha kuchanganyikiwa kuhusu upande upi auunge mkono. Lakini mwishoni, wimbi la mapinduzi linapovuma anajipata akichukuliwa nalo na kuungana na wapigania haki wengine katika wimbo wa ukombozi. Askari wa Pili ashachukua upande wa wakoloni.

Kupitia mashtaka kortini, Kimathi anaandaliwa jukwaa la kutoa malalamiko ya dhuluma wanazofanyiwa watawaliwa. Kwa namna hiyo mashtaka ya kortini yanapinduliwa, hakimu na wakoloni wenzake wanaishia kushtakiwa kutokana na udhalimu wao. Hakimu anabaki kukariri mashtaka ilhali Kimathi kila wakati anaendelea kuukashifu ukoloni. Hukumu ya ukoloni ni wito wa Kimathi wa kuendeleza mapambano hadi ung'atuliwe.

### 4.2.2 Muhtasari wa Tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda*

Tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* inaigiza hali ya Kenya baada ya uhuru. Hata hivyo, historia inayopelekea hali hiyo imeigizwa kupitia mbinu rejeshi. Hata hivyo, tukio kuu linaloangaziwa linahusu usaliti ulioanza wakati mfupi baada ya uhuru. Gicaamba anaeleza mahali matatizo yao yalipoanza,

Gicaamba: *Nchi hii yetu ilikwenda kombo*
*Wakati baadhi yetu waliposahau walivyoapa*
*Wakasahau ushirikiano wa wananchi*
*Wakazingatia shabaha za wasaliti*
*Wakasema...hapana ndege mwenye mdomo wa kudonoa amdonoyeaye ndege mwingine (uk. 107)*

Usaliti huu unaonyeshwa kupitia wahusika, Kioi, Ikuua, Ndugire pamoja na wageni kutoka mataifa ya Ujerumani, Amerika na Ujapani. Wahasiriwa ni wafanyakazi na mafalahi kama Kiguunda na Gicaamba. Dini za kigeni zinapigiwa tashtiti kwa namna ambavyo zinatumiwa kuhalalisha ukoloni mkongwe na ukoloni mambo-leo. Dini hizi zinarejelewa kama "ulevi wa moyo" na "uchawi wa mawazo" (uk. 62). Dhana za kisemiotiki zinazowakilishwa na maneno "ulevi" na "uchawi" haziwezi kupuuza katika muktadha huu. Katika muktadha wa jamii za Kiafrika uchawi na ulevi ni dhana hasi zinapohusishwa na mtu. Hivyo, zinapotumika hapa zinakuwa sehemu ya mtalaa wa kuupindua ukoloni na hasa dini za kigeni zilizoletwa na ukoloni huo. Dereva wa trekta katika shamba la Kioi anasifiwa na waajiri wake kwa kuwa yeye hadai nyongeza za mshahara na hufanya kazi kwa bidii huku akimsifu Yesu. Kwa maneno mengine, ni mtu aliyekengeushwa na uhalisia wa mazingira yake.

Unafiki wa kidini uliokithiri unaonyeshwa na familia za Kioi na Ndugire ambao ni matapeli wanyonyaji ambao ni wepesi wa kutumia dini kuhalalisha unyonyaji wao. Kwa mfano, Ndugire anaeleza kuwa ni Mungu aliyewaelekeza waende benki kuchukua mkopo ili kukistawisha kishamba chao bila hata kutoa hata senti moja mfukoni.

Mchakato ambao Kioi anautumia kumnyang'anya kiguunda kijishamba chake cha ekari moja na nusu ndio unaounda ploti ya mchezo huu. Ni hali inayoonyesha namna masikini wanavyoumbuliwa utu wao chini ya ubepari. Kioi anahitaji kijishamba cha Kiguunda kwa niaba ya wageni wa Ujerumani, Amerika na Ujapani wanaotaka kujenga kiwanda cha kutengeneza dawa za kuulia kunguni. Ni kiwanda ambacho kinatoa harufu mbaya na kwa hivyo kilipaswa kujengwa mbali na makazi ya "waheshimiwa" mabepari.

Kijumba kidogo cha Kiguunda ndicho kinachotumiwa kama mandhari kuu ya mchezo. Hati ya ardhi inachukua nafasi muhimu na hata maelekezo ya uigizaji yanapendekeza ipewe nafasi ya kati. Mandhari haya yanachangia sana katika kujenga maudhui ya tamthilia na katika kutoa teleolojia yake.

Mvutano wa vizazi pia unaonyeshwa kupitia uhusiano wa Gathoni na wazazi wake. Kinyume na matakwa ya wazazi wake, Gathoni anatoka nyumbani na kuandamana na mwanawe Kioi, John Muhuni. Kioi, Jespheli, Ndugire na Helina wanapotembelea familia ya Kiguunda na kupendekeza Kiguunda na mkewe wafanye arusi ya kanisani mchezo unachukua mkondo mwingine. Wangeci mkewe anafikiria kuwa Kioi na mkewe walitaka wafanye arusi ya Kikristo ili wanao nao wafanye yao. Ingawa Kiguunda anakataa kwanza

akidai kuwa alimuoa Wangeci, mkewe Kiguunda kufuatana na mila na desturi zao kihalali, baadaye anasalimu amri. Gicaamba na Njooki walio sauti ya urazini katika tamthilia wanawatahadharisha kuhusu kujiingiza katika uhusiano na mabepari. Lakini Kiguunda na mkewe wanakaidi.

Kiguunda anapoomba Kioi amsaidie ili aweze kugharimia arusi yao anashauriwa apeleke hati ya ardhi katika benki ili apewe mkopo. Ni katika onyesho la tatu ambapo mabadiliko makubwa yanaonyeshwa katika nyumba ya Kiguunda, kila kitu ni kipya. Mahali palipotundikwa hati ya ardhi sasa pana kibao chenye maandishi "Kristo ndiye mkuu..." na picha ya Nebukadinezari (uk. 88). Maandishi haya na picha yamewekwa pale kitashtiti. Namna Nebukadinezari alivyokuwa mfalme mkandamizaji wa Babuloni ndivyo nao ukoloni ulivyo. Kwa hakika Kioi kwa namna anavyomnyanyasa Kiguunda haonyeshi kuwa tofauti na Nebukadinezari. Kwa mtazamo mwingine, picha hiyo na maandishi hayawezi kuchukua nafasi ya hati ya ardhi kama yanavyoonyeshwa. Ikiwa hati ya ardhi inawapa jamaa ya Kiguunda hisi za kuwepo, matumaini na uhai, picha ya Nebukadinezari na maandishi, "Yesu ndiye Mkuu..." hayajitokezi kuwa na maana yoyote kwao.

Hata hivyo, mtindo huu wa Ngugi unajitokeza kuwa kinaya. Kwa hakika, dini ya Kikristo ilitumiwa kufanikisha ukoloni hivyo mradi wa ukolonishuaji hautarajiwi kutumia asasi hizo zilizotumiwa katika ukoloni. Anaelekea hivyo kuhalalisha asasi hizo na hivyo kujikanganya anapozitumia katika mtalaa wa ukolonishuaji.

Kiguunda na Wangeci wanaigiza arusi bunifu kanisani, kwa kujitayarisha kwa arusi ya kweli. Uigizaji wao unakatizwa na Gathoni, mwanao, anayeingia akilia kwa kuachwa na John Muhuni akiwa na mimba.

Kiguunda na mkewe wanawaendea Kioi na Jespheli kuwataka arusi ya Muhuni na Gathoni ifanywe kwanza lakini wanapokelewa kwa kero wanapolaumiwa kwa kutomlea mwanao kikristo. Kiguunda anamtolea Kioi sime na kumtaka atie saini kukubali ndoa ya wanao lakini Jespheli anakatiza juhudi zake kwa kumtolea bunduki.

Katika onyesho la mwisho vyombo alivyonunua Kiguunda kwa mkopo kutoka benki vimetwaliwa baada ya kushindwa kulipa. Maisha ya familia ya Kiguunda ni ya kusikitisha. Shamba lao linanunuliwa na Kioi. Kiguunda anaingilia ulevi. Mwanawe naye anaingilia umalaya huku Wangeci akiomboleza maafa yaliyowapata. Kwa mara nyingine Gicaamba na Njooki ndio wanaotokea kuwashauri namna ya kujiendeleza tena.

Kupitia ploti hiyo, waandishi wameweza kuzungumzia maudhui ya aina mbalimbali. Tamthilia inawakilisha ushirikiano wa kiujima kupitia kutumiwa kwa ngoma na nyimbo kutoka kwa maisha ya kijamii. Lugha ya tamthilia inaakisi maisha ya kila siku ya jamii ya tamthilia.

### 4.3. Mikakati ya Ugatuzi

#### 4.3.1 Maelezo ya Kiethnografia

Waandishi katika *Mzalendo Kimathi* na *Nitaolewa Nikipenda* wameshughulikia yaliyomo katika muundo wa utamaduni mahsusi wa jamii ya Gikuyu. Msomaji katika tamthilia hizi anapitishwa katika mfumo wa utamaduni wa jamii ya Gikuyu ili kuonyeshwa namna unavyojipambanua na ule wa Kimagharibi. Hali hii inaugatua utamaduni wa kikoloni na kuupa nafasi ya kati utamaduni wa jamii ya waandishi iliyotawaliwa kikoloni. Utamaduni ni namna ya maisha wanavyoishi watu fulani katika kipindi mahsusi cha kihistoria katika kuitikia changamoto za hali za kijamii, kisiasa na kiuchumi (Lo Liyong 1972: ix). Jamii huwekea seti ya thamani nyanja zake mbalimbali za kimaisha na thamani hizo husaidia wanajamii wake kujiangalia kupitia kwazo. Vilevile, utamaduni huelekeza yanayostahili kufanywa na wanajamii na yasiyostahili. Kwa mfano, kuhusiana na taratibu za ndoa matambiko ya wakati kifo kinapotokea miongoni mwa mengine (Lo Liyong 1991:29). Kazi za kifasihi kama taashira ya maisha ya jamii fulani huweza kuangazia tu baadhi ya nyanja za kitamaduni kutokana na upana wake. Hivi tamthilia tunazozishughulikia nazo zinateua baadhi ya masuala ya kitamaduni kuyashughulikia.

Baadhi ya masuala ya kitamaduni yanayashughulikiwa katika tamthilia za *Mzalendo Kimathi* na *Nitaolewa Nikipenda* ni ndoa, dini, ushujaa, sheria, metafizikia, uzalishaji na umiliki wa mali miongoni mwa masuala mengine ya kitamaduni. Ni masuala haya ya kitamaduni ambayo yanaelezewa katika muktadha wa jamii ya tamthilia yanayoonyesha kupambanuliwa kwa utamaduni wa jamii husika. Upambanuzi huu wa tamaduni za jamii zilizotawaliwa kikoloni katika fasihi za baada–ukoloni hudhamiria kuonyesha jamii hizo

na utamaduni wake kama kitovu bainifu kilicho huru. Hivi utamaduni wa kikoloni uliodhamiria kuzifanya jamii na tamaduni za watawaliwa kuwa sehemu yake hugatuliwa. Afrika katika kugawanywa kwake na mataifa ya Ulaya ilikusudiwa kuwa sehemu ya mataifa haya hasa ikiangaliwa katika uhusiano wa siasa za ulimwengu (Thairu 1975: 16). Ilikuwa iwe mwendelezo wa mataifa hayo kijiografia na kitamaduni. Ni ubeberu wa aina hiyo ambao fasihi ya baada–ukoloni hupinga kupitia kuonyesha ubainifu wa tamaduni za watawaliwa.

Waandishi katika tamthilia hizi mbili wanaiangazia asasi ya ndoa. Katika *Nitaolewa Nikipenda* inaangaziwa katika pande za utamaduni wa watawaliwa na ule wa kikoloni. Utamaduni wa Kimagharibi unawakilishwa na tabaka la mabepari ambalo linaufuata. Kulingana na tabaka hilo ndoa kama asasi huthibitishwa na arusi ya Kikristo ambayo hufanyika kanisani. Ni arusi ya aina hiyo familia za Kioi na Ndugire zinapendekeza Kiguunda na Wangeci waifanye. Kulingana na Kioi, Ndugire, Jespheli na Helina vitu vinavyotakikana ni nguo za bibi na bwana arusi, ada ya kasisi na keki miongoni mwa mengine ambayo hawaonyeshi kuyaelewa. Mabepari hawa wanadai kuwa Kiguunda na Wangeci wanaishi katika ndoa haramu na yenye dhambi, na kwamba suluhisho ni kubatizwa na kufanya arusi ya kanisani.

Ingawa Kiguunda anapinga madai yao mwanzoni na kujitetea kuwa ndoa yao ilibarikiwa kwa kuwa alimtolea Wangeci mahari, anakubali baadaye kufanya arusi ya Kikristo. Gicaamba na Njooki, walio sauti ya urazini katika tamthilia ndio, wanaoonyesha uhalali

wa utaratibu wa ndoa wa kufuatia mila na desturi za jamii yao. Gicaamba analisisitiza hili kwa kuuliza suali la balagha:

Gicaamba: *Kuhitimisha mahari kimila siyo baraka halisi*
*Kutoka kwa watu wa nyumba yenu*
*Na watu wa nchi yote?*
*Sauti ya wananchi*
*Ndiyo sauti ya Mungu (uk. 63).*

Kiguunda na wangeci wanapopuuza uhalali wa ndoa kulingana na utamaduni wao na kufanya arusi ya kibepari kanisani mambo yanaanza kuwaendea tenge. Arusi hiyo ndiyo inayowaletea majuto mali yote yanapotwaliwa na shamba lao kuuzwa. Aidha, mwanao, Gathoni anapokataa kufuata taratibu za kitamaduni anazofaa kufuata kuhusu ndoa anaishia kujuta.

Tamthilia ya *Mzalendo Kimathi* nayo inaonyesha athari za ukoloni katika asasi ya ndoa. Msichana na Mvulana wanajipata wakizurura mitaani baada ya familia zao kusambaratishwa na ukoloni (uk 13). Nao wapiganaji wa Mau Mau wametenganishwa na jamii zao. Hali hii inaathiri ndoa zao. Kwa mfano, babake Kimathi aliuawa katika Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia na kwa hivyo Kimathi na nduguze wakaachwa wakiwa watoto chini ya malezi ya mama yao. Kupitia ndoa ya Gicaamba na Njooki koo za jamii yao zinatajwa. Kinachojitokeza ni kwamba katika ndoa za jamii yao watu waliooana walipaswa kutoka katika koo tofauti. Njooki alitoka katika ukoo wa Aagaciku naye Gicaamba akatoka katika ukoo wa Aambui. Kwa namna hii utamaduni wa jamii ya tamthilia una utaratibu changamano kuhusu ndoa na msomaji anaalikwa kujifahamisha nao.

Dini pia ni suala la kitamaduni lililoshughulikiwa. Dini huhusisha imani kuhusu mambo ya kiroho hasa uhusiano wa binadamu na Mungu. Dini ya Kikristo katika muktadha wa kikoloni inajitokeza kama chombo cha kikoloni. Inatumiwa kuwapumbaza watawaliwa ili mabepari wayafikie maslahi yao. Ni hali inayowaonyesha mabepari kama wanafiki wakubwa. Katika tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* ambapo Gicaamba anaeleza:

Gicaamba: *Wakati mabeberu wa Kiingereza walipokuja huku 1895*
*Mabwana wa dini zote*
*Walishika Biblia kwa mkono wa kushoto*
*Na bunduki kwa mkono wa kulia (uk. 57).*

Ukoloni ulileta mtapanyiko wa dini katika bara la Afrika ambazo ziliishia kuwakanganya watawaliwa. Badala ya dini kuwaelekeza watu kuishi maisha mazuri inawalevya wasijitambue. Kwa mfano, wafuasi wa Dini ya Dhiki wanachangisha pesa za kujenga kanisa ilhali wao hawana mashamba wala nguo. Hata hivyo, ni katika ubepari ambapo dini inatumiwa kuhalalisha unyonyaji. Kioi na mkewe wanamsifia dereva wa trekta ambaye ni Mkristo, hufanya kazi kwa bidii na hadai kuongezewa mshahara lakini ni katika utajiri wa Ndugire ambapo unafiki huu wa kidini unapojitokeza.

Ndugire: *Mungu ndiye vilevile aliyetuelekeza twende benki.*
*Tukapata mkopo wa kukistawisha (Kishamba chao).*
*Na fahamu sikutoa hata senti moja mfukoni (uk. 50).*

Tofauti inayojitokeza katika dini ya Kikristo na dini ya Kiafrika ni kuwa katika dini ya Kiafrika hakuna unafiki. Viapo vinavyofanywa katika dini hiyo havivunjwi kinyume na unafiki uliokithiri wa Kasisi katika *Mzalendo Kimathi* na Wakristo katika *Nitaolewa Nikipenda.* Tofauti kuu inatolewa na Kiguunda, *"Na makanisa hayo hutumiwa siku moja*

*tu"* (uk.17). Hii ni kinyume na dini za Kiafrika ambapo dini ni sehemu ya maisha ya kila siku. Hivyo, maisha yao na kila tukio huzungukwa na imani za kidini na hutafsiriwa kidini (Mbiti 1969:15). Hivyo, wao hawawezi kutenga siku ya kusali kwani kila siku huongozwa na imani za kidini. Dini za kigeni zilileta dhana ya kutenga siku ya kusali hali ambayo haieleweki katika dini za kimapokeo za Kiafrika. Tofauti hii ndiyo waandishi wa tamthilia hizi wanayobainisha kama njia ya kugatua utamaduni wa Kimagharibi.

Hata hivyo, uhalisia katika miktadha ya mwingiliano–tamaduni katika mchakato wa ukoloni lazima uzingatiwe. Hivi ukweli ni kwamba asasi za kitamaduni katika jamii za baada-ukoloni hazina umenyu tena. Dhana za athropologia ya tamaduni kama usilimisho au utamadunishaji *(cultural assimilation and acculturation)* ni potofu na haziwakilishi ukweli (Lionnet 1995:113-14). Mgusano wa tamaduni mbili unapotokea athari huhisika katika tamaduni zote. Hivyo, dini za Kiafrika zilipata athari kutoka kwa dini za kigeni, nazo za kigeni zikapata athari kutoka kwa dini za Kiafrika. Imani katika wahusika kama Kiguunda, Wangeci, Kioi, Jespheli, Ndugire na Helina miongoni mwa wafuasi wa Dini ya Dhiki katika tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* inaonyesha umahuluti huo. Nyimbo za kidini wanazoziimba ingawa zina ujumbe wa imani ya kigeni mtindo wake wa uwasilishaji ni wa Kiafrika. Aidha, wahusika wa Kiafrika wanaoingilia utamaduni wa kigeni wanawakilisha umahuluti wa aina hiyo.

Imani za kidini katika muktadha wa Kiafrika hueleza hali ya kuwepo au metafizikia. Metafizikia ya Kiafrika husisitiza uunganifu wa binadamu na maumbile. Dini ni tukio la kiontolojia na huhusisha suala la kuwepo. Binadamu huwa kitovu cha ontolojia hii;

wanyama, mimea, mazingira anakoishi na haja inapotokea yeye huunda uhusiano changamano navyo (khj 15-6).Kwa mfano, katika *Mzalendo Kimathi,* Kimathi anaeleza:

> Kimathi: .... *Tumefanya urafiki na ndege, nyoka na wanyama ambao hutuonya juu ya hatari ya adui (uk. 63).*

Katika muktadha wa Kiafrika ni jambo linaloeleweka. Aidha, kuna imani zinazomzunguka Kimathi zinazoonyesha metafizikia ya utamaduni wao. Kwa mfano, kwamba aliweza kuzungumza na Mungu au pia kwamba hangekufa na ni kivuli chake kilichokamatwa miongoni mwa imani nyingine. Kwa kuzingatia ukweli huu, utamaduni wa Waafrika ni changamano na asiyeuelewa atafanya upotoshi mkubwa kwa kuukatia shauri vivi hivi.

Kulingana na maisha ya kimapokeo ya jamii ya tamthilia watu waliishi katika maisha ya ujima na hali hii ilihakikisha usalama wa kila mmoja. Ukoloni na utamaduni wake ulivunjilia maisha haya na kuleta utamaduni uliosisitiza maisha ya mtu binafsi. Kwa kuangazia tamthilia ya *Mzalendo Kimathi,* wapiganaji wa Mau Mau wanatekeleza mapambano yao katika ushirikiano wa hali ya juu. Mwanamke anadhihirisha hili anapojishughulisha na kuwatumikia wapiganaji na hata kuwazindua vijana. Hata Kimathi, shujaa wa mapambano kila mara anasisitiza ushirikiano ili kumng'oa mkoloni.

Usaliti unaotokea unachochewa na tamaa ya maslahi ya mtu binafsi iliyochochewa na mkoloni. Kama anavyoeleza Henderson, wasaliti: Gati, Hungu, Gaceru na Wambararia walijisalimisha walipoahidiwa vyeo na mashamba (uk.31). Katika *Nitaolewa Nikipenda* warithi wa ukoloni kama Kioi, Ndugire na Ikuua wanaonyesha ubinafsi uliokithiri. Kioi

yuko tayari kumnyang'anya Kiguunda kishamba chake ili ajinufaishe yeye mwenyewe bila kujali wenye shamba wangeathirika vipi. Aidha, ubinafsi wa Kioi na mkewe unajitokeza wanapowanyima chakula Kiguunda na Wangeci wanapowatembelea. Kinyume na walivyoandaliwa chakula kilichowagharimu Kiguunda na mkewe pesa zote walizokuwa nazo, Kiguunda anapoomba maji, Kioi anamwelekeza mtumishi wake amchotee maji kutoka tangi la maji ya nguruwe.

Kipengele kingine cha utamaduni kinachoshughulikiwa ni sanaa. Waandishi katika tamthilia hizi mbili wanadhamiria kuibainisha sanaa ya Kiafrika hasa inavyojipambanua na sanaa ya Kimagharibi ili kuigatua. Sanaa katika muktadha wa Kiafrika ya kabla ya ukoloni ilikuwa ya kiuamilifu. Nyimbo, ngoma na muziki zilikuwa sehemu ya maisha ya Waafrika katika mapambano yao na mazingira. Hasa ngoma na nyimbo zilifungamana na shughuli mbalimbali kama, tohara, arusi, kazi, maombolezo, kuzaliwa kwa watoto miongoni mwa shughuli nyingine za kijamii. Hii ni kinyume na sanaa ya Kimagharibi ambayo msisitizo wake huwa katika kujieleza kwa hisi za mtu binafsi (Wa Thiong'o 1972:6-7, Soyinka 1976: 37-60). Sanaa ya Kiafrika ni lazima iwe ni kwa ajili ya jamii. Msanii ni mfanyakazi wa kijamii. Huu ni ubainifu wa fasihi ya Kiafrika vilevile.

Mintarafu hii katika tamthilia hizi mbili tunapata waandishi wakiyashughulikia maudhui yanayofungamana na maendeleo ya kijamii na siyo ya mtu binafsi. Katika *Mzalendo Kimathi* ukombozi wa jamii ndilo suala kuu. Aidha, wasaliti wanaoongozwa na maslahi yao ya Kibinafsi wanashitumiwa huku wanaojitoa mhanga kwa ajili ya jamii wakitukuzwa. Vilevile, nyimbo na ngoma zinazoonyesha ushirikiano wa kijamii

zinatumiwa. Ukwasi wa tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* unatokana na moyo huu wa maisha ya kiujima unaoonyeshwa na nyimbo na ngoma mbalimbali katika jamii husika. Nyimbo na ngoma hizi si shughuli ya mtu binafsi bali ni shughuli ya kijamii katika matukio mbalimbali. Ni katika hali hii ambapo utamaduni huleta jamii pamoja kwa kuwa husisitiza thamani sawa katika jamii husika.

Maisha haya ya ujima yanathaminiwa ambapo taasisi ya ushujaa inafasiriwa kutokana na mchango wa mtu kwa jamii yake kuliko kwake binafsi. Kimathi na wenzake waliopigania uhuru ndio tu jamii inawatambua kama mashujaa huku wasaliti wa juhudi za ukombozi wakidharauliwa. Kimathi analisisitiza hili katika *Mzalendo Kimathi* anapokataa kuhukumiwa kwa sheria za mahakama ya kibeberu. Sheria ambazo "*huwalinda wenye raslimali, tajiri, wanyonyaji walowezi*" (uk. 23). Aidha, katika sheria hii mgawo uwili unaopingana wa wenye urazini/wasio na urazini unavunjwa. Ikiwa mahakama ya kibeberu inamshtaki Kimathi kwa sheria inayoegemea upande mmoja, sheria katika kambi ya mashujaa katika msitu wa Nyandarua inatumia mantiki.

Askari wa Kwanza na wa Pili wa Kizungu wanatumiwa kupindua taswira potofu ya utamaduni wa uraziki wa Kimagharibi. Ingawa wametoka katika familia maskini hawako tayari kuhaini ukabaila wa Waingereza. Sheria ya kambi ya mashujaa inawahukumu kunyongwa kwa kutoupinga ukoloni – ambao umewaweka hata wao katika hali ya hatari. Mlowezi (Windhoek) pia anaonyesha hali hii. Utashi wa mali unamfanya awe kama kichaa anapohusisha uharibifu wa mali yake kuwa matokeo ya uchochezi wa Kimathi.

### 4.3.2 Lugha na Fasihi ya Baada-ukoloni

Katika fasihi ya baada-ukoloni, lugha hutumiwa kama mahali pa mvutano wa itikadi tawala na itikadi tawaliwa. Kwa namna hii basi lugha huwa taashira za tamaduni husika. Katika ugatuzi, lugha za kikoloni hupewa nafasi finyu na huvunjiwa usanifu wake ili itumikishwe kwa maslahi ya utamaduni wa watawaliwa. Katika tamthilia za *Mzalendo Kimathi* na *Nitaolewa Nikipenda* lugha ya kikoloni imepewa nafasi finyu. Hasa inawakilishwa na wahusika wa kikoloni kama Shaw Henderson, Johnnie, Askari wa Kiingereza, Mzungu, Windhoek (mlowezi), Delamere, Grogan, Mwanamke Mzee Mzungu, Afisa Mzungu, wageni kutoka Ujerumani, Amerika na Ujapani, pamoja na wahusika wa Kiafrika wanaowasaidia wakoloni (wasaliti) na mabepari weusi wa baada ya uhuru.

Katika fasihi ya baada-ukoloni pia lugha za watawaliwa hupendekezwa. Hii hudhamiriwa kuondoa lugha ya kikoloni iliyotumiwa kama chombo cha ukoloni. Lugha kama chombo kinachobeba thamani, kama zinavyoratibiwa na jamii husika katika kipindi fulani huweza kutilia msisitizo utamaduni wa watawaliwa. Kazi tunazozishughulikia ingawa ni tafsiri na baadhi ya nyenzo za lugha za ugatuzi hazijitokezi tunapata vidokezi vya jaribio la kuugatua utamaduni wa kikoloni.

Kwanza ni katika maneno na dhana za lugha ya jamii husika ambazo hazijatafsiriwa. Kwa mfano, katika *Mzalendo Kimathi*, wimbo wa Mwanamke (uk. 11) haujatafsiriwa. Wimbo huu unaonyesha uzalendo wa watawaliwa wa ukoloni. Aidha, Mwanamke anapotokezewa na Johnnie, askari wa kikoloni anatoa maneno ya mshangao kwa lugha yake (uk. 5). Dhana kama hizi zinahamisha msisitizo katika utamaduni wa watawaliwa ili

kuupa hadhi. Walinzi wa Kiafrika wanakariri maneno ya Kiingereza kikasuku, "*Liprightlipright…attention*!" (uk.56). Wanatumiwa kukashifu uigaji wa utamaduni wa kigeni badala yake wanafaa wajivunie utamaduni na lugha yao.

Vilevile, muundo wa lugha ya watawaliwa umetumiwa ili kuutambulisha. Kwa mfano, Mwanamke katika kumkanya Mvulana kumpiga Msichana anamwambia kuwa Msichana ni "*Binti ya mama yako*" (uk 12). Hapa waandishi wangeandika tu, "Ni dadako". Lakini hii haingeupambanua utamaduni wa jamii husika katika lugha yake. Hivyo, muundo huo unatumiwa kama taashira ya utamaduni wake.

Lugha ya Kiingereza inapotumiwa katika *Mzalendo Kimathi* ni katika kuleta dhana ya ubeberu. Kwa mfano, Mwamerika anayewapa kazi ya kubeba mizigo Msichana na Mvulana anaamrisha, "*here you take this boy. And your sister can take this, okey*... "*Take the baggage to that taxi over there. Understand*?" (uk.14). Kwa namna hii waandishi wanaionyesha lugha ya Kiingereza kama lugha ya kikoloni. Kwa namna lugha ya Kiingereza inavyotumiwa na Mwamerika inachukiza kutokana na ubeberu inaouwasilisha. Hii ni mbinu ya kupindua lugha hiyo kwa kuionyesha kwa namna hasi.

Katika *Nitaoelwa Nikipenda* ni mabepari Ndugire na Kioi, warithi wa ukoloni, wanaoitumia lugha ya mkoloni (uk.83, 85). Athari ya maneno ya Kiingereza wanayoyatumia ni kuonyesha unafiki uliofungamana na ukoloni uliotumia dini ya Kikristo.hasa Kioi anaposema, "*No more manna from Heaven* (uk. 85). Unafiki huo unajitokeza. Mali anayojivunia ni mirathi ya wizi. Hata babake, Kanoru alirithi mali ya

Mzungu aliyeitwa Kanoru na pia jina lake. Taashira ya urithi wa jina na shamba kutoka kwa Mzungu inawakilisha dhana pana ya utaratibu wa urithi wa ukoloni uliofanywa na tabaka ndogo la mabepari weusi.

Waandishi wa tamthilia hii wametumia majina ya tanzu za nyimbo za utamaduni wa watawaliwa. Ni majina yasiyoweza kupata visawe katika lugha ya kikoloni na yanaonyesha ubainifu wa utamaduni wake. Tanzu hizi za nyimbo ni kama: "*Mucung'wa*" (uk. 18), "*Nyangwecu*" (uk. 28), "*Gitiro*" (uk 42), "*Muumburo*" (uk. 66), "*Mugoiyo*" (Uk. 100), "*Mwomboko*" (uk. 102). Tanzu hizi haziwezi kueleweka bila kuutalii utamaduni husika na huu hasa ni mradi mmojawapo wa miradi ya fasihi ya baada-ukoloni. Kutalii huko kwa utamaduni wa watawaliwa ni kuuinua kihadhi.

Aidha, katika tamthilia hii waandishi wametumia methali na misemo ya lugha ya watawaliwa ili kuibainisha lugha yao. Busara inayobebwa na misemo na methali hizi ni namna ya kufasiri ulimwengu katika mkabala wa watawaliwa na ndizo hasa sauti za watawaliwa. Hivi utamaduni wa watawaliwa unatambuliwa katika mahali pake. Misemo na methali hizi kama sehemu ya fasihi ya watawaliwa inabeba falsafa yao ambayo ni changamano. Hali hii inaumbua dhana ya kikoloni kwamba akili ya mtawaliwa mweusi haiwezi kuelewa masuala changamano – hasa ya kisayansi ndiposa anajiingiza katika uchawi na ushirikina. Baadhi ya methali na misemo iliyotumiwa ni; kwa mfano,
"*Mpewa hajui akiba ikimalizika*" (uk. 25). Kiguunda anatumia methali hii kuonyesha kuwa hakuwa na pesa za chumvi alizohitaji mkewe. Yeye ndiye anayejua uwezo wake wa kifedha na kwa hivyo Wangeci anayemtegemea hawezi kuelewa mpaka aambiwe.

Mifano mingine ni:

i) *Hapana ajipambaye bila ya kujua atakavyoicheza ngoma (uk. 25)*

ii) *Mama wa warembo hana masikio (Uk. 27)*

iii) *Nyani akinyang'anywa mwanawe hutupiwa mumunye (uk. 37)*

iv) *Mazungumzo ni mapenzi (uk. 44)*

v) *Kukenuliwa meno si kupendwa (uk. 54)*

vi) *Mzazi hachukizwi na makamasi ya mwanawe (uk. 55)*

vii) *Hapana (mtoto) wa bepari au wa fukara. Uchungu wa kuzaa ni uleule (uk. 96)*

viii) *Mashuzi ya tajiri hayachukizi (uk. 98)*

Methali kama "Hapana (mtoto) wa bepari au wa fukara. Uchungu wa kuzaa ni ule ule" (Uk.96) anayoitumia Wangeci, inatumiwa kuukashifu utamaduni wa kikoloni. Utamaduni ambao unatumia vigezo vya uwezo wa kiuchumi kuwapa binadamu thamani tofauti tofauti. Methali hii inajiweka katika mtalaa wa upinduzi wa utamaduni wa kikoloni.

Misemo na methali hizi pia zinafumbata falsafa changamano ya utamaduni wa watawaliwa na zinafaulu kurekebisha upotoshi wa kikoloni kwamba utamaduni wa Kimagharibi ndio wenye uhodhi wa thamani zinazofaa kuigwa. Kwa kifupi lugha huwa msimbo ambao kwao jamii hufasiri ulimwengu wao, hufasiri jamii nyingine na huwapa uwezo wa kuyadhibiti mazingira yao.

**4.3.3 Fasihi Simulizi Katika Fasihi ya Baada-ukoloni**

Katika fasihi ya baada-ukoloni barani Afrika, imependekezwa kwamba fasihi ya watawaliwa iweke fasihi simulizi katika kitovu chake (Wa Thiong'o 1972:15-16). Hii ni kutokana na ukwasi wake wa thamani za kibunifu katika jamii husika. Tamaduni za

Kiafrika pamoja na kuwepo kwa teknolojia ya uandishi zimebaki vilevile katika hali yake ya kuwa tamaduni simulizi. Hata hivyo, cha muhimu zaidi ni kuwa fasihi hiyo huwa ni mali ya jamiii nzima na haihusihwi na mtu binafsi. Kwa hali hii dhima yake hulenga kuboresha maisha ya jamii husika. Hali hiyo ya ujima ni muhimu sana katika fasihi ya baada-ukoloni.

Kwa kulenga jamii za Kiafrika kabla ya ukoloni ni wazi kwamba jamii mbalimbali zilikuwa na mifumo yao tofauti ya kiutawala, kiuchumi na kijamii. Mifumo hii iliathiriwa na ukoloni ambapo mipaka ya jamii hizi ilivunjwa nazo zikalazimishwa kufuata mfumo mmoja wa nchi zilizoundwa na ukoloni. Kwa mfano, jamii kama za Wamaasai na Wameru zilikuwa na mifumo tofauti ya kiutawala, kiuchumi na kijamii. Lakini ukoloni ambao haukuheshimu tofauti hizo uliwalazimisha kufuata mifumo ya kigeni waliyoibuni walipounda nchi za kikoloni. Hali hiyo ya kuletwa pamoja na ukoloni ndiyo iliyoibua hali ya mwingiliano-tamaduni.

Fasihi ya baada-ukoloni hukumbatia ukweli huu wa umahuluti na huuona kama chachu ya kani za Kibunifu ambayo ni muhimu katika ujenzi wa jamii za baada-ukoloni. Hali hiyo huwa muhimu katika ujenzi wa utamaduni wa kitaifa. Moyo unaojengwa na fasihi simulizi basi ni muhimu sana katika kuleta ushirikina unaotakikana katika kujenga utamaduni huo wa kitaifa. Aidha fasihi simulizi huwa kihisihi *(sensibility)* cha haraka cha kuonyesha mabadiliko ya kitamaduni. Hivyo, fasihi andishi ya baada-ukoloni inayodhamiria kupata hisi za kimsingi za jamii ya baada-ukoloni haina budi kuchota

katika fasihi simulizi. Aidha, fasihi simulizi huakisi historia halisi ya jamii husika inayopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Waandishi katika tamthilia za *Mzalendo Kimathi* na *Nitaolewa Nikipenda* wametumia tanzu za fasihi simulizi iliyo fasihi asilia ya jamii yao. Kwa namna hii fasihi hii inawekwa sambamba na tamthilia iliyo ya utamaduni andishi ili kuugatua na kutilia msisitizo fasihi simulizi ya jamii ya watawaliwa. Utanzu wa wimbo ambao ni wa fasihi simulizi umetumiwa sana. Katika *Mzalendo Kimathi* nyimbo zimetumiwa kuhamasisha umoja katika kupambana na ukoloni. Kwa mfano, wimbo wa kwanza (uk. 1) unakariri umuhimu wa kupigania uhuru. Nao wimbo wa Mwanamke (uk.11) unasisitiza uzalendo kama hatua ya kwanza ya ukombozi. Mwishoni mwa tamthilia wimbo umetumiwa kuhamasisha wananchi kuupinga ukoloni.

Dhana ya usimulizi pia inatumiwa ambapo Mvulana anasimulia kuhusu maisha yao mjini kama watoto wa mitaani, na namna alivyowapoteza wazazi wake. Sehemu ya tamthilia baina ya ukurasa 13 hadi 17 inachukua umbo la hadithi simulizi. Hotuba za Kimathi pia ambazo ni sehemu ya utamaduni simulizi zinachukua nafasi kubwa. Hali hii inaumbua tamthilia kama utanzu wa fasihi ya Kimagharibi unaojengeka katika vitendo vya maigizo.

Tamthilia hii haiwezi kusimikwa katika fasiri ya tamthilia katika fahiwa ya tamthilia ya Kimagharibi. Ina sifa nyingi za fasihi simulizi ya watawaliwa wa kikoloni wanaoangaziwa.

Ni katika tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* ambapo kilele cha matumizi ya fasihi simulizi kinapofikiwa. Nyimbo, ngoma na usimulizi zinachukua sehemu kubwa katika tamthilia. Nyimbo na ngoma zinazojitokeza zinaoana na maudhui yanayojadiliwa na hivyo kuongezwa nguvu. Dhana hizi za fasihi simulizi zinautambulisha utamaduni unaojikita katika usimulizi unaopingana na uandishi ambao huutambulisha utamanduni Kimagharibi.

Utanzu wa fasihi simulizi wa nyimbo ndio unaotumiwa zaidi na unaakisi maisha ya ujima ya jamii husika. Nyimbo na ngoma hizo ni anuwai na kinachojitokeza ni utashi wa utanzu huu katika fasihi simulizi. Tanzu za nyimbo kama *"Mucung'wa" (uk. 18), "Nyangwecu" (uk. 28), "Gitiro" (uk 42), "Muumburo" (uk. 66), "Mugoiyo" (uk. 100) na "Mwomboko" (uk. 102)* zimeangaziwa huku uamilifu wa kila utanzu ukijitokeza. Utashi huu unapindua utashi wa fasihi ya Kimagharibi ambapo tanzu za orodha kuu yake zimekuwa zikiangaliwa kama tanzu za kiubia.

Uchanganuzi huu wa vijitanzu hivi vya utanzu wa wimbo unamwalika msomaji ili kujifahamisha kuhusiana na utamaduni wa jamii yake ili aweze kupata maana kamili katika tamthilia. Utanzu wa wimbo unajitokeza kama utanzu changamano katika jamii ya Gikuyu. Uchangamano huu haupo tu katika wingi wa vijitanzu vyake bali pia katika uamilifu tofautitofauti wa vijitanzu hivyo na pia ukweli kwamba huimbwa na makundi ya marika mbalimbali katika jamii hiyo. Huu ni ubainifu wazi wa utamaduni huu.Kwa mfano, *Gitiiro* ni ngoma na nyimbo za wanawake pekee (Kenyatta 1966: 294) ilhali *Mucung'wa*: ni ngoma na nyimbo za vijana (khj: 300).

Kumbukumbu za ndoa za kitamaduni za Kiguunda na Gicaamba zinaelezwa kupitia usimulizi huku nyimbo za kubebea kumbukumbu zikiimbwa. Aidha, hapa nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi zinajitokeza kama kiakisi cha historia ya jamii. Kwa mfano, wimbo wa *Mucungwa* anaouimba Kiguunda unamtaja shujaa Kimathi. Hivi, pamoja na uamilifu wa wimbo huo, unajumuisha mtalaa wa ugatuzi kwa kuwaangazia mashujaa waliopigana kuusitisha ukoloni. Simulizi kuhusu ndoa za Gicaamba na Kiguunda zinaipa tamthilia ladha ya fasihi simulizi huku zikitelekeza fasihi andishi (tamthilia) pembezoni. Historia inayobebwa na simulizi hizo ndiyo inayoakisi maisha ya watawaliwa na inayosimamia sauti zao. Aidha, Vansina (1985:27-32) ameiangalia fasihi simulizi kama historia za jamii ambazo zilijikita katika utamaduni simulizi.

Methali ni utanzu mwingine wa fasihi simulizi unaojitokeza katika tamthilia hii. Ufanisi wa tamthilia yenyewe unajikita katika kuwa kazi inayojumuisha harakati za pamoja za kijamii za maisha. Gumzo kati ya wahusika inaakisi maisha yao ya kila siku falsafa, yao kuhusu maisha miongoni mwa wengine. Methali huhitimisha busara inayotambuliwa kuwa ya kweli katika jamii. Aidha, katika jamii ya tamthilia wanaotumiwa methali wanaanza kwa kusema "Gikuyu alisema..." Urejelezi huu wa mtu anayehusishwa na kisaasili cha chimbuko la jamii hiyo unaipa methali husika mamlaka ya ukweli usioweza kupingwa. Hasa hii ndiyo nguvu ya usemi dhidi ya uandishi. Matumizi hayo ni sawa na tunayopata katika fasihi simulizi ya Kiswahili katika msemo kama "Wahenga walinena..." Hali hii humwezesha msemaji kuhalalisha anachokisema kwa kukihusisha na mamlaka yasiyoweza kupingwa.Ukweli huu unashadidiwa na nguvu za kiapo.

Anayekubali kusema maneno ya kiapo huamini kuwa akikiuka yaliyomo katika kiapo hicho atadhurika. Baadhi ya methali katika tamthilia ni:

Gicaamba: *Gikuyu alisema nyani akinyang'anywa mwanawe hutupiwa mumunye (uk. 37)*

Hapa Gicaamba anaeleza hali ya mfanyikazi kwamba ananyang'anywa nguvu zake kwa kudang'anywa kupitia kupitia kutupiwa ukofi wa pesa. Methali hii haielezi tu ukweli kuhusu ukoloni bali pia inaakisi mandhari ya utamaduni wa jamii ya mtumizi. Methali nyingine ni kana: "*Fisi hamli mwanawe*"(uk. 99). Gicaamba katika methali hii anawatolea nasaha Kiguunda na mkewe wasimwache mwanao kwa kuingilia umalaya. Methali nyiingine ni kama:

Kiguunda: *Mtambazi ukingoka humea mtini (uk 25)*
*Mama wa warembo hana masikio (uk* 27)

Aidha mifano ya methali katika tamthilia hizi ni mingi. Kwa kifupi, dhana za fasihi simulizi zinadhamiriwa kuugatua utamaduni wa Kimagharibi katika fasihi ili kuusisitiza utamaduni wa fasihi ya watawaliwa.

### 4.3.4 Uandishi Tena wa Historia Katika Fasihi ya Baada-ukoloni

Uandishi tena wa historia ya watawaliwa kutoka kwa mkabala wao ni mradi mmojawapo wa miradi ya fasihi ya baada-ukoloni. Uandishi huu hudhamiria kutupilia mbali historia iliyoandikwa na wakoloni isiyowakilisha hali halisi ya watawaliwa. Historia hiyo yenye

taswira dufu huendeleza mtazamo fulani wowote katika muktadha wa kikoloni. Aidha, waandishi wa tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* wanaeleza katika utangulizi:

> *Zamani, kabla hati ya Kirumi kuingia hapa Kenya, historia yetu -methali, hadithi, vitendawili, mashairi, ngoma na nyimbo- yote hayo yalifundishwa kwa mazungumzo, kizazi kikipokea kutoka kwa kizazi kingine kwa hivyo wazungu na hao wageni sio walioanzisha historia katika nchi yetu (uk. 6)*

Mintarafu hii tamthilia hii inadhamiria kuwakilisha historia ya jamii ya waandishi kutoka kwa mkabala wa jamii yao. Hali hii inaiweka tamthilia hii katika kitovu cha usomi wa fasihi ya baada-ukoloni. Nao waandishi wa *Mzalendo Kimathi* wana lengo lisilo tofauti na hilo:

> *Wanahistoria wetu na waandishi wetu wamekuwa na kazi nyingi wakihariri maandishi ya wakoloni yanayosema eti watu wetu hawakuwa na la kufanya ila kuzurura hapa na pale wakipambana wao kwa wao na kwamba waliweza kufurahia utawala wa Mwingereza! (Utangulizi).*

Hivyo, tamthilia hii inakosoa upotoshi uliofanywa na wasomi wa Kimagharibi na wenzao watawaliwa waliopata elimu ya kikoloni. Madai ya waandishi hawa in kuwa watawaliwa kama Kimathi, Mwanamke, Ole Kisio, Matenjagwo, Njama miongoni mwa wengine ndio wajenzi wa historia ya jamii yao. Walichangia katika kumuondoa ubeberu. Aidha, riwaya hii kama waandishi wake wanavyoeleza katika Utangulizi lengo lake ni kukosoa vitabu vya historia vilivyoandikwa na wakoloni kama: Henderson: *The Hunt for Dedan*, Huxley: *A Thing to Love* na Ruark: *Uhuru and Something of Value*.

Tamthilia hii, ingawa inalenga zaidi katika mashtaka anayofanyiwa Kimathi, kupitia mbinu rejeshi matukio ya kihistoria yanaigizwa. Kwa mfano, kuhusu biashara ya Utumwa na vita vya Mau Mau. Katika kuunda utamanduni wa kitaifa mashujaa wa jamii nyingine wanatajwa: kwa mfano, Waiyaki, Me katilili, Mbatiani, Koitalel. Aidha, usaliti unakashifiwa na wasaliti kama: Mumias, Wango'mbe, Karuri Gakure, Luka Kinyanjui (uk. 63). Miongoni mwa wengine wanatajwa. Hii ni njia ya kuitalii historia ya watawaliwa tena.Kimathi hakuwa mpigania haki ya kupata ardhi ya jamii yake tu bali pia na utamaduni. Anaeleza:

Kimathi: *(Watu wetu) Walikuwa wakicheza ngoma hizi kabla ya mkoloni kuingia nchini. Walicheza wakati wa tohara, matanga, arusi halafu mara mkoloni alipoingia, watu wetu wakaanza kuigiza michezo yao (uk. 34).*

Tamthilia hii pia inaiumbua historia iliyofumbia macho mchango wa wanawake katika ukombozi. Mwanamke anasawiriwa akishughulika katika harakati za ukombozi. Hali inapokuwa ngumu anajibadilisha kwa kuvalia nguo za mwanamume. Aidha, anawazindua vijana ili kushiriki katika mapambano. Tamthilia hii inasawazisha historia kwa kuangazia pande zake zote. Waandishi hawasiti kueleza kuwa machifu Waafrika walishirikki katika biashara ya watumwa kwa kuwauza Waafrika kwa bei ya nguo na shanga. Wanaikashifu historia hiyo ya usaliti kwa kuonyesha madhara yake.

Katika tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* historia ya watawaliwa inaonyesha kupitia mazungumzo ya wahusika kutoka kabla ya Hali ya Hatari, vita vya uhuru na baada ya uhuru. Kumbukizi za ndoa za Gicaamba na Kiguunda zinafungamana na matukio ya kihistoria. Hata hivyo, ni usaliti wa baada ya uhuru unaoangaziwa zaidi. Warithi wa

nafasi za wakoloni: Ikuuwa, Ndugire na Kioi wanauendeleza ukoloni. Wako tayari kuwarejesha wakoloni kwa hila za uwekaji wa wageni. Historia ya usaliti inaonyeshwa kutoka kwa babake Kioi, Kanoru aliyerithi shamba la Mzungu aliyeitwa Kanoru na kisha Kioi akaliridhi. Utaratibu huo hauelekei kuisha kwani mwanawe Kioi, John Muhuni yu tayari kuendeleza mienendo ya babake. Kiguunda ametumikia aina hizo mbili za ukoloni. Na haelekei kuonyesha dalili za kujinasua na mtando huo na unyonyaji.

Gicaamba ndiye aneyejibainisha kama mfanyikazi aliyezinduka. Ndiye anayeirudisha mahali pake hati ya ardhi baada ya kuangushwa na akina Kioi wanapopita. Aidha, anaelekea kuelewa uhusiano wa kimatabaka katika jamii yao. Gicaamba na Kiguunda walishiriki katika vita vya uhuru na ni kinaya kwamba ndio wahasiriwa wa ukoloni mambo-leo wa mabeberu weusi. Historia hii ya usaliti ndiyo waandishi wanayodhamiria kuiwakilisha. Aidha, dini ya Kikristo imetumiwa katika kuufanikisha ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba waliopata elimu ya kikoloni walipaswa pia kujifunza dini hiyo huku wakitupilia mbali dini zao za kimapokeo na utamanduni.

Hivyo, historia inayowakilishwa na waandishi wa tamthilia hizi ni tofauti na historia ya mkabala wa kikoloni iliyoeleza kuwa ukoloni na shughuli za wamishenari zililenga kustaarabisha bara la giza la Afrika.

### 4.3.5 Mandhari na Uhusika Katika Fasihi ya Baada-ukoloni

Mandhari na uhusika ni dhana zinazojitokeza kama mikakati ya ugatuzi katika tamthilia hizi. Wahusika wanaoakisi hali ya watawaliwa wa kikoloni wamesamiriwa katika mandhari ya tamaduni zao. Mandhari katika fasihi ya baada-ukoloni huwa ni suala kuu. Mtafaruku wa utambulisho wa wahusika kwa njia moja, huangaziwa katika kuondolewa katika mandhari yao ya asili. Kwa kuzingatia hili ni wazi kwamba mandhari ni muhimu katika utambulisho. Mintarafu hii, Kiguunda anapopoteza shamba lake kupitia kwa Kioi, si kiuchumi tu anapopoteza bali pia sehemu ya utambulisho wake pamoja na ule wa familia yake. Hapa basi kinachojitokeza ni uhusiano wa kimsingi wa nafsi na mahali. Hivyo, si sadfa katika tamthilia zinazoshughulikiwa kuangazia kwa utondoti wahusika katika uhusiano huo.

Wahusika hawa wanapambana na mazingira yao katika kujaribu kuwa na maisha yenye wiano. Vilevile, mandhari yanayoshughulikiwa yanawahusu wahusika hao, watawaliwa wa kikoloni. Lugha wanayoitumia inaonyesha ukweli huu. Kwa mfano, Njooki anapowapiga vijembe Kiguunda na mkewe:

Njooki: *Kwani hawa ni wageni wa aina gani tusiotakiwa tuwajue? Huenda ikawa ni Wazungu kutoka Ulaya? Na kila mtu anajua vizuri Mzungu hajali hali za watu? (uk.36).*

Anadhirihisha urazini wa watawaliwa kuhusu Mkoloni ambaye ana utamaduni tofauti na wao. Utamaduni wa jamii hii unasisitiza ushirikiano na kujuliana hali ili kuhakikisha mwanajamii haumii bila kusaidiwa. Haya ni maisha ya ujima. Maisha haya ni tofauti na ya Kiulaya ambapo maslahi ya mtu binafsi (utamaduni wa kibinafsi) hutiliwa mkazo.

Waandishi wanashughulikia athari za ukoloni katika jamii za Kiafrika. Dhana kama: unafiki wa kidini, matabaka, uozo wa kimaadili, unyonyaji ni dhana zilizoletwa na ukoloni katika jamii ya watawaliwa. Wahusika wanaonyeshwa wakikabiliana nazo. Kwa kutumia nyenzo za mandhari yao. Gicaamba anaeleza:

Gicaamba: *Natushirikiane kwa mapenzi*
*Gikuyu alisema,*
*Nyegere wawili hawashindwi na mzinga wa nyuki*
*Utaalamu wa mtu mmoja hautoshi*
*Kigingi kimoja hakiwezi kuwamba ngozi*
*Gogo moja haliwezi kuukeshesha moto ukiwaka*
*Kidole kimoja hakivunji chawa,*
*umoja ni nguvu utengano ni udhaifu (uk. 108).*

Mhusika huyu aliye sauti ya urazini katika tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* anafanya urejelezi wa kisasili cha jamii yale ili kupata mamlaka yasiyopingika kuhusu suluhisho la matatizo yao lenye asili ya mapokeo yao. Ujima unaoashiriwa na fasihi simulizi ni taashira ya mambo ya kimapokeo yaliyo na thamani za kuiwezesha jamii kuikabili hali iliyopo na ijayo.

Hali hii inapinga mawazo ya Mkurugenzi katika *Mzalendo Kimathi* anayesherehekea ushindi wa Waafrika, tabaka la mabepari ambao baada ya uhuru waliweza kufanya na kumiliki vilivyokatazwa na wakoloni katika kipindi cha ukoloni. Mkurungezi ambaye ni mmoja wa waliorithi nafasi za Mkoloni anajali maendeleo ya kundi hilo ndogo huku walio wengi wakiendelea kuwa katika hali waliyokuwepo kabla ya uhuru.

Wahusika katika tamthilia hizi mbili wanagawika katika makundi mawili: waosimamia upande wa watawaliwa na waathirika wa ukoloni pamoja na wanaosimamia upande wa ukoloni. Wazungu pamoja na tabaka la mabepari weusi wanawekwa katika upande mmoja. Hapa hata wasaliti wa juhudi za watawaliwa za kujikomboa wanajumuishwa. Mkao wa watu mahakamani unaonyesha mgawo huo katika *Mzalendo Kimathi*. Katika tamthilia hizi mbili msimamo wa waandishi ni kuwa hakuna msimamo wa kati- ama unaunga mkono mapambano ya watawaliwa au unapinga.

Hata hivyo, panatokea hali ya usebusebu katika wahusika ambapo kwa hakika ni vigumu kusimika baadhi ya wahusika katika makundi hayo mawili. Ni dhahiri kwamba wahusika kama Mkurungenzi, Kioi, Ndugire, Ikuua, Muhuni wanakalia pande zote mbili. Kwanza, wao ni wakoloni. Hali hi inaumbua uwakilishaji wa kikoloni uliowaona na kuwarejelea watawaliwa kama kundi moja ambalo halikuwa na mgawanyiko. Hii ilikuwa mbinu ya kurahisisha utawala wao hasa katika mchakato wa kuunda taswira potofu kuwahusu watawaliwa.

Waandishi wametumia majina ya wahusika yaliyojikita katika utamaduni wa watawaliwa katika ugatuzi. Ni majina yaliyo na maana katika mandhari ya utamanduni huo. Kwa mfano, katika *Mzalendo Kimathi* majina wanayopewa wasaliti ni ya kitashtiti. Majina kama Gati, "mtu asiye na thamani", Hungu, "mwewe", Gakunia, "kijigunia" (Gatotia), Waitina ni majina ya kushusha hadhi – hali inayoendana na vitendo vyao na hamna wanavyochukuliwa katika jamii. Majina haya yanaonyesha vizuri namna ambavyo usemi

katika lugha ya watawaliwa huitikia ukoloni. Kwa mfano, Waitina ambaye Askari Mzungu anapewa jina linalomaanisha, "aliye wa sehemu ya makalio" (asiye na thamani). Kwa hakika ni matusi na hii inajitokeza kama namna ya utamaduni wa watawaliwa wa kuupindua ukoloni. Vilevile, Gati linaonyesha dhana hiyo ya kudharau. Hungu lina maana ya mwewe, anayenyakua vifaranga- iliyo tabia ya ukoloni na Gakunia (Gatotia) pia linawakilisha hali hiyo ya kudharau, linamaanisha "Kijigunia".

Vilevile, majina ya wahusika katika *Nitaolewa Nikipenda* yanafungamana na maana ya majina hayo katika utamaduni husika. Kioi, "anayenyakua", Kiguunda, "Shamba kubwa", Gicaamba "Shujaa mkubwa," Jespheli *(Jezebel)* "Mwanamke asiye na maadili" (Mkewe Ahabu katika Biblia, Agano la kale). Maana ya majina ya wahusika hawa kujikita katika utamaduni wa jamii ya tamthilia ni kuuelekezea utamaduni huo msisitizo.

Aidha, katika tamthilia ya *Mzalendo Kimathi*, majina ya Kizungu yanatumika kama taashira ya utamaduni wa kikoloni. Majina kama Henderson, Windhoek na Johnnie yanaoonyesha kutokuwa sehemu ya utamaduni (kuwa mageni) unaotiliwa msisitizo. Vitendo vyao vya kuchukiza ndivyo vinavyowatambulisha kuliko majina yao yasiyo na maana katika utamaduni wa watawaliwa.

### 4.4 Hitimisho

Katika dhana zote tulizozijadili katika sura hii ni dhana zinazopendekeza kuangaziwa kwa utamaduni wa watawaliwa. Hivi msomaji anaongozwa katika welewa wa utamaduni husika ili kutambua thamani zake na ubainifu wake. Utamaduni huu hivyo ni kitovu cha

aina yake katika tamthilia hizi. Hapa ukoloni unasukumizwa pembezoni na wahusika wanaouegemea wanasawiriwa kwa njia ya kuchukiza na hasi. Kwa mfano, wahusika watawaliwa wa kikoloni wanapewa nafasi ya kusikiwa. Wanamfasiri mkoloni kutoka kwa mkabala wao hali inayopindua utamaduni wa kikoloni uliomfasiri mtawaliwa kutoka mkabala wa Kimagharibi.

Uandishi wa tamthilia za baadaye unaonyesha kukua kwa urazini wa kiitikadi katika ubaada-ukoloni ikilinganishwa na ilivyo katika tamthilia za awali. Aidha, kukua huku pamoja na kuonyesha maendeleo ya mwandishi huyu, kunaweza kuwa kumechangiwa kwa kiasi fulani na waandishi alioshirikiana nao.

# SURA YA TANO

# 5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Kazi hii imeangazia ugatuzi wa utamaduni wa kikoloni katika tamthilia za Ngugi wa Thiong'o. Aidha, tamthilia alizoziandika kwa kushirikiana na waandishi wengine kama *Nitaolewa Nikipenda* na *Mzalendo Kimathi* zimeshughulikiwa. Usomaji wa tamthilia hizi umejikita katika mtalaa wa fasihi ya baada-ukoloni. Wazo linalojitokeza katika usomaji wa aina hii ni msimamo wa mwandishi/waandishi katika kuumbua utamaduni wa kikoloni katika jitihada za kubuni utamaduni wa kitaifa.

## 5.2 Mjadala na Maoni

Kwa kulinganisha kazi za awali, (*Mtawa Mweusi* na *Kesho Wakati Kama Huu*) alizoziandika Ngugi na tamthilia za baadaye (*Mzalendo Kimathi* na *Nitaolewa Nikipenda*) alizoziandika akishirikiana na Micere Mugo na Ngugi wa Mirii mtawalia, tunagundua kukua kwa urazini wa ubaada-ukoloni. Kwanza, kwa kuangazia matumizi ya fasihi simulizi tunapata kwamba katika *Mtawa Mweusi* na michezo iliyoko katika mkusanyiko wa *Kesho Wakati Kama Huu*, fasihi simulizi imetumiwa kwa ufinyu sana. Hali hii ni kinyume na ilivyo katika *Mzalendo Kimathi* na *Nitaolewa Nikipenda*. Katika tamthilia hizi za baadaye nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi zinazowasilishwa katika hali ya ujima zinachukua nafasi kubwa.

Aidha, utamaduni wa watawaliwa unaangaziwa kwa upana zaidi katika tamthilia za baaadaye. Uandishi tena wa historia ya watawaliwa unafanywa kwa njia ya kina huku

matukio mahsusi yakirejelewa. Wahusika wanaowakilisha jamii ya watawaliwa wanashirikishwa zaidi na hili linasaidia uwakilishaji wa sauti zao. Ikiwa uandishi wa tamthilia ya *Mtawa Mweusi* unajitokeza kama mwanzo wa uandishi wa Ngugi wa tamthilia ambapo mhusika mkuu, Remi anaonekana kupachikiwa maneno anayopaswa kuyasema, *Nitaolewa Nikipenda* na *Mzalendo Kimathi* ndio kilele cha uandishi wake ambapo wahusika wakuu Kiguunda na Kimathi wanakuzwa katika mandhari ya utamaduni wao na maneno wanayoyatamka yanajitokeza kuwa yao wenyewe.

Dhana za uumbuaji pia zimetumiwa, hasa katika kubainisha migawo uwili inayopingana. Lengo hapa ni kufuta mipaka hiyo ili kuonyesha kuwa haikujengeka katika "mantiki" ya kikweli bali ilitumikia maslahi ya kikoloni. Hasa upinduzi wa migawo ya aina hiyo ni sehemu ya mradi wa ugatuzi. Uekuaji wa sehemu ya mgawo iliyochukuliwa kuwa ya hadhi ya juu hulenga kuangazia sehemu ya mgawo uliopuuzwa. Migawo uwili hapa inaainishwa katika kufuatia mgawo mkuu wa Kiulaya/Kiafrika, (mtawala kikoloni/mtawaliwa).

Mikakati ya ugatuzi ambayo imejitokeza katika tamthilia zilizoshughulikiwa ni maelezo ya kiethnografia, lugha, fasihi simulizi uandishi tena wa historia, uhusika na mandhari. Kinachojitokeza hapa ni tamthilia hizi kuwa mtalaa wa utamaduni wa watawaliwa. Utamaduni wa kikoloni katika tamthilia unatekelezwa katika nafasi ya pembezoni. Uhakiki katika utafiti huu unakubaliana na nadharia tete zilizouelekeza.

Kwanza, tamthilia hizi zinajitokeza kuwa harakati za ugatuzi wa utamaduni wa kikoloni. Jambo hili linadhihirishwa na upana ambao utamaduni wa watawaliwa unashughulikiwa na ufinyu katika upande wa utamaduni wa kikoloni. Hata hivyo, ukweli kwamba utamaduni wa watawaliwa si mkamilifu na una mapungufu yake umezingatiwa. Kwa hakika, tamthilia zinaalika maingiliano huru ya tamaduni husika ili zote zifaidi kutokana na maingiliano hayo. Nadharia ya baada-ukoloni hukumbatia umahuluti katika jamii za baada-ukoloni kama kani ya ubunifu inayoweza kuleta mabadiliko chanya. Umahuluti katika mtalaa wa fasihi ya baada-ukoloni huhakiki ubeberu wa kitamaduni na huangazia athari za kuchanganyika kwa utambulisho na utamaduni. Hali ya umahuluti na ungitamaduni zina uwezo wa kuondoa mchakato wa utawala wa kibeberu katika utamaduni kupitia kufasili tena na kupindua mitalaa iliyopokezwa watawaliwa kupitia ukoloni. Hivyo, dhana hizi huangazia tena kihakiki nafasi inayotokea katika mipaka ya tofauti wakati tamaduni tofauti hukutana (Bhabha 1994:181).

Mawazo ya Bhabha yanasherehekea ungitamaduni na uwezo wa upinduzi wa umahuluti. Muundo wa kitamaduni wa umahuluti katika ukoloni ulizua usebusebu katika mtalaa wa kikoloni na hivyo kutoa nafasi kwa watawaliwa (waliokuwa si watawaliwa kamili na si wakoloni kamili) kupindua mamlaka ya mkoloni. Hii ni kushadidia ukweli kwamba utamaduni wa kikoloni unazo chembe za manufaa katika utamaduni wa watawaliwa. Mathalan, wandishi katika tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* hawakashifu namna mpya ya uzalishaji mali wa kigeni. Hivyo, ikiwa uzalishaji mali huo utawanufaisha watawaliwa walio wengi badala ya tabaka ndogo la warithi wa ukoloni basi utwaaliwe ili ujenge utamaduni wa watawaliwa.

Aidha, katika *Waasi* na *Mtawa Mweusi*, mwandishi hapingi ndoa zitakazohusisha tamaduni tofauti bali anapinga ufinyu wa kimawazo ambao wahusika kama Nguru na Remi wanao kuhusiana na ndoa hizo.

Pili, tamthilia zilizoshughulikiwa zinaakisi uandishi wa fasihi ya baada-ukoloni. Hii inatokana na masuala anuwai yanayoshughulikiwa ambayo ni kiini cha fasihi ya baada-ukoloni. Baadhi ya masuala hayo ni: uandishi tena wa historia ya watawaliwa, fasihi (simulizi) ya jamii zilizotawaliwa kikoloni, lugha, ukengeushi katika utambulisho na ubeberu wa kiutamaduni (Ashcroft na wengine 2002: 4-11). Hata hivyo, kazi zilizoshughulikiwa kutokana na kuwa ni tafsiri, ugatuzi unaojikita katika lugha yenyewe unaeleka kutojitokeza. Lakini pamoja na hili suala la kiitikadi kuhusu lugha katika fasihi ya baada-ukoloni linajitokeza vizuri. Lugha ya kikoloni katika tamthilia zilizoshughulikiwa inapewa nafasi finyu na mtazamo hasi. Mathalan, katika *Mzalendo Kimathi* ubeberu wa utamaduni wa kikoloni unafumbatwa na lugha ya mtalii Mwamerika anayetumia lugha hiyo na namna anavyoitumia.

**5.3 Mapendekezo ya Utafiti**

Utafiti huu unapendekeza kufanywa kwa utafiti ambao unaweza kuangazia na kubainisha athari za kutafsiri katika kazi za kifasihi za baada-ukoloni kutoka lugha ya kikoloni hadi lugha ya watawaliwa wa kikoloni. Kwa hakika hili lipo nje ya upeo wa utafiti huu. Hii inatokana na ukweli kwamba nadharia ya baada-ukoloni huangazia matumizi ya lugha kiitikadi na wala sio matumizi ya lugha kimatini.

Pengo linalojitokeza katika tamthilia hizi ni uchukulio sahili kwamba utamaduni wa watawaliwa ni kama "mtoto mchanga" anayefaa kulindwa asidhuriwe na tamaduni nyingine zenye nguvu. Ingawa tamthilia hizi zinapendekeza mwingiliano na uhusiano huru wa tamaduni zinazogusana, hazionyeshi kutambua kuwa tamaduni mbalimbali huwa na namna ya kuitikia mgusano wake na tamaduni geni. Fasihi simulizi ya utamaduni ulioingiliwa huakisi uitikio huo. Katika sura ya pili kitendawili kama, "Mzungu anachungulia dirishani" ambacho huwa na jawabu "Kamasi" kilifafanuliwa. Kitendawili hiki kinaonyesha uitikio wa utamaduni wa watawaliwa kwa utamaduni wa kikoloni. Hasa kinauekua na kuupindua utamaduni huo. Aidha, mifano ni mingi katika tamaduni za watawaliwa katika tanzu zake za fasihi simulizi.

Kinachopingwa hapa ni upinzani finyu wa utamaduni wa kikoloni. Utamaduni huo uliharakisha taratibu ambazo hazingegunduliwa pasipo ukoloni katika jamii za watawaliwa. Kwa mfano, kuletwa pamoja kwa jamii za Kiafrika. Muungano wa jamii za Kiafrika ulikuwa ushaanza hata kabla ya majilio ya ukoloni lakini ulikuwa unatokea polepole. Kwa mfano, kupitia shughuli kama ndoa na biashara zilizohusisha makabila tofauti. Hivyo, ukoloni uliharakisha utaratibu huo kupitia kuunda na kuyagawa mataifa mbalimbali. Ubaada-ukoloni husherehekea umahuluti ulioletwa na ukoloni. Umahuluti huu ni kani ya mabadiliko (chanya na hasi) na maendeleo ya jamii za baada-ukoloni.

# MAREJELEO


Amin Samir (1988*) Eurocentrism.* New York: Zed Books.

Ani Marimba (1996) "The African Asili". In Ladner, J.A. and Gbadegesin, S. (eds) (1996*) Ethics, Higher Education and Social Responsibility.* Washington D.C.: Howard University Press.

Ashcroft. B., Gareth, G. and Helen, T. (2002) *The Empire Writes Back: Theory and Practice in Post-colonial Literatures.* 2nd edn. London/New York: Routledge.

Barry, P. (2002) *Beginning Theory; An Introduction to Literary and Cultural Theory.* Manchester: Manchester University Press.

Bhabha, H.K. (1983) "The Other Question." In Mongia, P. (ed) (1996) *Contemporary Post-colonial Theory; A Reader.* London: Arnold.

……… (1994) *The Location of Culture.* http://www.en.wikipedia.org/wiki/hybridity

Chacha, C.N. (1986) *Marejeo.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Chimerah, R. (1998) *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons.* Nairobi: Nairobi University Press.

Chinweizu, Jemie, O. na Madubuike, K. (1980) *Towards the Decolonization of African Literature; African Fiction and Poetry and Their Critics.* London: KPI.

Conrad, J. (1972*) Kiini cha Giza* .Mtafsiri. Kisanji, W. T. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

Conrad, J. (2005) *The Heart of Darkness.* Delhi: Surjeet Publications.

Cook, D. na Okenimkpe, M. (1997) *Ngugi wa Thiong'o; An Exploration of his Writings.* 2nd edn. Oxford: Oxford University Press.

Denham, R.D. (1978) "Introduction." In Frye N. (1978) *Northrop Frye: On Culture and Literature; A Collection of Review Essays*. Chicago/ London: The University of Chicago Press.

Derrida, J. (1966) "Structure, Sign and Play in the Discourse of the Human Sciences." In Lodge, D. and Wood, N. (eds.) (1988) *Modern Criticism and Theory; A Reader*. 2nd edn. Delhi: Pearson Education.

Fanon, F. (1963) *The Wretched of the Earth; The Classic of Third World Politics*. Harmondsworth: Penguin Books limited.

......... (1964) *Toward the African Revolution; Political Essays*. New York: Grove Press.

......... (1967) *Black Skin, White Masks*. New York: Grove press.

Gibbe, A. G. (1978) "Fasihi na Jamii: Baadhi ya Washairi wa Kiswahili 1960-1977." *Kiswahili .toleo 48/1. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.*uk 1-25.

Gitahi, G. (1980) "The Development of a Writer's Social Perspective: An Assessment of Ngugi wa Thiong'o's Selected Texts". M.A. Thesis (Unpub.) University of Nairobi.

Githae, M.M. (1978) *Visions of Africa; The Fiction of Chinua Achebe, Margaret Laurence, Elspeth Huxley and Ngugi wa Thiong'o*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Gromova, N.V. (2004) *Tafsiri Mpya za Fasihi ya Kirusi Katika Kiswahili.* http://www.ifeas.unimainz.dw/ suafo/ sf// Gromova.pdf.

Hardy, T. (1998) *Tess of d'ubervilles*. Boston/New York: Bedford Books.

Hussein, E.N. (1971) *Mashetani*. Dar es Salaam. Oxford University Press.

Irele, A. (1981) *The African Experience in Literature and Ideology*. London: Heinemann.

……… (2002) "Francophone African Philosophy". In Coetzee, P.H. and Roux, A.P. J. (eds) (2002*) Philosophy from African*. 2nd edn. Oxford: Oxford University Press.

July, R. W. (1987) *An African Voice: The Role of Humanities in African Independence*. Durham: Duke University Press.

Karanja, P.N. (1990) "Tamthilia za Kiukombozi: Taswira za Mwafrika Katika Vita vya Ukombozi Dhidi ya Ukoloni". Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Kenyatta, J. (1996) *Naushangilia Mlima wa Kenya*. Mtafsiri. Kibui, L. Nairobi: East African Publishing House.

Killam, G.D. (1984) "Ngugi wa Thiong'o". In Killam, G.D. (ed.) (1984) *The Writing of East and Central Africa: The Countries, The Writers, The Genres*. Nairobi: Heinemann.

Lionnet, F. (1995) "Logiques Metisses: Cultural Appropriation and Postcolonial Representations." In Myriades, K. and Mcguire, J. (eds) (1995) *Order and Partialities: Theory, Pedagogy and the Postcolonial*. New York: State University of New York Press.

Lo, Jacqueline (1999) "Return of the "Native" in K.S. Manian's The Cord." In Gilbert, H. (ed) (1999) *(Post)colonial Stages; Critical and Creative Views on Drama, Theatre and Performance*. West Yorkshire: Dangaroo Press.

Loomba, A. (1998) *Colonialism/Postcolonialism*. London/New York: Routledge.

Lo Liyong, T. (1969) *The Last Word; Cultural Synthesism*. Nairobi: East African Publishing House.

....... (1991) *Culture is Rutan.* Nairobi: Longmann.

Lyre, J. (1997) *Some Issues in Postcolonial Theory.* http://www.brocku.ca/english/courses/4F70/postcol.html

Mazrui, A. A. (1990) *Cultural Forces in World Politics.* London: James Currey.

Mbatia, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbiti, J. S. (1969) *African Religions and Philosophy.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugai, K. (2000) "Images of Dedan Kimathi in Kenyan Creative Literature". M.A. Thesis (Unpub.). University of Nairobi.

Mulokozi, M.M. (2000) "Language, Literature and Forging of a Pan-African Identity." *Kiswahili Juzuu 63/1. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.* pp. 71-78.

Munday, J. (2001) *Introducing Translation Studies: Theories and Application.* London: Routledge.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkosi, L. (1981) *Tasks and Masks: Themes and Style of African Literature.* Harlow: Longman Group.

Osabutey-Aguedze, I. D. (1990) *The Principles Underlying the African Religion and Philosophy.* Nairobi. Maillu Publishing House.

p'Bitek, O. (1986) *Artist the Ruler; Essays on Art, Culture and Values.* Nairobi: East African Publishing House.

Rorty, R. (1995) "Deconstruction". In Selden, R. (ed.) (1995) *The Cambridge History of* Literary Criticism: From Formalism to Poststructuralism. Vol.8. Cambridge: Cambridge University Press.

Rutherford, A. (1992) "Introduction: The Essential Heterogeneity of Being." In Rutherford, A. (ed) (1992) *From Commonwealth to Post-Colonial.* Sydney: Dangaroo Press.

Said, E. (1978) "Orientalism." In Mongia, P. (ed) (1996) *Contemporary Postcolonial Theory; A Reader.* London: Anorld.

Smith, A. (1989) *East African Writing in English.* London: Macmillan.

Soyinka, W. (1976) *Myth, Literature and the African Worldview.* Cambridge: Cambridge University Press.

Tejani, B.M. (1973) "Local Significance and the Importance of the Local Audience in Modern African Writing: Studied in Ngugi, La Guma, Mphahlele, Okara and Peters." Ph.D Thesis (Unpub.). University of Nairobi.

Thairu, K. (1975) *The African Civilization: Utamaduni wa Kiafrika.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Thomas, N. (1994) *Colonialism's Culture; Anthropology, Travel and Government.* Princeton: Princeton University Press.

Vansina, J.(1985) *Oral Tradition as History.* Wisconsin:The University of Wisconsin Press.

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

............(2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

Wanjala, C.L. (1978) "Alienation in Modern East African Literature". Ph.D Thesis. (Unpub.) University of Nairobi.

Wa Thiong'o, N. (1970) *Mtawa Mweusi.* Tafsiri. Nairobi: East African Educational Publishers.

.......... (1972) *Homecoming; Essays on African and Caribbean Literature, Culture and Politics.* Nairobi: Heinemann.

......... (1976) *Kesho Wakati Kama Huu.* Mtafsiri. Kiango, S.D. Nairobi: East African Educational Publishers.

......... (1986) *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature.* Nairobi: Heinemann Kenya.

......... (1993) *Moving the Centre; the Struggle for Cultural Freedom*. Nairobi: East African Educational Publishers.

.......... (2004) "Homecoming; Address at The University of Nariobi, August 2004". *The Nairobi Journal of Literature. The Journal of the Department of Literature*. University of Nairobi. (3) pp 62-67.

Wa Thiong'o, N. na Micere, M. (1978) *Mzalendo Kimathi.*Mtafsiri. Kahaso, R. Nairobi: Heinemann Educational Books.

Wa Thiong'o, N. na Wa Mirii, N. (1982) *Nitaolewa Nikipenda.* Mtafsiri. Kabugi, C.M. Nairobi: East African Educational Publishers.

White, L. (1943) "Energy and The evolution of Culture". In McGee, R. J. and Warms, R. L. (eds) (2000). *Anthropological Theory: An Introductory History*. 2nd edn. New York: McGraw Hill. pp. 243-262.

Zaja, J. O. (1986) "Fasihi Tafsiri Katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili; Matatizo na Athari Zake". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.

EAST AFRICANA COLLECTION



JOMO KENYATTA MEMORIAL LIBRARY